

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, LAMU WEST
CONSTITUENCY, HELD AT MPEKETONI CATHOLIC CHURCH**

ON

30TH APRIL 2002

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, LAMU WEST, MPEKETONI HELD AT MPEKETONI CATHOLIC CHURCH ON 30TH APRIL, 2002

Present:-

1. Mr. Ahmed I. Hassan - Commissioner
2. Dr. Mosonik arap Korir - Commissioner

Secretariat in Attendance

1. Treza Apondi - Programme Officer
2. Carolly Okeyo - Asst. Programme Officer
3. David Muturi - Sign Language Interpreter
4. Asha Boru - Verbatim Recorder
5. Mohamed Abubakar - District Coordinator

The meeting started at 9.35 a.m. with Mr. A. I. Hassan in Chair.

Prayer was conducted by Father Daniel Karau of the Catholic Church

Mungu wetu ni asante kwa vile umetujalia tukaweza kusanyika hapa siku ya leo. Wewe umetuumba ukaumba ulimwengu mzima na kuweka sheria yako, sheria inayo muuongoza kila mwanadamu na kila kiumbe na majira yake, umetujalia akili yakuweza kuunda sheria zetu ili tuweze kuwa na mwongozo mwema, tunakuomba tunapo jadiliana siku ya leo katika ukumbi huu kuhusu sheria inayo tukabili katika nchi yetu ya Kenya sheria ambayo intuongoze tukaweze kuangazwa na sheria yako ili ikaweze kutuunganisha, yale yote mtaleta kuchangia asubuhi ya leo yakaaweze kuwa ya manufaa kwa kila mwananchi wa Kenya ili kwa pamoja tuweze kuishi kwa kuelewano umoja na upendo, tunaomba hayo kwa jina la Yesu Kristo, Amen.

Mohamed Abubakar – District Coordinator - Kama nilivyo eleza second tuta introduce mfahamu vizuri kwa hivyo upande wangu kule, (kule) kabisa tuko Kamiti members wa Lamu West Constituency anaitwa Kassim Rahman, huyu ni mwenyeji wenu mnamu fahamu vizuri ni Mwalimu, huyu hapa ni kama kuna wale mabubu basi atawasaidia kwa sign language, nafikiri jina atayatamka yeye vizuri zaidi.

Jina langu ni David Muturi mimi ni sign language interpreter.

Mimi mwenyewe ni Mohamed Abubakar, District Coordinator wa Lamu District na kushotoni kwangu yuko Programme Officer majina atatamka yeye vizuri.

Treza Apondi: Hamjambo, mimi kwa majina naitwa Treza Apondi nafanya na Constitution of Kenya Review Commission as a Programme Officer.

Com. Hassan: Habari zenu mimi kwa mjina naita Ahmed Issac Hassan mimi ni Commissioner Constitution of Kenya Review Commission.

Com. Mosonik: Mimi ni Mosonik arap Korir, ama Dr. Mosonik, Commissioner.

Carolly Okeyo: Habari ya asubuhi, mimi naitwa Carolly Okeyo mimi ni Assistant Programme Officer.

Asha Boru: Habari zenu, mimi ninaitwa Asha Boru Verbatim Recorder.

District Coordinator: Kwa hivyo bila kupoteza wakati tutaendelea na programme, yule ambae yuko na maoni nafikiri karatasi yetu inazungumza hapa uko na maoni, kama ni oral utazungumza, kama ni memorandum utazungumza utuwachie karatasi yako, na ukija hapa tafadhali upatie majina yako kamili na baada yakuzungumza utajiandikisha na utie sahihi kwa Madam Treza, Commissioner endelea.

Com. Hassan: Wananchi wa Mpeketoni tunawakaribisha kwa hii kikao leo cha Constitution of Kenya Review Commission, leo ni siku ya pili tunakaa hapa Lamu West Constituency kwa kawaida tunakaa kwa kila constituency siku mbili jana tulikuwa Lamu Town na leo tuko Mpeketoni ni leo itakuwa mwisho wa Lamu West Constituency kutoka hapo kesho tutakuwa Lamu East. Kwa hivyo kabla hatujaanza nilikuwa nataka kuwapatia rules ya hearing yetu, mtu akikuja kutoa maoni tunataka ajitambulisha aseme jina lake, kwa sababu tuna rekodi hii kitu kwa njia ya redio tunataka kuchukua makaseti kwa hivyo unaanza na jina lako, ni hile kikundi ambae unawakilisha ikiwa wewe ni kutoka kwa kikundi ama wewe ni kuzungumza wa binafsi lazima ujitambulisha. Halafu pia ukimaliza kutoa maoni utatuandikia kwa register jina lako, address yako na kila kitu hapo (hivyo) signature, kwa hivyo hiyo ni rule ya kwanza.

Ya pili kama wewe uko na maandishi umeshaandika, utatupatia hiyo maandishi pia, na hatukubali wewe usome hiyo maandishi neno kwa neno kwa sababu hiyo itachukua muda mrefu sana tunataka mtu aseme ile main points, a highlight ile main points ambaye hiko kwa hiyo memorandum badala yaku soma neno kwa neno na atupatie hiyo memorandum na huyo mtu tutampatia dakika tano afanye hivyo. Kama ambayo hauna memorandum ambaye umeandika na unataka tu kutoa maoni pia unakubaliwa utakuja pia na utoe maoni kwetu. Na tunaomba saa zile unatoa maoni watu wengine tunataka wampatie mtu nafasi aongee kila mtu ako na haki yakutoa maoni yake, hata kama haukubaliana na yale maoni anatoa ni haki yake kutoa maoni kwa hivyo, hatutaki mtu awe anafanyiwa heckling ama booing. Kwa hivyo ni lazima tumpatie mtu heshima yake atoe maoni yake ndio ye pia aweze kusikiza wakati unatoa maoni yako, hiyo pia ni rules ya hearing hii, kwa hivyo, nataka kwanza tufahamu hiyo basic

rules kabla hatuja anza hii hearing.

Sasa tutaanza na Emmanuel Kamau, Emmanuel Kamau, karibu Emanuel.

Emmanuel Kimani: Okay asante sana, kwa majina yangu si Kamau ni Emmanuel Kimani.

Com. Hassan: Kimani?

Emmanuel Kimani: Ile nataka kuzungumzia yangu kama kwa maoni ninafikiria zile powers President anazo, nafikiria hizo ndizo imeshika mambo yote hata mambo ya pamba na kila kitu ambaye tunaweza kuzungumzia kwa leo kwa hivyo, kwa maoni yangu kwa ufupi, nafikiria zile powers kama zinge gawanywa kwa wale wakubwa ambaye kama kwa mfano (inaudible) wamechuga wao, kwa vile kikundi kwa mfano ni Commission ama ni Attorney General, wale kama ni ma Judges wawe ndio wawe ndio wanamchagua Attorney General, kama ni kwa mfano kama University Rais asiwe ni mkubwa wa asiwe Chancellor, iwe ni wale wa kule kama Universities wawe ndio wanachagua Chancellors. Rais asiwe anachagua kama ni mtu wa uchaguzi kama Commissioner wa uchaguzi maanake sioni vile unaweza kumchagua mtu asimamie uchaguzi halafu yule mtu asikuchague wewe, kama anauwezo. Halafu kitu nyingine sioni kama vile Commission vile inaweza kubalidishiwa maanake hizo powers ambazo itandikwa kabla hii mambo tunasema saa hii.

Points ingine naongea, ni kuhusu World Bank I.M.F. mimi kulingana na vile nafikiria nchi yetu tunachukua loan, taxation ambaye tunatoa ambaye tunaweza kujistahimili hapa nchini, kwa hivyo kama ni mwana Kenya, mimi nafikiria zile taxi ambaye tunatoa ikitumiwa vizuri itaweza kutengeneza kwa uchumi wetu. Hatutaki kuwa manipulated na watu wa nje, watufanye maskini halafu wachukue mali ile ambaye tunao wawe wanapeleka kule kwao. Mimi nina hayo maoni mawili tu.

Com. Hassan: Tunashukuru asante sana, Wa pili ni Bw. Fredrick Mwangi

Fredrick Mwangi: Asante sana Commissioners kwa shuguli hizi za leo. Maoni yangu ya kwanza inakuwa ni kuhusu uchaguzi wa Rais. Ningependekeza qualifications za Presidential candidates, awe ni raia wa Kenya, awe ni amejandikisha katika sehemu za uwakilishi Bungeni na pia awe na support ya chama cha kisiasa, pia awe na elimu awe amehitimu kwa shahada ya degree ya Economics katika moja ya vyuo vikuu, pia awe na umri wa miaka arobaini hadi miaka sitini na tano hizo ziwe qualifications za Presidential candidates wa Kenya. Halafu matokeo ya uchaguzi huo atakaetangazwa kuwa Rais wa Kenya awe amepata asili mia hamsini na moja ya kura zote ambazo zitakuwa zimepigwa Kenya.

Sehemu nyingine ni uteuzi wa Baraza la Mawaziri, Baraza la Mawaziri (inaudible) kuteuliwa kulingana na (inaudible) katika Bunge kulingana na maoni yetu yateuliwe katika wanaweza kutoka nje ya Bunge ndio waweze kupatikana professionals kulingana na taaluma mbali mbali ambazo zapitakitana katika Ministries.

Halafu jambo lingine maoni mengine ni kuhusu criminal proceedings ikiwa President atafanya makosa wakati yuko kwa mamlaka lazima afikishwe Mahakamani na ashitakiwe kulingana na sheria, sheria iwe ina wanasilimisha wana Kenya wote bila kujali huyu ni nani wala ni nani.

Halafu shida nyingine ni uteuzi wa Makamu Rais. Makamu wa Rais kulingana na sasa anateuliwa na President. Mimi ningependekeza Makamu wa Rais achaguliwe na wananchi moja kwa moja na qualification zake, ziwe ni kama zile za President.

Halafu sehemu nyingine Bunge lazima iwe huru. Bunge iwe na kalenda maalum ambayo itaelezea inaanzia wapi na inaishia wapi, isiwe ni secret weapon ya mtu moja ambaye atakuwa anavunja Bunge wakati anataka ama ana prorogue vile anavyo taka yeye. Kwa hivyo pamoja na hayo upande wa wakulima hizi industries ambazo zinahusiana na mazao badala yakujengwa town, ziwe katika areas hizi ambazo production (inaudible) ambazo zinakuzwa, tuseme kama hizi textiles na kama hizi cashewnuts industry vitu kama hizo. Na pia Co-operative Societies ziwe empowered zaidi ili ziweze kusimamia wananchi kwa njia inayo stabili.

Mambo ya liberalization pia ziangaliwe kwa sababu imeumiza sana wakulima. Wakulima wawe na power zaidi kuliko kutegemea middlemen ambao wanaangamiza wakulima. Hayo ndiyo niliyo nayo Commissioners asanteni sana.

Com. Hassan: Asante sana bwana Mwangi tafadhali utuwekea kidole hiyo register. No 3 atakuwa ni Sylvester Mutegi

Sylvester Mutegi: Asante sana Commissioner, wananchi watukufu wa Kenya, mbele yangu kwanza ningepomba ukiwa katika Katiba yetu kuna provision yoyote ambayo inahusu mambo ya pesa ningepomba Kenya pound isitumiwe maana hakuna ma currency International ingine ambao inatambulikana.

Tukiingia katika wafanyi kazi wa Serikali, wanalipwa kulingana na Kenya Pound ambaye imeleta confusion haya mambo yakiingia katika hali ya International World. Jambo lingine ambalo ningepomba kuwa wafanyi kazi wa Serikali wanafanya kazi nzuri sana na ngumu lakini ikingia wakati wa kuretire wazee wanaumia sana, mtu amefanya kazi miaka arobaini na zaidi akija kuretire anakaa miaka mitano wengine wanakufa kabla hawajapata pension yao hii jambo Commissioners irekebishwe.

Jambo lingine ni tuseme jeshi letu mkuu, jeshi liwe na group na ningepomba kusiwe na mahali ambapo kuna ingia aina yeyote ingine ya jeshi ambao halitambulikani. Kama juzi tunasikia habari ya vikundi kadha kadha kama jeshi la mzee, sijui kingole mambo kama yale yananyima jeshi letu nguvu na vile vile tunajua katika Kenya tuna youth moja ambaye tunaita National Youth Service imeingia kwamba kuna kikundi nyingine asa iwe siasa iwe ni DP iwe ni KANU kina kuwa na youth yake, hii youth inaleta tatizo katika nchi na wanakuwa na nguvu mpaka wana jeshi wetu hawawezi kufanya kazi yao vile instabili. Kwa hivyo, katika Katiba yetu, hile jambo litiliwe mkazo.

Jambo lingine ningeomba Wabunge ambao Tumewachagua hata kama tunawapenda namna gani iwe wanaenda kwa mizimu miwili, miaka mitano mitano, ikiwa ni mzuri sana apumzike kwa muda ingine mitano tunachagua tena ili awe na wakati wakuangalia wananchi wake.

Jambo lingine ambalo linakera sana wanaKenya ni kuwa Tumepatiwa kitambulisho mimi ni mwanaKenya nimezaliwa hapa na vile vile naitwa squatter, jambo hili la squatter ni jambo ambalo linaumiza sana, maana inaonekana hata refugee ni afadhali kuliko squatter maanake refugee anahudumiwa na chama cha kile cha UN lakini squatter nani anakuangalia? Kwa hivyo ikiwa kuna wanaKenya kusiwe na mwanaKenya anaitwa squatter.

Jambo lingine ambalo linatukera sana vile vile ni kuwa tumesahau marginal population ambao inatokea tokea. Watoto wetu wamekuwa machokora na huku tunasema tunalinda wananchi. Hao machokora wanaaibisha taifa hata na uongozi wa nchi, kwa hivyo, kwa maoni yangu ningeomba hawa watoto wa mitaani katika Constitution yetu tujaribu kuangalia vile tunaweza fanya ili waweze kutoka mitaani na wahudumiwe ipasavyo.

Jambo lingine ambalo ningetaka kutia mkazo kidogo ni yakuwa nchi yetu ni ukulima na tunategemea kilimo. Natunajua kilimo ni uti wa mgongo wa nchi yetu lakini ukiangalia vile tuna tuma nchi yetu hairidhishi. Maji tunayo yakutosha, mito iko kama hapa, tuna Mto Tana. Kuna mto Athi na ukiangalia maji yake yote inapotelea baharini. Tungeomba Serikali isaidia katika wakati wakuunda hii Constitution tuone haya maji yetu hayapotei itumiwe kwa kuhudumia wananchi.

Jambo lingine ni ya kwamba tunaingia mambo la uchaguzi na uchaguzi ni muhimu lakini tukiangalia tunaona kuna watu hapa wana nyimwa haki yao yakuchagua watu, kwa mfano, mtu ni mgonjwa yuko hospital sidhani huyu mtu kama akiruhusiwa kupiga kura yake pale alipo ataweza katika hospitali aende ingine pahali apige kura? Vile vile kuna hawa watu wa kwa Jela wako kule kwa rehabilitation na tunatarajia wakitoka watakuwa ni wazuri kwa nini asipatiwe nafasi yakupiga kura akiwa jela? Vile vile kuna hawa askari ambao wanaenda kusimamia vituo, wengi wao hawapigi kura. Kwa hivyo mimi maoni yangu hawa watu wapatiwe nafasi yakupiga kura ili kujieleza kulingana na vile wanataka asanteni sana.

Com. Hassan: Asante sana Bw. Sylvester, tafadhali piga signature yako, tuliwaomba wale wako kuja wajaribu kujaza form hapo mbele kwa ofisi kwa huyu msichana, hata kama utoi maoni lakini unakuja tusikiliza tafadhali pia ujiandikishe kwa sabaabu tunataka tuwe na rekodi ya wale wamekuja leo hapa. Kwa hivyo, kama unataka kuandika kutoa maoni unasema hivyo, kama unataka kuona tu ku observe pia unasema hivyo, kwa hivyo tafadhali weka jina lako kwa hiyo list asanteni sana. Next ni Nancy Mwarania.

Nancy Mwarania: Asante sana mwenyekiti - Kusimama hapa na simama kwa niaba ya akina mama lakini ninaona hata karibu nje nitoroke kwa sababu sioni kina wakina mama. Sasa ninshangaa nina uliza ni kwa nini? Sasa mimi wakati nina

simama hapa kwa niaba ya akina mama. Unajua mama ni yeye ndiyo mwenye mji na wakati huu ni wakati mwingine wakufanya haraka haraka kama (inaudible) pengine ndiyo sasa wakina mama wana (inaudible) sasa ni kweli sasa mimi hapa maoni yangu nasimama kwa wakina mama kwa shida za kina mama tuna shida sana kina mama kwa sababu sisi wakina mama tuna kikundi na hicho kikundi hiyo ndiyo intusaidia lakini nguvu hakuna, sasa mimi maoni yangu au maombi yangu ni tu saidiwe upande wa Serikali kwa sababu sasa tupate nguvu.

Tena nikingezea kama mimi natoka mashambani (inaudible) vile naongea kwa sababu sisi Tumezoea kukaa huku mashambani lakini nashukuru sana kwa sababu Mungu ananiwezesha nisimama hapa. Sasa nikisema kuna mashida mengine upande wa kina mama, wakina mama kuna wengine wajane na kunashida inaonekana tunajaribu kushikana na ndio sasa ugonjwa inangia kama hawa watoto wa chokora kwa sababu nguvu hakuna, sasa ndio mimi nasema tusaidiwe upande wa Serikali kwa kikundi, sababu kikundi ndio sasa nguvu ya akina mama.

Na nikirudi upande ingine kama upande wa huko nyumbani wanaume mutusaidie tena kufungua akina mama halafu twende kushikana kufanya maendeleo kwa sababu sasa ndio pengine ninaomba sasa upande kwa wanaume. Fungulieni akina mama tushikane kwa bega kwa bega kwa sababu sasa tukikosa kushikana, maendeleo hainekani na maendeleo inatakikana itoke kwa nyumbani tunaishi kuna maendeleo. Yangu wajua nilikuwa ninafikiria mengi sasa nikija hapa inapotea. Sasa maombi yangu ni kama grupu tusaidiwe sana na tuangaliwe sana.

Na tena kama sasa nikirudi nikiangalia kama upande wa akina mama yaani hata akichaguliwa kuwa kiongozi kuna mambo mengine hata mambo inaenda kuharibu kwa mikutano si wengi akina mama wakienda kwa mkutano, na sijuini kwa nini? Na unajua sasa mama na bwana wakishikana mashauri ni mengi, sasa yangu tuangaliwe sana akina mama tusukumwe Kenya twende mbele, kwa sababu tukikosa kusukumwa, mambo itakuwa nyuma ndio sasa tunaone mambo inakuwa sana sasa akina mama waangaliwe sana. Natukiangalia sana kama chokora mambo ya chokora itaisha mimi upande moja ni wajane ninaona tunashida sana. Kuna wengine hana baba nini nini pesa inakosa hata yakupeleka watoto shuleni zina kosa ndio vile tunataka maoni yangu tunataka tuangaliwe sana ni Serikali sina mengi pengine ingine itokee asanteni.

Com. Hassan: Asante sana mama Nancy tafadhali piga signature yako kwa register. Sasa ni wakati wa Father Daniel Karau wa Catholic Church.

Fr. Daniel Karau: . Asante hapo nimeandika Catholic Church lakini mimi niko kama individual I am not representing the Catholic Church.

Com. Hassan: Okay.

Fr. Daniel Karua: Yes, kwa hivyo siyo maoni ya Kanisa ya Catholiki Kenya .

Com. Hassan: Sawa.

Fr. Daniel Karua: ni maoni ya Fr. Daniel, the Priest in the Catholic Church from Mpeketoni Parish.

Com Hassan: You should have written here.

Fr. Daniel Karua: Yes niliona ni baadaye niliona ni

Com. Hassan: You write individual

Fr. Daniel Karua: Yes it is individual, sababu naweza kushtakiwa na Kanisa

Com. Hassan: Sawa endelea

Fr. Daniel Karua: Tunawashukuru sana Commissioners na wale ambao mumeandamana nao na yangu ni haya. Jambo la kwanza nikuhusu Non-Governmental Organisation. Kanisa ikiwa especially Non-Government Organisations ambazo they are non profit making bodies. For example, kwa mfano kama ni vitu vinahitajika kutokana na hivi vikundi kama wanahitaji vitu kutoka nje ambayo ni kusaidiwa wetu hapa wakubaliwe kuzileta bila tax. Kama vitu vinaagizwa nje kwa sababu kama ni gari ama vitu vyovyote vile vinakuja kwa sababu yaku saidia mwana Kenya, kwa hivyo hilo ndilo ombi ambalo ningeomba kwa upande huo. Makanisa, Wakristo, WaisLamu wa vikundi vyote waweze kukubaliwa kulete kama ni vitu ambavyo vinasidiwa watu bila kusumbuliwa na mambo ya tax kwa sababu hakuna profit yoyote ambao wanafanya kutokana na hivyo vitu.

Ningetaja juu ya Local Governments mambo yakuchagua Mayors. Hili ni oni langu pengine inaweza kufafanuliwa. Mayor achaguliwe asiwe ni wa chama Fulani lakini achaguliwe na watu, kwa sababu gani? Kwa sababu sasa vile tunavyoona kinatendeka Mombasa Mayor Mwahima Mhe. Mayor Mwahima shida alizo nazo ni kwa sababu ati ametoa maoni yake. Sasa anaangamizwa kwa sababu ametoa maoni yake na kwa hivyo, ingehitajika huyu Mayor achaguliwe na wate wa eneo hilo eneo lake ili aweze kuwahudumia na kuwe na muda ambao atahudumia hawa watu. Kwa sababu hawa ma Councillors, ama viongozi wengine, wanachukua nafasi hiyo ku victimize mtu, ni hii ni mtu aweze kufanya kazi afanyie watu kazi sio afanyie watu fulani awaridhishe watu fulani.

Halafu ningeongezea kidogo aliyo sema kuna aliyeongea hapa wa kwanza akasema juu ya mamlaka ama zile nguvu za Rais kwa upande wa ya kwamba ndiye anayekuwa mkuu wa majeshi ili jambo lingeondoka asiwe mkuu wa majeshi kwa sababu hii tukiangalia sana mifano mingi katika Africa kuwa ma Rais wa Africa ndiyo walio wakuu wa majeshi wanafanya nchi zetu hata wakati mwingine zikose kuwa na uongozi mwemwa kwa sababu yale majeshi yanakuwa lazima yawe, they have to toe his line,

that is the problem. Kama vile ilivyotokea Zimbabwe juzi wakati wa uchaguzi wana jeshi wanasema kama Mugabe hatachaguliwa hawata kubali mwingine hawatamkubali kwani wanatumikia Rais ama wanatumikia nchi? Kwa hivyo asiwe mkuu wa majeshi kwa sababu majeshi yanajitambulisha naye. Hiyo niliongezea tu kuhusu zile nguvu za Rais wa Kenya wa Jamhuri ya Kenya.

Halafu kuna jambo lingine kama identification ya mwananchi wa Kenya, kuwa tunapewa kitambulisho. Mimi ni ombi langu ni kwamba mwananchi wa Kenya yeyote aliye pewa kitambulisho awe na right yakupata Passport bila kusumbuliwa. Mtu asisumbuliwe ati unaenda kuambia leta cheti cha nani lete nini lakini mtu awe anapata vile anaweza kupata kitambulisho aweze pia kupata Passport. Mtu awe na uhuru kama unataka kwenda kama kutembea nchi ya ngambo kama tourist kama unataka kwenda kufanya nini use na uhuru uko, lakini isiwe ati Passport ni kwa wale tu wenye pesa. Kwa sababu ukiuliza ni wangapi hapa mlio na Passport na ukitaka kuipata is a very tedious process, very painful one. Kwa hivyo hiyo pia iwe ni sehemu ambayo ni kama kitambulisho cha mwananchi wa Kenya kwa sababu pia unaweza kujitambulisha na Passport . Kuna sehemu nyingi ambazo mtu either unaweza kupeleka birth certificate ama kitambulisho ulicho pata kwa Serikali ama Passport yenyewe ni kujitambulisha wewe ni mKenya.

Halafu jambo lingine hii sijui itaingilia sehemu gani lakini tunajua ya kwamba kumekuwa na Rais ameteuwa Commissions nyingi za Enquiries, Commissions nyingi na hizi Commissions zote zinatimia pesa za wananchi, taxpayers money na drafts za hizi Commissions hazitolewi. Kungekuwa na kipengele Katiba yetu ambacho kina sema hizi Commissions zikiteuliwa lazima matokeo yake yajulishwe wananchi, kwa sababu mambo haya yameendelea, Commissions zipo ndio results zimetolewa lakini bado ziko na mtu fulani mahali fulani anashikilia hatujui ni nini kilicho endelea watu walisha lipwa na pesa za zetu na kwa hivyo hayo mambo yanabaki hivyo, Hilo ningeomba liwe ni jambo moja ambapo tutajulishwa matokeo ya hizo Commissions.

Halafu la mwisho ni juu ya Political parties zetu ni Katiba inge ningeomba kingeweza kutenga ni how many political parties should be there. Lakini sasa tukiacha hivyo it is open hata mimi nikitaka kutengeneza political party yangu nitatengeneza, yule mwingine akitaka kutengeneza sasa sisi we are totally confused. There are almost fifty political parties in Kenya now na kwa hivyo, hatujui namna ingawaje tunasema ni democracy lakini kuna wakati itaepukana itaendelea hivyo kila nyumba iwe na political party yake, so unless kuwe na mpangilio ya kwamba tunahitaji mimi I would suggest that we have three political parties in Kenya just three of them. Political party tatu ambacho ili kukiwe na kwa sababu kusiwe na huu kwa sababu hata zingine zimejengwa katika msingi ya kikabila. Ni ipi itatusaidia ili watu waweze kuwa hizo tatu makabila ni mengi Kenya na kwa hivyo, haitwezekana kila kabila iwe na political party yake, kwa hivyo yangu ni hayo asanteni sana.

Com. Hassan: Thank you very much just hold on.

Com. Mosonik: Question, Swali moja umesema Rais asiwe Commander-in-Chief , lakini ningependa kukuuliza hata Rais wa America ni Commander-in-Chief? George Bush Junior ni Commander-in-Chief ndio akatuma jeshi Afghanistan tofauti ni gani?

Fr. Daniel Karua: mimi ndio maanake nikasema hapa haitaji kufanuliwa kidogo, lakini tofauti ile tunapata ya kwamba kama sasa upande wetu wa ki Africa yeye mwenyewe ndio mwenyewe anaweza jeshi lifanye hivi bila hata consultation ya mtu yeyeto I am ready to be corrected in that sense.

Com. Hassan: Okay thank you very much Father Daniel. Our next person is James Kimani.

James Kimani: Mwenyekiti wa Commission na wananchi hamjambo?

Crowd: Hatujambo

James Kimani: Mimi swala ambalo ningependa kutoa kwa Commission ambaye iko mbele yetu hapa ni kuhusu elimu. Kenya nafikiri tangu mwanzo Tumetajiwa kwamba elimu iko inaenda free, education is free we are told education is free. Nina weza kuuliza inaenda free, how free is free? Na nikiangalia maswala mengi kama vile sisi tulivyo hapa wakulima tunashugulika kutafuta karo za shule tunakuta kwamba tumetazika tukitafuta hiyo free education na hatuja ipata kwa hivyo kama ni mKenya tuneweza kupendekeza kwamba sisi watoto wetu waweze kusoma bila malipo haswa kwa masomo ya msingi iwe ni right ya mtoto bila malipo, ili hawa watoto wasije wakayumba nyakati kama ulo mwanzo na ndio maana tunajikuta kwamba watoto wetu wengi wanaenda kujitafutia karo wenyewe na kama mzazi hawezi, mtoto ndiye anaenda kujitafutia karo ili aweze kusoma, anajitafutia haki mwenyewe. Kwa hivyo mimi ningependelea sana kama nyinyi mukienda kupendekeza swala hilo msem kabisa tunahitaji elimu iwe bure kwa watoto wetu ili waweze kusoma. Ni machache mimi siko na mengi yakusema.

Com. Hassan: Okay asante sana Bw. Kimani. Our next person is sasa huyu Priscilla is she an observer or she wants to give views? Priscilla Karanja, unataka kutoa maoni ama umekuja tu kuhudhuria kikao?

Priscilla Karanja: Natoa kidogo.

Com. Hassan: Basi ungeandika kama unatoa kwa sababu sioni kama umeandika kitu (inaudible).

Priscilla Karanja: Mimi maoni yangu ile niko nayo ni kuhusu wasichana

Com. Hassan: Endelea

Priscilla Karanja: Maoni yangu ile niko nalo ni kuhusu wasichana kwa vile kuna wakati tunasikia msichana anapatwa na problem ya raping akienda kwa korti hiyo mambo inapigiliwa hivi, hivi halafu napotelea bure, kwa hivyo kitu nigeonelea msichana akiwa na raping yaani Judge awe ni mwanamke ndio azingaitie ile mambo vizuri kwa sababu tunajua raping kuwa ina haribu msichana ama mwanamke. Kwa hivyo, mimi huwa ninaumia nikisikia mambo hiyo ya raping imeenda hivi hivi ikaisha.

Halafu ingine kuhusu msichana ama mama na jua kawaida tunaolewa mtu akisha olewa inakuwa nyumbani kwao kule ametoka hakuna nafasi anaweza kupata, baba anashamba na anasema kule ameolewa basi kwa hivyo nikiuliza naweza kusema akiolewa ana nafasi yake mpaka nyumbani kwa sababu yeye amezaliwa na baba yule na mama yule na yule kijana amezaliwa pamoja anapata kitu kwa baba, kwa hivyo ningelizwa nigesema mpaka msichana awe na nafasi yake kwa mzazi wake. Ndio akipatwa na shida hata akija nyumbani mzee pengine amekufa anafukuzwa na wale ndugu zake na akiwa nafasi yake ataondoka aende pahali pake na hakuna problems atakao ingia yangu ni hiyo.

Com. Hassan: Asante sana Priscilla, tafadhali tupigie kidole hapo register. Next is Patrick Kariuki. Patrick Kariuki you are from the Task Force, which Task Force is this?

Patrick Kariuki : From Civic Education Providers

Com. Hassan: Okay

Patrick Kariuki: Asante ma Kamishna. Maoni yangu kwanza nitaangalia upande wa Judiciary. Kulingana na vile ilivyo wala ambao wanaenda Mahakamani ni wale ambao wana pesa, kwa hivyo mimi nikiomba ndiyo kila mtu apatenafasi yakwenda Mahakamani, zile pesa ambazo zinatozwa either zipunguzwe na ikiwezekana zitoke kabisa. Na hiyo pesa ambazo zinalipwa wakati una appeal ama wakati unataka kufile case. Pia kitu kingine wale Ma Judge wasitowe vitu vyote uamuzi na ningomba kuwe na ofisi ingine ya Ombudsman ambae atakuwa anangalia shuguli ambazo zinaendelea Mahakamani kwa mfano kama pengine mumeenda kortini na mtu pengine amekuzidi pesa kidogo kuhakikishwe ya kwamba kesi yako hukuumizwa upanda moja kwa hivyo Ombudsman atakuwa nashugulikia ule mtu ambaye haijiwezi kuseama.

Kisha kitu kingine utaangalia upande wa Executive, kwanza kabisa President amepewa fursa ku appoint watu wengi sana ma Judge na Judges of High Courts, Courts of Appeal na wengine wengi. Sasa mimi nitapendekeza azidi ku appoint lakini Bunge ithinishe, ithinishe na ikiithnisha iseme mtu fulani haifai kuotaka kwa sababu fulani Rais awajibike kuteuwa mwingine ambae atakubalika. Pia ukiangalia kwa sasa Rais hakuna njia ya muafaka, ya ki halali ya kumtoa Rais kwenye kiti. Kwa hivyo ningeliomba Katiba itoe njia ya muafaka mabayo inweza kumtoa Rais kwenye mamlaka. Na circumstances ambazo zitamuezesha Rais kutoka mamlakani ni ikiwa gundulika ya kwamba ametumia vibaya pesa za uma, ama natural resources ametumia vibaya pia zingine ikiwa amepatikana na kosa yaku rig votes, halafu hiyo ingine anatomia mamlaka yake vibaya na pengine akiwa na ugonjwa (inaudible) sasa kumtoa kuwe na Commission ambaye ni Korti na ambae ni non partisan ambao ita determine ya kwamba Rais atatoka katika mamlaka.

Kisha qualifications za President Presidential candidates ziwe kama zifuatavyo: Kwanza Kenyan by birth, ya pili a University graduate with a minimum of Diploma in Economics, ya tatu awe na minimum na maximum of 35yearsrespectively pia awe na record mzuri kwa muda wa ambao miaka ishirini tano imepita, nyuma ichunguzwe at least 25years ndiyo haikishwe

kama hana criminal yeyote, pia Rais asiwe Member wa Parliament.

Kisha kitu kingine ambacho tunaangalia ni Land and Property Rights. Mimi ningeonelea ya kwamba kila mtu ahakikishiwe vile anaweza kupata ardhi, na pia kitu kingine Katiba ya sasa unaweza pata shamba yote ambayo unataka provided you have money. Mimi ningeomba Katiba iweke, kiwango kulingana na idadi ya watu ambao iko ndio kuwe na maximum land ambao unaweza ku acquire kama una pesa nyingi usipitishwe hapo. Na pia kitu nyingine mtu awe anaweza kupata shamba pahali popote mradi hatapitisha kile kiwango ambacho kile kimewekwa.

Kisha kitu kingine ambacho ningeangalia ni Constitutional Supremacy. Kwa sasa waBunge wamekuwa na mamlaka yakubadilisha yaku amend Constitution, na tumeona kwa mfano hii Katiba ambao tuko nao imepoteza sura yake ile ya kwanza.

Kwa hivyo ningeonelea kabla Bunge haija amend kitu chochote cha Katiba, mwanzo consult watu through referendum, ya pili waBunge wasiwe na mamlaka yoyote yakubadilisha kipengele ambacho kinawaadhiri watu kwa mfano, human rights, kipengele ambacho kinahusiana na haki za binadamu na Land and Properties Rights, hiyo ni mpaka kiangaliwe kindani kisipitishwe. Na hii Katiba, yetu ningeonelea kuwa na Commission mahali ambao ni huru ambao itakuwa inaangalia hii Katiba yetu haitakuwa abused na hii Katiba among others ningependekeza kuwe na religious leaders, ambao na waKenya na pia ni reputable political leaders ambao ni Kenyans, hawa ndio waweze kuangalia Katiba yetu ikawa manipulated na Parliament.

Halafu ingine ni electoral processes, kwa fursa, President anakuwa declared winner kama pengine ameshinda tu kura, mimi maoni yangu nilikuwa ninaonelea President lazima awe amefikisha nusu ya votes zote ambao zimekuwa voted na kama pengine hakuna mtu amefikisha kama pengine walikuwa wanapigania wanne, number one and number two waingie tena mpaka kupatikane yule ambae anafikisha 50% ndio aweze ku lead majority awe hapo amechaguliwa na majority.

Halafu ile rule ambao inasema President lazima awe na 25% representation in at least 5 provinces hiyo ningeomba iondolewe kabisa. Na pia defection from parties and party crossing the floor hiyo ningeonelea ki Katiba ichukuliwe kwamba ni uhalifu kuhama hama vyama, Katiba isi ruhusu watu kuhama hama vyama. Pia ile ambao current geographical Constituency system ambao tuko nayo, ningeonelea ibadilishwe tena na wakati inaundwa kuzingatiwe wingi wa watu, kwa sababu unakuta Wabunge wengine wamechaguliwa na watu kidogo na wengine wamechaguliwa na watu wengi na wakienda Parliament ambapo wana represent watu unakuta votes ni sawa ikifika mahali pa kuinua mkono. Ni hayo tu asanteni.

Com. Hassan: Asante sana Bw. Patrick Kariuki. Joseph Munene. Munene from Civic Education Programme.

Joseph Munene: Asanteni sana walio ma Commissioners na wageni wengine wote waliokuja leo siku ya leo kusikiza maoni ni karibuni. Yangu nafikiri si mengi ni kidogo tu hata ingawa nafikiri ningeandika katika (inaudible) Lakini ningependa ile ingine incase kuna mtu ambae angependa kutoa maoni individual ama mengine yote anaongezea. Mimi yangu ni upande wa Rais, Rais kusema kweli katika Katiba yetu ambao sasa unakuta kuna upande ambao watu citizens wenyewe wanachagua wana elect a

Member of Parliament. Halafu kuna watu wengine wanachaguliwa na Rais. Ni ajabu kwamba unakuta mtu aliyechaguliwa na watu wenyewe atakuwa yuko weaker more weaker than a D.C.

District Commissioners ana nguvu kuliko hata Mbunge hata Chief, mtu kama Chief ana nguvu kuliko mtu ambae anachaguliwa na watu ama Councillor. Councillor mtu ambae tunaona anakuja ameletwa na watu kwamba awaongoze na anajue maslahi yao na shida zao anajua yeye, lakini unakuta Chief ana power. Kwa hivyo ningependa pengine kama inaweza kubadilishwa hiyo mambo ya Rais iwe kwamba Katiba yetu ibadilishwe ya kwamba inaweza kutegemea watu ambayo Tumechaguliwa wenyewe kama vile mwenzangu moja anasema kwamba pia Vice President na mambo kama hayo, yote hawa watu viongozi wote hawa hata Mayor.

Jambo lile lingine ni upande wa the Three Arms, hii mambo ya Judicial, Executive na Parliament ni kwamba (inaudible) ni kwamba unakuta imeingiliana Rais ndio juu ya kila kitu, kwa hivyo hata saa akisema (inaudible) aseme tu saa hii kwamba wanajeshi waingilie watu waanza kuchapa watu ndio wahaingaike watahaingaishwa. Kwa sababu (inaudible) unakuta hakuna pengine upande kama hakuna Katiba zingine kama za South Africa kuna section zingine kama Commission zingine zakuangalia maslahi za watu, kama hii opportunities from the employment section ama sector, unakuta kwamba kuna watu wanaangalia zile haki za kila moja ambae lakini unakuta hapa nchini kuna watu wakupatiwa kazi na kuna wengine hawapatiwi. Pengine utakuja ingia kwa mambo kama hayo kwa hivyo tungependa pengine iangaliwe mambo gani (inaudible) asanteni sana.

Com. Hassan: Thank you very much. Sasa tunataka kumuona Peter, Peter Mbui

Peter Mbui: Commissioners na muheshimiwa mlokuja hamjambo?

Crowd: Hatujambo

Peter Mbui: Asanteni, labda maoni yangu si mazito sana na si mepesi sana. Naye Katiba ya Kenya zamani hapo mbeleni ilikuwa imekuja hasa chama cha kitawala, kilikuwa kimwezesha mambo matatu; elimu, magonjwa na umaskini na mambo hayo hayakutimizwa hata leo, nawauliza sasa tunapokwenda kutengeneza sasa tujaribu kuona tume pata elimu kama umesemwa hivi nilipata elimu kwa watoto kuanzia standard one mpaka nane ama kuendelea juu bure, kwa sababu tunalipa pesa.

Pili ni mkulima, mkulima amekuwa ana lima tu na tunasema kuna Serikali anatutafutia bei labda anatutafutia mambo mengine lakini hakuna chochote kinacho patikana kwa mkulima anasahaulika mtu anakuja kukuambea nataka mimea wako na shillingi kumi, hiyo Serikali itupe macho sana kuona hakuna kitu mkulima apate chochote (inaudible) tuko na Serikali wakulima hawa wamelima pamba wamelima chochote lakini Serikali imemtia ndani (Inaudible) mali yake na bei inayofaa.

Tatu ni Afya, yaani ninaposema afya ukienda hospitalini utasikitika sababu utakuta watu wanasema hakuna dawa, jambo la

kusikitisha sana ukienda sasa utaambiwa hakuna dawa, na tunatoa pesa kila siku, tunatoa nchi nyingine (inaudible) kwa hivyo mambo kama hayo yaimizwe laikini zaidi ukulima uwe kuna Serikali imetushika mkono (inaudible) kuhakikisha mkulima amepata kinacho faa.

Ya nne ni kuhusu haya madaraka yamesemwa hapa katika ofisi hiyo ya mtukufu, ni jambo la kusikitisha na lakuhuzunisha ikiwa Rais anaweza kuwa na ma Minister sita katika safari, ma Ministers kumi na sita hawa utakuta night out ni pesa ngapi hizo, ni pesa nyingi ambako zaweza kuandika watu kumi au watu ishirini kwa hivyo hili nalo lichunguzwe sana na wakati anakwenda safari za nje iwekwe kiwango ambako iko na watu wawili ama watatu badala yakuchukua watu kumi pesa nyingi sana night out ukitizama. Kwa hivyo mambo kama hayo ndiyo nilikuwa nayo. Nina mengi lakini mengi yamesemwa na watu asanteni sana.

Com. Hassan: Shukrani mzee Peter, tafadhali tujazie hapo form. Michael Kamau.

Michael Kamau: Nashukuru sana (inaudible) hii maoni yangu nataka yachukuliwa kama yangu binafsi. Mimi kulingana na maoni yangu ama vile navoonelea nitaongea kuhusu electoral system yetu na (inaudible) kama mwenzangu ilivyo sema hapo mbeleni mimi naona kwamba Mayor ama mma Chairmen wa Councils, wawe wakichaguliwa na watu binafsi raia na kama mwenzangu alivyosema hapo mbeleni, maoni yangu vile vile ni kuwa asiwe ni wa chama chochote kile kwa sababu tumeona katika Kenya yetu leo hii mvurugano wa ma Mayor kulingana na vyama, tunaenda tunakupata mtu ambaye pengine amewekwa pale na amewekwa pale kwa sababu ya chama si kwa sababu yakuwa ana uwezo wa kudeliver the services. We need kwa hivyo ningenelea maoni yangu ya kwamba Mayors wawe ni watu ambao hawako katika chama chochote kile na wanachaguliwa direct na raia, awe na elimu pai kuanzia form 4 na kuendelea.

Nikija upande mwingine nitaongea kuhusu defection, mimi naonelea kwamba wabunge wana defect pengine Tumewachagua na wameenda katika Bunge halafu pengine ameamua ku defect awe haruhusiwi kupigania kile kiti tena, awe ata kaa kwa muda wa miaka mitano halafu anapigania kile kiti, baada yakuwa ame defect kwa sababu tunaonelea katika experience ambazo tumepita hapo mbeleni Tumegunduwa kwamba wabunge wengi ama na ma Councilors wengi wamekuwa kuwa waki defect kwa sababu (inaudible) yao wenyewe sasa wanataka kudefect kwa sababu wamekuwa promised pesa ama vitu kama hizo. Vile vile vyama vyetu naongea pia kuhusu chama, maoni yangu ya vyama vya Kenya viwe ni vichache Katiba yetu ieleze kuwa tutakuwa na vyama kama vitatu ama vine ambavo vitakuwa recognized. Tusiwe na vyama vingi maanake vyama vimezidi kuwa vingi mpaka sasa tunaona kuna vyama vingine vidogo, wengine wana form vyama tu, akipata support kidogo pengine anajiuza ama ji solve tu kwa minajili ya kikabila.

Kuhusu ardhi, ningependa wa Kenya wote wawe na urithi sawa kama ni msichana au ni kijana wakati tunapo rithi ardhi kutoka kwa familia zetu ama baba zetu, tuwe tunaangaliwa sawa tuwe tunaangliwa mimi ni mtoto wa fulani isiswe kama ni vijana kama tunafuata mila zetu za ki zamani kwamba ni lazima vijana peke yake wapate uriithi.

Halafu kuna marginalized groups kama hapa kwetu Lamu tuna watu kama wa Boni wameweza kuishi katika ardhi zao kwa muda wa miaka mingi sana na wakati unapo fika umilikaji wa ardhi tunakuta kwamba ardhi zile zao watu hapo pengine sehemu za Nairobi ama katika ofisi kuu za ma ardhi, hawawezi kuelewa watu kama wale na wakati ardhi zinapo peanwa watu wale they are not considered wana kuja kuambia ardhi hii ina belong kwa mtu fulani na hao wameishi pale kwa miaka mingi, kwa hivyo Katiba yetu iwe inaelezeya kwamba kuna ile marginalized groups wajaribu kuangaliwe haki zao za urithi wa ardhi. Halafu vile vile tusi ruhusu wageni kumiliki ardhi zetu, wageni ni watu kutoka non-citizens wasiruhusiwe kumiliki ardhi.

Langu la mwisho ningependa Katiba yetu ielezee ama ifafanuwe hasa ni Ministry ngapi ambazo Serikali inaweza kuwa inazo, isiswe Tumeachiwa uhuru Rais kusema tu leo hi anaweza ku appoint Ministers ishirini kumi na nanae au ngapi, Katiba inaelezeya kwamba Ministry fulani fulani na fulani iwe ndio ziko katika Katiba yetu.

Na mwisho ni kura ya maoni hii ambayo itafanyika baadaye ya Katiba yetu itengenezwe halafu ita referendum that is what I mean iwe yale maoni wale watakao chukuliwa yachuliwe in the District si lazima tuchukuliwe watu wachukuliwe wapelekwe Nairobi Wabunge maanake the percentage kwa sababu ni kura wale wana weza kuwa manipulated wakapiga kura zao kulingana na vile sababu vyama ama there are some people wana weza kumanipulate because of their selfish end katika Katiba yetu. Asante.

Com. Hassan: Asante sana hebu ngoja kidogo.

Com. Mosonik: Ningependa kukuuliza kama ungepewa kazi yakupunguza vyama vya

Ki siasa viwe ni vitatu vile ulikuwa umesema ni vitatu vipi? Kama sasa Tumesikia tuna vyama kama hamsini, vipi vitatu? Yaani criteria of reducing them to three.

Michael Kamau: Kama sasa, kama wakati huu mwa mfano tuko na vyama ambavo vina wabunge wengi katika Bunge letu, tunaweza kuchukua (inaudible) kuangalia ni vyama gani vina support kubwa vile vidogo ambavo havina representative in Parliament kwa wakati huu viwe abolished ili yule mtu anayejisikia ana haja kuongoza vyama aingie katika chama chochote kile kwa hizo tulizo nazo kubwa na atafute uongozi na kufikia juu katika vyama vile.

Com. Hassan: Asante sana, ume sign hapo form? Elias Stephen Gitoto

Elias Gitoto: Asante sana ma Kamishna kwa kunipatia nafasi hii, mimi nafikiri mengi ya yale ambayo nilikuwa nijiaanda kuyasema ni kama wenzangu wametanguliya kuyasema lakini nitayagusa kidogo kidogo kulingana na hali yangu. Mimi naona kwamba katika Katiba ya Kenya lazima kuweko na kitengele ambacho kinaonyesha falsafa yetu ambaye sisi kama wa Kenya intuongoza kwa hii Katiba mpya. Na hicho katika desturi zetu zakuwa Kenya wote.

Pia Katiba ni chombo muhimu sana kwa nchi, kwa hivyo tusi ruhusu kuwe na badili ki holela holela kama vile Tumeona katika historia ya Katiba iliyo pita, ili kwamba kitengele chochote katika Katiba kwa sababu hiyo Katiba imeuunda ya Bunge kwa hivyo usione kile wewe unaweza kubadilisha kitu ambacho kimekuunda wewe, kwa hivyo lazima maoni yatoke kwa raia katika referendum.

Uraia, katika uraia, ningependa kwamba kuwe na uhuru kwa mtu yeyote ambaye amezaliwa Kenya anahaki ya kudai andikishwe kuwa raia wa nchi hii kama vile mfano wa Uingereza, mtu yeyote ambaye amezaliwa katika meli imetiwa nanga katika Pwani wa Uingereza ana haki yakutaka uraia wa nchi ile. Ili kwamba, tusiwe na raia wengine ambao tunasema hawa ni raia asili yakutoka Sudan, hawa ni raia wa asili Somali, hawa ni raia ya asili wa Ethiopia tuwe na raia ambayo ni raia wa Kenya kwa sababu wamezaliwa katika nchi hii. Lazima Katiba ifafanue katika defence mamlaka ya jeshi. Tunaona ya kwamba katika nchi nyingi za kifaraja kuna shida ya kwamba kikosi cha jeshi kinatumika katika badala yakulinda usala wa nchi kinatumika katika kuwasukuma raia wale wale wa nchi ile ambaye ni tax payers wako ndio wanalipa ile jeshi.

Roles ya Ministers. Hiyo ninaona katika vyama vya kisiasa tunajua sasa hivi vyama vingi vya kisiasa ambako tuko nacho vimeandikishwa katika Societies Act. Lakini mimi ningependekeza kwamba katika Katiba ijayo, Katiba iingize kipengele ambacho kita sukuma kiwe na political parties act ambavo vyama vya kisiasa vitakuwa ni vyama vichache vitatu na leo vinakuwa funded kutoka katika Consolidated Funds, ile vile vyama vimekuwa ni vyama yenye nguvu na vyama zina muelekeo na mtazamo kama mfano wa nchi zingine.

Katika Judiciary ningependa Katiba ambayo itakayokuja iwe na mpaka mkubwa kati ya Executive wasiweze kuingilia shuguli za Judiciary. Na pia kwa sababu ya vile tunaona mambo yanayo endelea katika Courts za nchi yetu kuwe na Supreme Courts na kuwe na Constitutional Courts. Katika Mahakama ya ki Katiba itanza kupata watu wenye kipawa tofauti ambao wengine ni watu wa dini wengine ni watu wa dini wengine ni watu siasa ili walete mchango wao pale sababu ni Mahakama ya ki Katiba halafu tuwe na High Courts. Na ningea pia wajibu waongezewe wale Kadhi katika Katiba mpya ili waweze kuingia hata katika Appellate Courts. Pia ningependa kuwe na system katika Mahakama ya Law Reporting, sababu Mahakama zetu hazina mawasiliano mazuri kwa sababu ya ukosefu wa Law Reporting. Kwa hivyo kuwe na Law Reporting Committee, ambayo lazima Katiba yetu ituelekeze mahali hapo, na pia kuwe na Law Reforms Commission ambao ni permanent.

Interjection Com. Hassan: Tuko na Law Reforms Commission ambaye iko permanent.

Elias Gitoto: ambaye iko independent? That is the question.

Com. Hassan: endelea.

Elias Gitoto: Nafikiri shida zote zinalalia Kortini kwa sababu, independent imekuwa hakuna, tunaona kwa mfano, chukua

mfano Constitution Courts juzi imefanya ruling Madagascar na (inaudible) angeweza kumzuia lakini kwa sababu ya independent wameweza kuchukua decision kile wangeweza kuchukua because they are independent. Kwa hayo machache asanteni sana.

Com. Hassan: Thank you very much. Next person is Madam Esther Njoroge NCKK, Esther Njoroge, ame enda? Ni wewe? Okay

Esther Njoroge: Kwa majina naitwa Esther Njoroge ni mobiliser wa wanawake Mpeketoni Division. Kwa sababu mengi yanaweza kuongewa mimi nitaongea mambo ambayo inawahusu wanawake ingawaje wengine wametoka hapa na wanaweza kuongea. Katika vile wanawake nilikuwa nimeandika memoranda lakini nitasoma zile muhimu kwa sababu ninajua wakati hakuna.

Wanawake waliweza kuona ya kwamba ni vizuri kama Serikali inaweza kusaidiwa kupatia mikopo katika group zao kwa sababu ya shida ambazo zinawapata. Katika groups ambao zimetembelea huko mashambani unaona ni wanawake ambao wako na ule morale wa Organization ya ile group yao lakini wako na shida ya kifedha, sasa tulionelea ya kwamba ni vizuri kama Serikali inaweza kusaidia wanawake kuwapatia mikopo, wanapatia mikopo ni kuwasiadia kwa njia nyingine ili waweze kujiamsha.

Kuna nyingine pai ya Divorcee's Right, siku hizi mwanamke akiolewa na bwana ake na wanaume mtanisamehe hapo ukikaa na bwana yako tuseme for 5 years ama for 6 wakati uko na watoto kama wanne ama watano unafukuzwa umeambiwa uende na wakati unapo fukuzwa, hauna mahali pa kwenda kule kwenu nyumbani hauna shamba ama nini. Bwana amekufukuza uko na watoto hataki kukuona after one week analeta mwingine sasa hapo tunataka wanawake waweze kuangaliwa, kama huyu bwana amemfukuza bibi yake, iwe ni jukumu yake kuangalia wale watoto kuwalisha na kuwavisha na mpaka na elimu mpaka kufa kwao.

Kisha kuna nyingine ya forced marriage, sisi wasichana inakuwa wazazi wetu wakituona tuko nyumbani, anaona nimefikisha 30 years niko nyumbani anafikiria ni bwana nimekosa nikiwa pale unaona mzee wangu antuletea mtu rika yaani, mzee rika na yeye anakuambia basi umekosa chukua huyu ndiye atakaye kuo, sasa tunaona ya kwamba hii mambo iweze kuondolewa. Kama mimi ni msichana niwe na ile haki yakujichagulia mtu ambaye mimi ninataka. Siku hizi si wote ambao wana (inaudible) yakwenda kuolewa ama nini kwa zile taabu ziko. Kwa hivyo wazazi waweze kuambia mimi nikiwa kama msichana niwe na ile right yakujichagulia mtu ambaye ninamtaka hata nikifika 40 years nikawa nyumbani, amenizaa mimi ni mtoto wake.

Kisha kuna mambo mengine katika tradition ambaye yana nyanyasa wanawake sana, unaona wakati Tumesimama hapa niko hapa I am very sure, hauzi wanawake wengi hapa maanake wengine wameambiwa na mabwana zao, musinde munaenda kufanya nini? Unaona sasa ningpenda mambo ambaye yana nyanyasa wanawake mila ati mwanamke kama siwezi mbele ya wanaume naongea na ile hali mimi naweza kuongea lakini vile mwanaume anajiona yeye ni mkubwa kunishinda yaani si ignore

wanaume ndivo kuko sivo kina mama? Kwa hivyo tuntaka ya kwamba tupatiwe ile freedom yakuonge hata kama mbele ya wanaume.

Kisha kuna mambo mengine yakurithii, mimi nikiwa kama msichana ama mwanamke yeyote unaona mimi tumezaliwa tukiwa wawili tukiwa kwetu nyumbani na vijana ni wawili baba yangu alikuwa na mashamba mawili, siku moja baba alisema kwa vijana chukua hili shamba na wewe chukua lile, mimi nikiwa msichana sina mahali pa kupatiwa, hata robo siwezi kupatiwa na mimi ni mtoto wake kwa hivyo tunataka tuweze kuangaliwa kama ni mashamba mimi niwe na piece pale nyumbani ili kama nitaweza kufukuzwa na bwana yangu nipate mahali pa kwenda na kujitegema.

Kama kuna zile shida ambazo zinani fanya ni seme hivyo kama sita gawanyiwa mimi ile piece ya land nyumbani nikifukuzwa pengine wazazi wangu wamekufa wote, baba yangu na mama yangu hawako nikienda niwakute wale brothers pale niwaambie nimefukuzwa na bwana yangu sasa nimekuja tukae. Sasa wataanza kunichukulia mapanga waniambie msichana we huna kitu huku rudi kuke umetoka. Lakini kama mzazi angekuwa ametoa ile command akiwa amesema ya kwamba hili shamba ni la msichana wangu, hii sehemu ni msichana wangu hata nikirudi sitakuwa na mtu wakunifukuza, kwa hivyo hiyo yakusema iweze kuangaliwa sana sana kwetu sisi wasichana.

Kisha waliangalia maslahi mengine ya hospitalini, hospitalini kuna hizi shida hakuna madawa, hakuna madawa yakutosha raia, kwa hivyo unaenda hospitalini pengine hata uko hata karibu kufa unaambiwa hakuna dawa kwanza enda kwa private ununuwe kisha uje tukutengeneze, sasa hiyo kitu ni nzuri ikiangaliwa vizuri ili tuweze kuangaliwa.

Kisha kuna hii mambo ya succession, mimi nimesema nitaongea mambo ya wanawake kwa sababu mengi najua hama taja mtaja ya upande huo mwingine. Kuna succession, mimi nimeolewa mahali ama mwanamke yeyote ambae ameolewa ambao mko huko nyuma, kisha umeposikia katika community zote si kabila zote nyingine hata hivyo Tume nyanyaswa ni wanawake na ni wasichana.

Sasa hapa unaolewa, bwana yako by bad luck anakufa, basi unaambiwa utaolewa na brother yake, waona, sasa mimi si ati nitakuwa mzee hivyo sana sitakosa mtu kujichagulia hata kama sitaolewa nikae pale nyumbani, lakini kwa nini unaniforce niolewe na brother yake bwana yangu? Na ila hali sijui kama yule ni HIV positive kisha unaniambia niolewe kwake waona imekuwa katika mila zingine zina nyanyasa wanawake, kama bwana yako amekufa kama ume amua kuolewa, jichagulie mtu ambae atakuoa, kama umamua kukaa, kaa lakini usiambiwe ati olewa na brother yake bwana yako hiyo si vizuri. Ama wanawake mna sema nini huko nyuma? Eh hiyo siyo nzuri.

Com. Hassan: Ngoja Esther, tafadhali toa maoni kwetu, usijaribu ku complain hapa.

Esther: Okay sawa, kisha kuna ile ingine ya handicapped, kuna hawa kiwete. Wanawake waliweza kuangalia wakaona ya

kwamba kuna hawa viwete, kama ni makazi wanapatiwa pamoja, kama mimi niko mzima mwingine pale ni kiwete hana miguu mimi nikienda kuuliza kazi mahali nitachukuliwa mimi lakini yule kiwete hata chukuliwa. Sasa tunaonelea ya kwamba mimi ambaye ninajiweza na yule kiwete ambaye hajiwezi, aweze kupatiwa nafasi sawa.

Kisha kuna ile ingine ya rape cases, kama mwanaume ame rape msichana ama mwanamke yeyote yule achukuliwe hatua kisheria na hakuna msamaha kwa sababu hii kitu iko, iko katika Kenya yote, hata katika Mpeketoni Division Lamu District hii kitu hiko, mimi niki rapiwa na mtu ambaye ni tajiri ninaenda pale Polisi nina shtaki nina anza kuwa harassed hata siwezi kuongea mara, ninaambia hata hauku rapiwa hata sijui nini, ninaogopa ninarudi, sasa tunataka ya kwamba hii rape cases, tena kuna mwanamke moja amesimma hapa akasema iangaliwe na polisi mwanamke ana Judge mwanamke. Sasa tunataka ya kwamba hii rape cases kama umenirape mimi uchukuliwe hatua kisheria na hakuna kutoa mambo ya hongo kwa sababu nitarapiwa na mtu tajiri ataenda pale atoe hongo mimi nitawachwa hivyo sina pesa za kwenda kutoa.

Kisha Wameandikisha kuna mambo mengine ya sexual harassment, mimi nikiwa kama msichana ama mwanamke, kwa mfano nataka kazi ofisini mahali, mimi nikienda pale ofisini nikimkuta boss ninamuambia ninataka kazi, nikimuambia ninataka kazi mimi niko ni ile hati yakujiriwa yakupatiwa kazi, lakini ataniambia kwanza ufanye vile ninavyo taka kisha uweze kupata kazi, sasa tumeona ya kwamba hii kitu hawa ma boss waambiwe waache kuwasumbuwa wasichana ama mwanamke yeyote ambaye anakwenda ofisini kuuliza kazi. Sina mengi ni hayo tu. Na Mungu ataweza kuwabariki.

Com. Hassan: Asante sana dada Esther kwa hayo maoni yako mazuri Tumeshukuru, please give us your submissions hiyo written document utawacha, ume sign? Have you signed? Just sign it halafu give it to us. Okay Michael Muchini Mwangi.

Michael Muchini Mwangi: Asante sana Commissioners kwa namna mulivo kuja hapa kuchukua maoni yetu. Kwanza mimi nitaongea kuhusu mambo ya uchuuzi, ama kwa kweli utaona wachuuzi ni watu muhimu katika taifa letu, lakini utaona ya kwamba hawa watu hawatiliwi maanani hata kidogo. Kama juzi Mombasa hivi, utakuta askari wa manuspaa wanakuta wachuuzi wakifanya uchuuzi mtaani lakini utakuta ya kwamba Serikali inachukuwa jukumu lakuwafukuza wale wachuuzi na wale askari wengine. Jambo hili ni jambo inatatiza sana katika taifa ambalo inataka watu waendele. Jambo lingine ni kuwa ya kwamba kama siku hizi hakuna ya kazi, vijana wamemaliza shule na hakuna mambo yaku ajiriwa, badala yakupatiwa (inaudible) kujitafutia riziki utakuta ya kwamba wakianzisha tu mambo ya kujitafutia riziki utakuta mambo yao yanakatazwa, jambo hilo tunataka Katiba yetu iki uundwa iweke mambo ya wachuuzi wapatiwe msaada na wasionekana kama watu ambao wanaleta uchafu katika mji yetu mbali wapatiwe jukumu lakuendeleza taifa.

Jambo lingine ningependa ku oungea ni mambo ya kilimo, kilimo kama mjuavyo ni uti wa mgongo wa taifa letu, na katika kilimo, utakuta ya kwamba kama hivi sasa mvua inanyesha watu wengi wako mashambani wanashugulika mambo ya kupanda lakini uakuta ya kwamba baada ya kazi kubwa unakuta ile kilimo haifaidi mkulima hata kidogo, wakati wa kuvuna kama ni mambo ya tuseme mfano ni pamba utakuta baada ya kuvuna na kutafuta soko unakuta wale ambao unwauzia, utakuta tayari bei

imeshawekwa na hakuna maongezo ambayo umeonge na wao. Hiyo ni jambo ningependa Serikali ichukuwa jukumu, kama vile tuna wizara ya Kilimo baada ya wananchi kufanya kazi ya kilimo, Wizara iwajibike kuwatafutia bei ndio watu watauzazao yao, soko Serikali iwajibike.

Jambo lingine ni mambo ya elimu, kuhusu mambo ya elimu nitaongea kuhusu mambo ya elimu ya msingi kama watangulizi wangu walivyo sema elimu ya msingi inafaa iwe ya bure kabisa, tusiambiwe elimu ni bure hivi kwamba tunalipa. Shule elimu iwe ya bure. Kama Kenya imestahili katiba katika umoja wa wamataifa elimu itolewe bure. Hiyo lazima itekelezwe, wananchi yeyote elimu ya msingi iwe ni bure kabisa, bile kutoa hata ndururu, hii sheria ya watoto iweze kufanya kazi.

Jambo lingine ni mambo ya afya, mambo ya afya ni jukumu la Serikali kuangalia ya kwamba wananchi wana afya jema, kwa mfano kama hospitali ukienda huna mambo ya dawa hakuna, na katika budget yetu wizara inaleta makadirio yake kuhusu mambo ya afya. Tunauliza, ikiwa ukienda hospitali zingine za kibinafsi utakuta madawa. Jee! kwa Serikali kuna nini? Mbona madawa hayapatikani? Na ili ya kwamba wananchi wanalipa kodi. Jambo hiyo ni jambo ambayo inasikitisha sana ukienda hospitali nyingi watu wana kufa na bado kuna taifa ambalo inataka watu waendeleo. Natumaini yangu tu ni hayo.

Com. Hassan: Asante sana. Asante sana bwana Muchiri, Julius N. Kimotho

Julius N. Kimotho: Asante sana Commissioners na wananchi ambao wamekuja kutoa maoni yao. Hasa kuhusu jambo hili la Katiba ambao ni ya muhimu sana katika nchi yetu. Mimi nimesema hapa represent Ecumenical Justice Centre for Justice and Peace as well as N.C.C.K. family in Lamu. Nina memoranda hapa lakini nita outline yale ambaye yalikuwa hapa, jambo la kwanza nimeonelea Katiba yetu kwanza haina ule utangulizi preamble na kwa sababu Katiba ni lazima ieleze ni nani ameandika na ni kwa nini na itafanya kazi namna gani. Ile tuliyo nayo inaonyesha kazi itafanywa hivi lakini kwa nini na nani hakuna, kwa hivyo tutaweka utangulizi ambapo tumeanza na kumtukua Mungu wetu in the name God Almighty, sisi watu wa Kenya tukiwa tunajali maslahi na wajibu wetu kuelekea uumbaji, basi tumeamua kuungana kwa pamoja kuelekea uhuru na demokrasia, mambo ya amani na muungano wetu na kuwa wazi kuelekea dunia na ule mambo yetu kuwa ya sawa, tuko wengi lakini tutaungana tumeamua kuungana kwa sababu ya heshima ya mtu na mwingine.

Tukijua ya kwamba yule tu aliye huru ambayo husherehekea uhuru wake na tukijua ya kwamba utajiri wa watu hupima na wale wanyonge basi ndio tukaamua tuandike Katiba ambao inaanza hivi. Kuna Executive Parliament na Judiciary yaani mikono ile mitatu ya Serikali, Bunge Serikali na Mahakama. We recommend that Tume recommend ya kwamba ile mikono mitatu iwe huru hakuna ambaye itakuwa na nguvu zaidi ya nyingine iwe na nguvu sawa, yaani hiyo ni principle of separation of power. Iwe Katiba separate nguvu. Halafu Tumeonelea tuka recommend kwamba, Kenya iwe na kiongozi wa nchi na kiongozi wa Serikali, Head of State and Head of Government.

Na tuka recommend kwamba kiongozi wa Serikali wa nchi awe ni yule itakuwa sovereign leader of country na yeye pia awe

hana chama chochote cha siasa, hakutoka kwa chama chochote cha siasa, na yeye atakuwa ndio focus of national unity kitu cha kielelezo cha nchi na hapo hapo, lazima awe na qualities zifuatazo:- Awe mzaliwa wa Kenya, awe ana kama university degree na awe ana akili timamu ana umri wa miaka 40 mpaka 70, na awe ameolewa, na utajiri wake au tangaze na awe hana criminal record. Halafu kiongozi wa Serikali tuka recommend kwamba yeye awe ni mwananchi wa Kenya, awe pia elimu yake amefika university ama equivalent, ama umri wa miaka 35 mpaka miaka 60, afya awe ana afya nzuri na utajiri wake pia ujulikane ameupata wapi, na awe na record nzuri na experience at least ya Public Administration na Financial Management na awe ni mtu ana tabia nzuri na tabia yake ijulikane ni nzuri.

Na hapa kuna powers of Executive zile nguvu za Serikali lazima zipunguzwe, tume recommend kwamba, Constitution, Katiba yetu ni lazima I approve iwe inatowa nafasi kwamba kila mtu akiwa amekuwa appointed ama mtu yeyote awe ni waziri amekuwa appointed by the President lazima awe approved by the Parliament. Apitie kwa Parliament wa approve. Na Katiba yetu pia ilimit Presidential terms to two. Executive nayo Serikali iwe inaweza kuondolewa mamlakani na Bunge, Katiba itoe nafasi kwamba Serikali ikiwa imetenda makosa Bunge inaweza kuiondoa, iwe na uwezo huo.

Members of Cabinet, tume recommend kwamba mawaziri wanaweza kuwa wanatoka nje ya Bunge, Bunge iwe wale walio chaguliwa bwana, wale ni wakutungia sheria na kupeleka malalamiko ya nchi na shida zao lakini mawaziri wanaweza kutoka nje ya Bunge. Hapo tukasema pia, Executive inaweza kutolewa tu na Parliament katika mamlaka siyo kama kwa sasa ni Cabinet ina uwezo huo. Head of Government na huyo kiongozi wa Serikali lazima awe aki attend mijadala ya Bunge. Awe akifika Bungeni kujibu maswala. Na tena ofisi ya Attorney General na ofisi ya Director wa Public Prosecution ziwe separated, hiyo in maana kwamba, ofisi ya Attorney General yeye ndio ana staki ndiyo anastaki, halafu mtu wa Serikali yeye ndiyo wakili wake kwa hivyo yeye ndiyo anamstaki na yeye ndiyo wakili wake hizo office ziwe separated.

Na Chief Executive yaani President awe anaweza kushtakiwa asiwe above the law. Hapa tuna powers of Parliament vile nguvu za Parliament, Bunge kazi yake kwanza ni approve appointment zile ambazo watu wamechaguliwa wakawa appointed, wana approve ingine lazima iwe na power to set and summon Ministers and other public officers, iwe inaweza kum summon minister na public officers ikiwa ametenda makosa, Parliament must have powers to impeach the President na iwe inaweza kumshtaki hata Rais na iwe na power to create and its own ministry hii mambo ya wizara kama inaundwa na President kwa sasa, basi iwe ni Bunge, ndiyo itakuwa inauunda wizara ama kuivuta.

Parliament must approve all expenditure na pesa zote za matumizi yote ya pesa za uma. Bunge iwe ina approve kwa sababu wale ni wakilishi wa watu, Parliament must determine its own calendar, na lazima muda wake iwe ndiyo inamua itafunga lini na itafungwa lini? Parliament will have powers to set up Commissions to discuss matters of national importance, zile. Tume, Tume zile zinaundwa hiyo ni ya Bunge ndiyo itakuwa ikichagua Tume kwa sababu yaki discuss mambo ya kitaifa, halafu yale yameweka mambo yao kwa Bunge, Bunge inatangaza. Parliament must not have powers to enact a law that undermines the basic structures of the Constitution or (inaudible) to the rights of individuals, katika Katiba yetu kuweke provision ambaye

itazuiya hata Bunge hiyo ku enact law ambaye ita undermine Katiba hii ama haki za binadamu hiyo tume recommend hivyo.

Hii nayo ni Judiciary, nayo appointment ya Chief Justice, Judges of Appeal, appellates and any other Judges should be approved by Parliament, ma Judge wakuu, ma Judge wa high Courts ikiwa wamekuwa appointed na President bas Parliament ina approve. There should be a Parliamentary Committee to vet appointments and public terms of service. Kuwe na Tume ya Bunge ambayo itakuwa iki chagua, all Judges should have Security of Tenure, na Judge ikiwa amechaguliwa awe ana kinga ya ki Katiba hawezi kuondolewa ovyo ovyo, ili aweze kama msemaji moja amesema hapa aweze kutoa uamuzi wa haki bila kuogopa, na pia tumependekeza tuwe na Supreme Courts, na tutapendekeza ma Magistrate wawe pia wakiajiriwa na independent Judicial Service Commission. Khadhi nao kabla hawaja kuwa nominated, appointed, basi Muslim Community wawe mu nominate, Muslim Community waseme ni huyu halafu ndiye awe appointed.

Election, Tumependekeza kwamba, kuwe na independent na representative Electoral Commission, Tume ya uchaguzi ambao ni huru na ambao ina uwakilishi. Katiba yetu lazima adopt the principle of proportionate representation ieleze itakuwa represented ki vipi? Voter education must be a duty on the part of the Electoral Commission and a right on the part of the voter. Elimu ya upigaji kura, iwe ni wajibu ya Tume ya uchaguzi na ni haki yakupiga kura. Katiba yetu iseme hivyo, every Kenyan will be entitled to vote where he/she may, MKenya yeyote anaweza kupiga kura popote alipo, siyo kwamba nikiwa hapa na kura nilichukua kule Vihiga isibidi niende nikaipiga huko, hapo hapo nilio nipige nichague huyu,

Com. Hassan: Mr. Julius please try and summarise now.

Mr. Julius Kimotho: Okay, I am just about, na Constitution Katiba yetu lazima iwe na kipengele yakuelezea vile uchaguzi utakuwa ukitangazwa wa uhuru na haki. Na Electoral Commission iwe iki toa results yake kwa Constitutional Courts before announcing, kuwe na Courts ya kiKatiba ambao vile Electoral Commission watapeleka huru halafu ziwe vetted kabla hazija tangazwa. Ikiwa mtu kuja kuwa Head of Government, awe kiongozi wa Serikali apate at least 51% of the total votes cast in the election, yule atapata 51 kwenda juu aunde Serikali.

Human rights, Katiba ni lazima i provide ndani yake haki za binaadamu kama vile ilivyo katika ile covenant on Economic, Social and Cultural na pamoja na ile Civil and Political rights zile ziko katika covenant (United Nations Covenants).

Na katika national Declaration of Human Rights, na katika African Charter on Human and Peoples Rights, zote ziwe recognized by our laws. Human rights education iwe ni haki ya mwana Kenya wakati wowote, iwe ni kitu inafundishwa mwana Kenya na kuwe na independent Human Right Commission. Katiba itenge hiyo na pia Constitution should protect the right of minority, kuna wale ambao ni wanyonge Katiba nao iwalinde iweke katika provision yake ilinde wale wanyonge and then iwe i provide Children's Commission. Haki za watoto kuwe na Tume ambayo itazishugulikia na tena the Kenyan society should be based on the principle of equality, including equality of sexes, usawa ule wa kina mama, baba, watu wote Katiba itoe hiyo. Na

tena hapa Katiba isi ruhusu any institution ya Serikali ambao italeta itatoa policy ama pasiwe policy or engage in practice that offends women. Katiba isi ruhusu policy yote ikaja tutolewa na Serikali pahali popote ambao ita umiza kina mama itawatenga kina mama kutoka kwa jamii ya hao wengine.

Sasa kuna hii ya mwisho ambayo ni finances, Parliament lazima approve finances expenditures, Controller and Auditor-General, should be independent and have Security of Tenure, yule mchungaji wa mali ya uma lazima awe na kinga ya ki Katiba hawezi kufutwa hata akikutaja wewe, asije aka ogopa na tena huyo huyo apewe nguvu yakustaki wale ambao wametumia pesa vibaya na all corruption offenders wale wote ambao wamejipatia pesa kwa njia isiyo halali itakuwa sasa wanaweza kulazimishwa hata kuzilipa. Establish an independent anti corruption unit with powers to arrest and prosecute, Katiba i provide hii na tena the Government must make public quarterly report of all revenues collected which must disclose actual projected expenditure of the revenue ya Serikali, quarterly kila mwaka mara .

Com. Hassan: Mzee umechukua nusu saa peke yako.

Julius Kimotho: Okay the last one now. Type of Government, we recommend Government of national unity where the will of the people shall be the basis of Government clearly stated in the preamble. Nafikiria nimefika hapo asante sana.

Com. Hassan: Thank you very much please for us and sign the document. Nilikupatia hii muda yote kwa sababu nakuona una wakilisha kikundi kubwa NCKK and ECJP. Kwa hivyo lakini noamba wale wengine ambao watakuja usijaribu kuchukua muda mrefu kama hii tafadhali kwa sababu kuna watu wengi hapa ambaye wamejiandikisha wanataka kutoa maoni kwa hivyo lazima tuwe na tuheshimiane muchukue amri mkipewa dakika kumi mjaribu kumaliza muda yako kwa hii dakika kumi. My next person is Elija Njoroge, hayuko, Joseph Njuguna hayuko pia. Wacha nimupatie Councillor Hussein Alawi fursa kidogo (inaudible) pia.

Councillor Husni Alawi: Mimi ni Councillor ya Witu Division, ambao tumekuja watu wawili kutoka Witu Division. Tunaomba ardhi ya Lamu, wakati inagawanywa ma ardhi, Katiba nataka ituhakikishie kwamba, watu wa area hii waangaliwe majority ardhi ya huku kwa sababu ardhi nyingi za Lamu zimeenda ambao si (inaudible) na kwa ufupi kuangalia Rift Valley, Central zimekuwa Trust Land zile ardhi, lakini ardhi ya Lamu, katika Kenya imebakia Lamu na Tana River peke yake ndiyo siyo Trust land na ambayo ni kama inawadhulumu watu wa Lamu kwa sababu Serikali ndiyo inafanya kuwa dhulumu siyo Trust Land, ikiwa wa Masai wana Trust Land naomba na Katiba iwe ina linda wananchi wa Lamu kwa sababu watu wa Lamu Ardhi zao nyingi zimeenda kwa wageni, 90% zimeenda kwa wageni hiyo naomba Katiba.

Kitu ya pili uchumi wa Lamu, ukienda Nyanza wamepatiwa ma nyavu na Serikali wamepatiwa vitu vya kuvua samaki, lakini Lamu Serikali imesahau na imetupa ni kama haijulikani, sasa tunaomba Katiba iwalinde watu wa Lamu kuangalia haki zao, kwa sababu ikiwa mtu wa Nyanza atapatiwa nyavu watasaidiwa matata hata huku na watu wa huku Serikali iwasaidie.

Tangu Kenya kupata uhuru Lamu District peke yake ambayo haijapata tarmac (lami) ni Lamu na North Eastern kidogo kwa sababu uongozi wote uko Nairobi, inasaidia wale wakubwa wa kule area zao wamesahau Lamu na Lamu ni katika Kenya ni moja District ya kwanza ikipata huru ni sisi lakini, lakini hata kilometer moja haija wekwa lami kwa sababu power zote ziko Nairobi na hakuna uongozi kwa wananchi, sasa nitafurahi Katiba ikitengenezwa iangalie maslahi ya hawa makabila ambao wako huku wapate haki zao.

Kitu kingine ni uwongozi, uongozi tunaomba Katiba ilinde watu ambao wa area hii wapate uongozi. Kwa sababu mara nyingi area nyingine zinaenda ambao siyo indigenous za watu wa zile area kwa sababu ni umaskini watu kidogo sasa wanavamiwa na watu wa kutoka up country an hawapati haki zao kwa sababu wao ni wengi na power wanazo, sasa ikiwa Serikali kuu inaweza Katiba iwalinde watu ambao kutoka up country kama mgeni amekuja afanye biashara afanye kila kitu lakini asiwe haki yakuchukua kiongozi kwa ile area kwa sababu kuna watu wamezaliwa pale. Wameishi pale sasa wengine watakuja ujue uongozi wawadhulumu wale ambao na Serikali iwe pamoja na wale, sasa tunaomba Katiba iwalinda watu wa ile area wamezaliwa pale wana zile pale wawalinde kwa sababu ikiwa hivyo itakuwa ni kama wamedhulumiwa watu wa area hii kwa sababu wao ni wachache na hawana, ikiwa Serikali inweza kujua Lamu ni hardship allowance, kwenye shida pia Serikali uangalia angalia pai Lamu kuna shida ya hardship pia kuwe na shida kwamba nafasi zikitokea tuwasaidiye wao wengine ni wa (inaudible) kwa sababu kusema utapatia wengine ni kama kuwa dhulumu, na mtu kama atoki kwa area hii asipatiwe nafasi ya uongozi, afanye biashara afanye kila kitu lakini uongozi asipatiwe. Wakipatiwa uongozi makabila ya huku itamalizika kwa sababu ni kidogo hawana mtu anawasaidiya.

Na DDC ni viongozi wa Serikali wanafanya, na wenyeji ni huwa ni wawili watatu kutoka kwa District sasa wakipitisha wale watu wote hawatoki kwenye ile area hakuna kitu inafanya, nitafurahi kama Katiba ikiwa kutakuwa na DDC iwe ni wenyewe wana nchi watakuwa pale viongozi wa Serikali ni kusema tu kuwasikiza wananchi vile wanavyo take lakini siyo iwe ni DC iwe ni DO ma ofisa wa Serikali wao ndiyo watapitisha DDC na ndio wata kuwa wengi kwenye DDC itakuwa haina maana kwa sababu DDC wote ambao wanakuja hawatoki katika District ya Lamu na ambao wanapitisha mambo ambao wenyewe wenyeji hawayataki, ndio sasa naomba Katiba iwaangalie wenyewe wenyeji wa Lamu kwa sababu bila hivyo itakuwa Lamu kwenyewe makabila ya Lamu yataendelea yakionewa na yaki nyanyaswa, na hakuna sheria ambayo itwasaidia.

Kitu nyingine ni majimbo, nchi hii ikitaka kafualu, lazima ipate majimbo kwa sababu in Africa nchi zote za Africa ambayo nchi ambao zimeendelea Sierra Leone, South Africa, Nigeria, Mali hizo ni nchi zinaenda kimajimbo, bila ya majimbo nchi hii itaendelea ikianguka na itadidimia kwa sababu nchi ambayo ni Serikali moja ni nchi ya dictator, wanapewa Serikali moja kwamba ina controlwa na nchi zote ambao katika Africa ambao si za majimbo na nchi ambao zimeanguka katika sasa in Africa, Europe ni nchi zote za Europe zinaenda ki majimbo, America ni hivyo hivyo tunaomba Katiba imue ki majimbo kwa sababu ndio itapeleka power direct kwa wananchi.

Lamu kama Lamu County Council, tunaomba kwa Katiba Lamu County Council ipewe power yakusimamia kila kitu isiwe ni DC, DC ni mtu kutoka bara atakaa mwezi mbili tatu ata take off. DO ni hivyo hivyo sasa, yeye haja yake ni mshahara, tuna taka ile mambo ya ma DC wote yaondolewe, na ma DO hao ndio wanaharibu hizi ma District kama Lamu, Lamu sasa karibu miaka mitano El Nino bara ambao ni Kilometre kidogo intesa watu kwa sababu DC ni mtu hatoki huku ajali chochote ana fly by air lakini wale hawataki kwenda pale bara bara, El Nino pesa zimetoka zime liwa Serikali imetupa kabisa kwa sababu wote ni ma officer wa Serikali na hawatoki area hizi. Tunaomba ikiwa DDC Lamu County Council, iwe na power kuandika wenyewe vijana wafanyi kazi pale pale kama ni ma DC wanatoka ndio wataweza hii kuendesha bila hivi zitakuwa District kama zetu zina sahauliwa.

Na lingine waajiraji wa kazi wengi wa wafanyi kazi wa Lamu 90% si watu ya Lamu sasa hii inamaanisha ni kuwa nyonya na kuna vijana wengi Lamu wahana kazi, sasa nikuiomba Katiba wakati imetokea ma parastatal kitu chochote kinatokea, Serikali ni lazima kwamba imekuja Lamu District ni kutangaza hizi nafasi watu wa Lamu waajiriwe. Kama sasa watu 90% wafanyi kazi wa Serikali wanatoka bara na kuna vijana wa Lamu hawana kazi.

Com. Hassan: Interjection, hiyo point tumechukua tumefahamu endelea .

Councillor Husni: Kitu ingine ni kuomba majimbo nimemaliza.

Com. Hassan: Thank you very much, Councillor umsema tuko wawili kutoka Witu.

Councillor Husni: Naomba aendelee kwa sababu tunakimbia Mombasa.

Com. Hassan: Okay sawa yeye pia aendelee, Wewe pia tumepatia nafasi dakika tano.

Abubakar Hussein: Sisi tunaomba majimbo.

Com. Hassan: Jina, anaanza na jina.

Abubakar Hussein: Jina yangu naitwa Abubakar Hussein, Kanu Chairman kutoka Witu.

Com. Hassan: Abubakar .

Abubakar Hussein: Abubakar Hussein, Tunaomba majimbo, majimbo ni kitu muhimu sana kwa sisi wananchi. (inaudible) kwa upande mwingi sana.

Interjection Com Hassan: Tafadhali tuwe na mkutano moja, tuwe na mkutano moja tafadhali kuna mtu ako, anaongea apewe nafasi aongee ndiyo wengine pia waongee, please let us observe some silence.

Abubakar Hussein: Nikizungumza zaidi ni mambo ya ardhi, sisi tumekosa ardhi zetu pande hii ya Lamu District, tumekuwa hatuna mashamba twaomba Katiba itulinde kwa upande hiyo ya ardhi. Leo imekuwa wageni ni wengi wana mashamba, sisi ni watu kidogo sana katika mia ni watu 95% ndio hawana mashamba, na wengi ni wageni walipatiwa nafasi kama hizo wamepewa na hatuna nguvu yakusema, ukisema inkanyagiwa kwa sababu vile aliongea Councillor ma DC ni wageni, mtu akienda anapatiwa ambaye si mtu wa area hii.

Na kitu ingine ni kuhusu upande ma Chief, sisi tunaona Katiba itulinde kwa upande ya ma Chief ni kitu muhimu sana afadhali kama maChief wanataka kuandikwa, wananchi wenyewe wapige mlolongo wachague huyu ndiye atakaye kutufaa kwa sababu (inaudible) haki zetu lakini mtu akiandikwa mtu wa Serikali ni mtu hajulikani, uko vipi au uko vipi, tuna shida sana kuhusu upande hiyo, Katiba itulinde vizuri sana.

Na kitu nyingine mambo ya msitu wetu Lamu District umemalizika na unaendelea kumalizika hivi sasa watu wamejaa msituni mvua tumekuwa hatupati na ingekuwa Lamu District mvua imeanza saa hakuna bara bara kabisa kwa sababu hatupati. Ukulima umekuwa taabu, tunataka kusaidiwa upande wa msitu pia Katiba itulinde upande hiyo ya msitu.

Na hawa watu ambao wako hapa wote ni wananchi wa hapa Kenya na lakini ni wageni, Mpeketoni wamekuja kwa miaka kama sisi wananchi wa Lamu District tukitoka kumi tuendee upande ya Rift Valley tuseme sisi tumekuja hatuna makao tupewe mashamba tutachinjwa kama kuku. Naomba Katiba hapa itulinde, hawa ingawa ni wenyeji lakini si wananchi wa hapa, hawa wamekuja miaka thelathini waliletwa hapa, na walichukua ardhi zetu na tumewapa nafasi lakini sasa imekuwa sisi wenyewe hatupati mashamba, tukiingia Witu Location, yangu imekuwa 85% ni wageni wananchi hawana mashamba, na mwanachi akipewa shamba kilometer mia moja huko hataki kwenda kulima, huko hawezi anashindwa nini katia itusiadie sisi wenyewe wananchi ndiyo tuna gawanyia mashamba kwa wananchi isipitie kwa DC ama PC wala sisi wenyewe wananchi tugawanye tupitishie kwa DC bwana Tumechaguwa hao ni wananchi wakupewa mashamba, na yeye DC na mkubwa mwignine yeyote ana watu wake moja anaweza kumuomba, lakini siyo (inaudible) Witu Division hatujui ni msomali tuki simama kwa mfano, mwananchi anatuuliza mashamba iko wapi, kwa nini mashamba hatukupewa tumawambia nini sisi. tunataka majimbo tafadhali.

Com. Hassan: Asante sana Bw. Abubakar, tafadhali utuweke kidole hiyo kitabu. Christopher Mashegi, Christopher, tafadhali tuwe na nidhamu kidogo tunyamaze tusikie mwenzetu ana sema nini.

Christopher Mashegi: Asante sana Bwana Ma Commissioner na wenzetu, mengi yamesemwa lakini kwa sababu ni lazima tuhakikishe tuonyeshe vile tulikuwa tunataka kuyafanya nitasema hivi, mimi katika aina ya Serikali ningependa tuwe mimi ningependa ikiwezekana kuwe na Rais ambaye ni Rais wa Head of Government lakini kuwe na Prime Minister ambaye ndiye

atakuwa Head of Government. Sasa huyu Head of Government atakuwa ndiye mkuu wa majeshi na yeye atakuwa ni ceremonial Head tu ku preside wakati wa State functions. Prime Minister naye atakuwa kazi yake ni kuongoza Serikali, naye atakuwa atatoka katika chama ambacho kitakuwa kimeshinda wingi wa kura.

Ningependa ikiwezekana tuwe na two Chamber Parliament ambazo tukakuwa na Senate na tutakuwa na House of Representative, Senate itatoka wapi? Senate itakuwa ni katika Provinces zetu nane kila Province itatoa ma Senator wawili, halafu kila constituency itapeleka member wake katika House of Representative lakini katika Senate tunakuwa na members kumi na sita pamoja na Speaker wao.

Kwa hivyo, kila nyumba inakuwa na Speaker wake lakini Senate inakuwa na 16 members kisha hiyo ni kusema ya kwamba tutakuwa na Regional Government. Regional Government in kusema kila jimbo la Kenya litakuwa na Serikali yake ambayo Serikali hiyo itakuwa incharge of the following, itakuwa of Defence, Finance na Foreign Affairs. Hizi nne zote, zitakuwa kwa Regional Government. Kisha Natural Resources of all these regions ziwe zitagawanywa katika following basis; kwamba the Federal Government should have 40% of the Natural Resources and the Regional Government should have 60% of the natural resources ili iweze kupitia uendelezaji ya Serikali yake ya jimbo lake.

In order to avoid non-starting katika mpango huu, tungependa iwe hizi, kwanza tusiwe na uchaguzi mwisho wa mwaka huu, badala yake all the parties to form a Transitional Government ambayo itafanya kazi kwa miaka miwili, na katika hii miaka miwili kuna mambo kadha yatafanyika, ya kwanza ni Truth and Reconciliation Committee itafanya kazi ili tuweze kuangalia madhambi yote yaliyo tendwa tangu tupate uhuru mpaka leo. Waliotenda madhambi ni kina nani, na walitenda vipi? Kama ni pesa waliiba wafanye nini wajulikane na baada yakujulikana hizo pesa wazi rudishie nchi, wakishazi rudisha nchi tuwasemehe halafu wanarudi katika main stream ya Serikali, tunawasemehe halafu wanarudi, halafu baada ya hapo, miaka miwili itakapo kwisha sasa Transitional Government iandae uchaguzi baada ya miaka hiyo miwili na uchaguzi huo uwe the following will not be eligible for election, hawa wafuatao hawata kuwa na ruhusa ya kuwa katika uchaguzi, wa kwanza all former members who at one time served as Ministers or Senior Government officers like Permanent Secretaries wasihusike kwa sababu tayari wao wana madhambi, pili the present sitting Ministers because they are part of the system should not take part even those who are there now, kwa sababu wako pale hata kama ni kijana kiasi gani, lakini tayari ameingizwa katika ile system kwa sababu wale waliyomweka pale wanataka baadaye aje kuwatengenezea mambo yao, kwa hivyo he should also be disqualified.

The Truth and Reconciliation Committee should sit and reveal all the sins committed by the concerned even the President and then reconcile them with the citizens, incase of looting, the concerned should be forced to bring back all the money they had taken out of the country.

Civic Education should be an on going process and it should be taught in all schools, both Primary and Secondary schools even University, so that every mwananchi goes through all the system of education and by the time he is through, he already knows

what he is required to do as a citizen of the country. The Attorney General should be proposed by the President but must be grilled and discussed and confirmed by the Senate before appointment. These should also be for all the Ministers, all the Ministers should also go through the same system and even the Permanent Secretary and also the Judges, then these people their tenure should not be interrupted until the Parliamentary life expires, hii mambo yakuwa ati una kuwa na Permanent Secretary leo baada ya miezi mitatu unasikia Permanent Secretary amekuja mwingine that should go. Tuwe na hawa officers they should serve throughout the life of Parliament so that there will be continuity and proper, ili mambo kuwe vizuri, au pengine kama mtu amekufa hapo anaweza kuwa replaced.

The President's powers of hire and fire should also be curtailed, and in place the Constitution should be the supreme organ of the country. To avoid tribalism in our system we should only have two major parties and one minor party that is Three Parties, we should have three parties where just like we have in Britain, I am giving an example of Britain and also of countries like United States where we have Republicans and the Democrats, we have the Labour Party and the Conservative and also the Liberal, so we have Three Parties there now the two major Parties are going to be but will also be checked and balanced by the Third Party. So you find that like the British system where you find like the Conservative is the Ruling Party and then another Party, and then one does a mistake what happens the Labour Party tries its best to woo the "wananchi" to vote it out. If it finds that it cannot, it tries to enliff the powers of the Third Party which is the liberal and in that way they are able to form a coalition, so a coalition type of Government should also be allowed in Kenya.

Next is this question of lawyers and their clients, the lawyers have become very notorious in Kenya, you find that a lawyer, we call them ambulance chasers, when they see a person had an accident they follow this person to the hospital and then they promise to be the advocate and in the end of the day, when the case has been won and compensation has been made the client remains unpaid, he has no money and this gentlemen here, goes to buy the mercedez with his client's money. So the Constitution should see how they are going to protect the wananchi against such type of lawyers.

When it comes to the duties of the Parliament, when it comes to passing a Bill, a Bill becoming a law. We have in practice, to start the Bill as presented and then when it has been presented it is read in the Parliament, first reading and then these MPs are supposed to go out to wananchi to get views, this never happens. What happens is everything is done there in the Parliament you only hear over the radio and in the newspapers that something has happened and that is why you find it is not a wonder that a Bill can be presented in the morning and by the end of the day it has become a Law. So such a thing proper order should be followed. Referendum, we should have referendum in the country where the MPs should be forced by the Constitution to go to the wananchi and collect and get their views of the wananchi about any impending Law.

Pili kuhama hama vyama,

Com. Hassan: Your time is up.

Christopher: I am just finishing, hii kuhama vyama naye ingekuwa there should be a condition set so that any person who has moved from one party to another should not be allowed to participate in whatever election in new Party until after when the next life of Parliament begins.

That one will take checks from moving in and out of parties like the way we were seeing the other day with the Mayor of Nairobi.

Spreading the economic infrastructure to all parts of the country can only happen if we have these Regional type of Government, a good example is our road here, road between Lamu and Garsen, despite the fact that our place was given the money, this money has never worked but we are hearing that in other parts of the country El Nino money did abit of work in whichever places but what happens probably the money was diverted to other places. Land ownership also should be checked between the poor and the rich it is common practice in Kenya that you find that the rich are getting all the land and the poor are left without. So this one should be checked on.

And then when it comes to employment, I have heard a friend of mine being bitter about indigenou and settlers, but let us look at it critically and you will find that the settlers who are here are not benefiting from that, so what we should do is I am asking the Constitution reformers to see to it that the person who qualifies, be given that opportunity because he is also one member of the same society. Kwa sababu hata sasa mti ukituangukia hapa au bomb ikituangikia hapa Mpeketoni hapa Lamu, si tutakufa sote watu wa Lamu na wa kisiwani, au sivo, kwa hivyo kama tutakufa sote wa Lamu na kisiwani kwa hivyo hata nafasi za kazi tupatiwe pamoja.

Voting should let us have it in our Constitution that voting we should not allow any type of voting apart from secret balloting because this other ones are just a way of manipulating people inorder for some few people to get what they want. Thank you very much for listening to me.

Com. Hassan: Thank you very much Mr. Muthengi, Please try and keep to your time we give you because we are giving every person 10 minutes and I can see that you are going for more than ten minutes, try and keep to your time please, our next person is Peter Kibaki, if you can finish earlier than 10 minutes we shall be grateful.

Peter Kibaki: Asante sana kwa Tume ya uchaguzi haya ya Katiba, mimi langu ningetaka Katiba itusimimae kwa ajili ya hospitali kwa matumizi yake, kwa kuwa hospitali za uma zimekuwa kama ya mtu binafsi maanake ukienda unatoa pesa na dawa zinaitwa za bure kwa hivyo zikiwa ni za bure kila hospitali, Katiba ningependa itusimamie ikiwa ikitumika kwa bure, ya pili ningetaka katika Katiba yetu ya Kenya haijajitambulisha ni akina nani, katika section one ya Katiba inasema tu hii ni Republic of Kenya lakini haijajitambulisha imesimamia wakina nani, kwa hivyo yangu ni kama hayo sina mengine, asanteni sana.

Com. Hassan: Asante sana bwana Kibaki kuja tupigie signature hiyo. Tafadhali tunaomba wale wanakuja watoe mapendekezo yao, wasianze kutupatia story hapa mingi kwa sababu hatuwezi andika yote. Tumekuja maoni na mapendekezo ya wananchi. Councillor Julius Macharia.

Councillor Julius Macharia: Asante sana mwenyekiti Tume ya Katiba na wananchi hamjambo? Basi nafikiri yangu itakuwa ni machache sana kwa sababu mengi imewahi kuzungumzwa kwa hivyo nitagusia tu pengine yale ambayo haijawahi kuzungumzwa. Kwa hivyo nitagusia tu yale yame pitiwa kidogo ama yale ambao kabisa haya guziwa, kwa hivyo kitu cha kwanza mimi ningependekeza katika Katiba ya sasa lugha ambayo imetumika, lugha ambayo imetumika kidogo ni ngumu kwa mwananchi kuielewa. Kwa hivyo, ningependekeza Katiba ya sasa iwe imeundwa katika lugha ya kitaifa ama kiswahili ambacho kila moja ataweza kuielewa kwa urahisi. Ya pili pia ningependekeza kwamba Katiba iwe ni kitu ambacho kitafundishwa watoto shuleni, kwa hivyo mtoto anapo maliza darasa la nane awe anaelewa Katiba.

Pia ningependekeza kwamba Katiba iweze kuwalinda mwananchi vilivyo kwa sababu Katiba ya sasa inasema ya kwamba itamulinda mwananchi, itampa elimu, itampa makao lakini kwa wakati huu hiyo yote haifanyiki kwa sababu kwa mfano katika upande wa elimu, uta kuta mtoto yeye amesoma amefukuzwa shuleni hakumaliza darasa la nane lakini Serikali haina jukumu lolote la kuweza kujua ule mtoto ameishia wapi, kwa hivyo ningependekeza jambo kama ile upande wa elimu iwe ni sheria mwananchi yeyote ikiwa hakuweza kupata masomo aweze kuwa anaweza kumshtaki Serikali, awe na hiyo sheria iweko kwa sababu ana shugulika hapo.

Pia ikiwa Serikali imeshindwa kuumpa mwananchi makao, sheria pia iweze kumrushusu yule mwananchi kushtaki ile Serikali iwe katika Katiba. Upande wa utawala ningependekeza pia, upande wa Chief wawe wakichaguliwa na wananchi kwa sababu Chief yeye anaongoza watu na hapigwi transfer kwenda sehemu ingine anakaa na watu pale kwa ule muda mpaka retirement yake itakapo fika. Kwa hivyo, ingekuwa ni vizuri wananchi ndio wanamjua vizuri na wanajua ule mtu anaweza kuwaongoza vizuri.

Kwa upande wa uchaguzi ninge taka kupendekeza Katiba ya sasa iwe kwamba kituo ambacho kura zimepigwa kiwe ndicho kituo kura zitahesabiwa pale, kwa hivyo all Polling Station, ziwe kura zina hesabiwa hapo halafu zinapelekwa sasa zile results zinatangwa halafu zote zinakusanywa katika District. Watacao chaguliwa kwa upande wa Bunge, ningependekeza Wabunge yeyote ambaye atakuwa napigania Ubunge awa amekaa katika ile sehemu ambao alikuwa akiwakilisha Bungeni at least for more than 3 years ili aweze kuja kupigania mahali hapo.

Pia qualifications zake ningependekeza pia awe na elimu ya degree, ili aweze kuhitimu kuchaguliwa. Pia kwa upande wa ma councillor ningependeza na wao at least wame soma hadi kidato pengine cha nne. Kwa upande wa Rais ningependekeza pia Rais asiwe ametoka katika chama chochote awe amechaguliwa kutoka kwa watu pia asiwe above the law. Rais awe chini ya sheria ili pia mwananchi awe anaweza ama mwanaKenya yeyote awe anaweza kumshtaki anapo pata ile kosa ambalo

amewezakuwa amefanya. Ningependekeza pia kwamba wale ambao wanaweza kugombea kiti chochote wasiwe ni watu wame retire, kwa mfano mtu ana retire katika Serikali halafu anakuja anagombania Ubunge ama anagombania Udiwani, kwa hivyo ningependekeza yeyote amabae anagombania kiti chochote cha uongozi awe ni mtu haja retire kwa hivyoaje kwa kazi awe ni mtu hajatoka upande huo.

Pia ningependekeza kwamba katika Katiba ya sasa haina limit ya kwamba mtu anaweza kuwa na kazi ngapi, kwa hivyo ni vizuri kila mtu awe na kazi moja. Ikiwa wewe una kazi usishike kazi ingine kwa sababu hiyo tunaona ya kwamba, inanyima vijana wengi au wananchi wengine kazi, kwa hivyo kila mtu kazi moja, mtu moja kazi moja, kwa hivyo pia hiyo tungetaka iingie katika Katiba. Katika upande wa wanawake ningependekeza kwamba mwanamke au mtu yeyote kijana au msichana ambae anataka kuoa, isiwe na kuwe na sheria kwamba ako na uhuru wakusema kama ikiwa ni kijana amempenda msichana awe na uhuru kwamba wamependana na waoane, kusiwe na ile mambo ya kwamba mzee ana sema ni lazima nipewe kitu kadha ndio uoe mshichna wangu ikiwa si hivyo huwezi muoa kwa hivyo unamnyima ule msichana haki yake yakuwa wamependana na huyu lakini mzee amekataa kwa sababu haja pewa hiki.

Pia ningependekeza ya kwamba hii equality kwa wanawake na wanaume iwe iwekwe free katika mambo tradition au mambo ya dini kwa sababu kuko na dini zingine haziruhusu mambo kama yale na pia kuna tradition zingine hazi ruhusu yale mambo, kwa hivyo ningependa ki-Katiba iwe imeachia mambo ya tradition kulingana na tradition zao vile ina kaa iwe ndiyo hivyo hivyo, kwa hivyo ningependekeza iwe imekaa naman hiyo. Nafikiri kwa sababu ya muda pia na mengi pia imezungumzwa nafikiri kwa hayo machache nitakoma hapo asante.

Com. Hassan: Asante Councillor. Pastor Luanda.

Pastor Lowanda: Mwenyekiti na watu Mpeketoni ama sehemu za Lamu nawasalimia wote. Jambo ambalo niko nalo hapo ni kwamba mengi yame nenwa, sisi wengine ni kama kurudia tu.

Jambo ambayo ningezungumzia kwanza ni jambo ya kwamba jinsi tuliposikia hapa ya kwamba Mahakama na Serikali na pia utawala ya Bunge utoshane katika mamlaka, kwa hivyo kusema ya kwamba Mahakama na iwe na mamlaka ya kutosha inaweza kustaki Serikali naye Serikali iwe na uhuru wakufanya kwa sababu Serikali ni kufanya, Serikali ni chombo cha kufanya kwa hivyo kufanya kazi yao inavo stahili na pia Mahakama naye ifanye kazi yao kuwa hukumu wanapo tenda yale ambayo hayastahili.

Na Bunge naye kwa sababu bunge naye ni chombo ambacho ni cha kulinda basi kiwe na mamlaka yake kusema ya kwamba Mahakama inaweza kumstaki Mbunge, Mbunge naye anaweza kuzungumzia hakimumu ama idara ya Mahakama na kufanya Mahakama ama kufikisha katika Bunge ya kwamba na kama imekosea kwa hivyo walio husika wanastahili kushtakiwa na pia na hiyo Mahakama kusema kwamba hizo sehemu zote zina uwezo katika upanmde wao. Jambo lingine ni kusema ya kwamba Rais asiwe na mamlka juu ya sheria ama juu ya mamlka, mamlka iweze kumshtaki Rais akawa amekosea, hata kama itakuwa

Marekani ya kwamba wa sherati peke yake kuleta Rais ashtakiwa iwe na uwezo kama huo, Rais aweze kwenda kortini na asimame na pia ashtakiwe kusema ya kwamba Mahakama ina uwezo juu ya Rais.

Kwa hivyo jambo lingine ambalo ninataka kuliguzia hapa ni kwamba Ministers ambao watachaguliwa na hile Serikali ambaye inauundwa, wawe ni watu wamesoma, wasomi ambao wana elimu yakutosha kama idara fulani yeye, ana ujuzi wa kutosha katika ile idara, na pia maoni yatoke kwa Wabunge ambao wanachaguliwa kule Bungeni na wao watoe maoni ya kwamba ana uwezo wa ukulima upande huu, anauwezo wa kujua habari ya hiki, mimea na mbegu na kila kitu awe na ujuzi wa kutosha si ya kwamba hajui mambo mengine, mengine ni kuwenda kuuliza kwa hivyo kusomea kwamba ni Minister awe yeye ana hiyo ujuzi wakutosha ana Wabunge wamemzungumzia kuonekana ya kwamba akifanya ile kazi, itakuwa inaendlea vizuri na atakuwa na uwezo wakuifanya hiyo kazi, kusema ya kwamba lazima awe amepitia kile chuo cha University and awe amesoma ya kutosha katika ile sehemu ambao yeye amefanywa kuwa Minister na Bunge anaweza kupewa ni mtu wa form 4 kwa sababu yeye ni mtetezi tu ambae anatetea watu wale wengine.

Kwa hivyo jambo lingine ambao ninge gusia ni kwamba mahari na rudi huko sehemu za wanawake ama vijana ama wasichana kwa wavulana ninge gusia kijana anapokuwa kama sasa mabadiliko yaingie katika 8-4-4- system na yakafanya system ikaongeza miaka na ilikuwa zamani miaka kumi minane kijana apate kitambulisho chake, amekuwa mtu kutafuta kazi yake, lakini sasa tokana na ile mabadiliko mabadiliko ambaye yanatakiwa hapa na pale, ningegusia pia kijana naye ili apate kitambulisha hiyo inaweza kuwa miaka kumi na minanae lakini ikifika ni wakati wa kuoia pia wawekewe sheria zao kwa sababu hapo ndio kuna shida upande wetu kama sisi watu ambao wanahudumia vijana katika (...) ningesema ya kwamba wale wana wapitishie sheria ya kwamba miaka yao ya kuoia itakuwa miaka ishirini na moja ama miaka ishirini na mine amma miaka mingapi ili yule kijana asiwe chini ya utawala ya mzazi lakini awe chini ya utawala wa Serikali kama nchi zingine ya kwamba miaka akifikisha miaka ishirini yeye anakuwa yuko chini ya Serikali.

Kwa hivyo kama ni msichana hatatoa mahari kama ni kijana hatatoa mahari bali watakubaliana kuishi pamoja na bwana na bibi kama kulingana na vile sheria inavyowalinda kwa sababu kupata cheti cha ndoa hiyo ni kumaanisha ya kwamba wewe Serikali imekushikanisha pamoja lakini kutengana kwenu itakuwa pia ni Serikali ambaye inapitisha mna tengana, kwa hivyo kusema ya kwamba mahari ndiyo itakuwa kikwazo kikuba nchini Kenya ama katika tamaduni zetu za kiafrika ningeguliza katika maoni yangu Katiba ya Kenyaiwe na uwezo wakusema kijana akifikisha miaka ishirini na moja ama miaka ishirini minne yeye anauwezo wa kuoia yule anataka hata kama ana mali ama hana mali, kama huyu msichana ana mali ama hana mali, lakini akue na sheria ambaye itasemwa ya kwamba msichana kwa mvulana ana haki ya kuriithi kwa utajiri wa baba yake kwa hivyo ana ile haki yakuriithi mali kutoka kwa wazazi wake, awe msichana ama awe mvulana ka sababu tayari pengine wameenda kule na wakapata kitambulisho na wana kila kitu wakawa wame.....

Kwa hivyo kama ana kitambulisho kwa nini mali wasije wakapata? Kwa hivyo kama ni mali pia wagawane mali katika ile uriithi yao na itakuwa ina amani ama itafanya akue na usawa kwa maisha. Kwa hivyo jambo lingine ambae nilikuwa nataka kuzumzia

hapo ningetaka kuguzia utamaduni, utamaduni nchini Kenya kama makabila tulivyo kama arobaini na mawili hivi ama kama kuna kumeongezeka mengine lakini nafikiri makabili kama arobaini na mawili, katika nchini Kenya hayo makabila tumeingiana tuna ile tuliingiana sasa kila mtu ukienda bara watu wameiniliana, huku sehemu za pwani watu wameingiana, Kule kuingiliana maoni yangu ni kuwa kama hivi ule utamaduni pia uwekewe sheria ambayo itakuwa kuwe na Tume yakuchunguza ambaye itakuwa ina uwezo wa sheria kuchunguza zile utamaduni zote ili kuzisawasisha kwa sababu mahali ambako tunaelekea miaka ambaye inakuja utamaduni wetu utukuwa umeingiana na kwa sababu ya ile kutoelewana hapa na pale hakuta kuwa na sheria ambaye itakuwa ina fanya mtu asije akaenda Mahakamani (...) upande huu ama upande mwingine.

Tuseme ya kwamba ule utamaduni wa Kenya ambaye sisi sote ni makabila Fulani, we kabila lako huyu kabila lake zote ziletwe ile hiyo utamaduni wote na mila zote ziletwe pamoja na tujaribu kusawazishwa kama kwa sababu zinataka Kenya ambaye itakuwa na watu wote, si kwamba ukikuja pwani wewe si mpwani ama ukienda sehemu nyingine wewe si wa sehemu hizo lakini kuwa na ile sheria amaye itafanya zile kabila zote ziwe na kiwango ya kwamba sheria imewasimamia wote ya kwamba ni wa Kenya na mila zao inasema hivi zote na imesawazishwa na sheria kuwa simamia hawa Kenya. Kwa hivyo nimesema Mungu abariki.

Com. Hassan: Asante sana Pastor tafadhali tupigie signature hapo. Anthony Mwaura.

Anthony Mwaura: Asante mwenyekiti wa Tume hii mimi kwa maoni yangu zaidi ningeguzia, kwanza ningeguzia mamlaka ya Ofisi ya Rais. Katika nchi hii kwa kweli hata kama hatumpata Rais nzuri kiasi gani, akisha ingia katika ile ofisi na kujua uwezo aliyo pata bila shaka hatatenda mapya.

Kwa hivyo, ni vizuri kwamba ofisi yake ikagawanywa na Bunge Ipatie uwezo mwingi kwa sababu ndilo limechaguliwa na wananchi wenyewe, pia Mahakama, Mahakama inamusimamia mwana wa Kenya bile kujua uwezo wake kabila lake ama alizo nazo kwa hivyo Mahakama inafaa kuwa Mahakama huru kwa wakati huu laiti wanyonge hawasikiki wakati wanapo fike Mahakamani pengine yule tajiri anatomia uwezo wake na kwa sababu Mahakama si huru basi yule mnyonge huwa mara nyingi hana haki.

Pia Bunge iwapo ofisi Fulani itatumia kwamba nimeamuriwa kutoka juu yeye amechukua nafasi hiyo (...) ofisi hili kwa sababu mamlaka yake hayako pahali pengine isipokuwa ofisi hiyo moja, kwa hivyo ni bora kama Katiba yetu itarekebisha ... upande huo. Upande mwignine katika Katiba yetu sijui kwa kweli hata kama imegusia juu ya mkulima, lakini labda ingefaa irekebishwe sababu tunapo agiza, tunapo nunua vitu kama fertilizer tunaitishwa ushuru, na sasa kwa kweli Katiba ingekuwa inalinda maslahi ya wakulima wangeombewa watumie hii kwa hivyo iwe duty free ili mkulima kufaidika na aweze kusimamia taifa hili.

Kwa kweli katika Bunge zetu tunaisikia kwamba Ministers na Wabunge wanakubaliwa kuagiza gari duty free kwa nini mkulima ambaye analima ili kulisha taifa hili apatiwi nafasi hiyo? Sehemu nyingine ni upande wa (...) katika utawala, utaangalia kwamba

kuna mlolongo mrefu wa viongozi lakini wote wanahitaji mishahara, kama kwa kweli ni mara ngapi nimeenda ni wananchi wangapi kila siku wanaingia katika ofisi ya chifu ndiyo wahudumiwe na chifu labda ni watano, na ni wananchi wangapi wanaingia hospitalini kila siku kwenda kuanangalia madawa wasiyapate? Kw anini Serikali isiangelie kama mzigo mkubwa kwa kimatumizi imeengia kwa Administration kwa nini wasipunguze ili yule naye, anaye kuna Assistant Chief, kuna Chief kuna D.O. mlolongo wa kiongozi kwa nini tuispunguze ili tukaweza kupata madawa hospitalini? Katiba ijaribu kurekebisha namna tunavyo weza kuchunguza gharama.

Upande wa usalama wetu, sisi ni walipa kodi ambao tuna Katiba inajua imeahidi ama imeeleza kwamba, ina linda mali yetu lakini mara nyingi utakuta kama ni maduka huko yanavunjwa, duka inaporwa na hata mtu kuuawa na hii inaishia hivyo hivyo. Kwa hivyo kama sisi ni walipa kodi, kwa nini njia zozote sizitumiwe ili mtu huyu aweze kulindwa na Katiba ya nchi yake?

Nyingine ningependa kuguzia kwenye Tume hii ni juu ya migomo, kwa kweli migomo si kitu halali kama vile inavoeleweka kwa wakati huu, lakini huwa ndio njia moja mtu huyu kujieleza shida zake, hii inachukuliwa kama ni uvunjaji wa sheria, mimi kwangu naona Katiba hii irekebishe maanake huu si uvunjaji wa sheria ikiwa mtu ata kuwa ametumia njia zinazo stahili kujieleza na kama haikusikika basi hana jambo lingine aweze kufanya mgomo, hii ni kumaanisha kwamba, hata mimi nikiwaajiri watu wangu watano na kisha niwanyanyase kwa njia zozote mimi nita sikika zaidi kuliko wao kwa hivyo ukiangalia kipengele nyingi haingepatiwa nafasi nzuri zaidi ni yule mauajiri. Kwa hivyo Katiba hii ijaribu kurekebisha.

Nyingine ni juu ya maandamano, mara nyingi wamepigwa wakifanya maandamano hii kwa sababu pengine Katiba ile haikusema wazi ni maandamano aina gani, sisi tutafanya maandamano kwa njia tulivu na ya haki, lakini huku tunatumiwa polisi kutu piga kwa nini tupigwe katika nchi yetu, kwa sisi tusiwe na uhuru wakujieleza, ikiwa nikipita hapa bara barani sikuvunja kioo cha mjengo hili kwa nini nipigwe? Nina hatia gani? Hatia yangu nikujieleza. Katiba hii iangelie mimi sina mengi ni hayo tu asanteni.

Com. Mosonik: Mary Mbugua – Ni Chairlady wa nini please?

Mary Mbugua: Chairman, na wananchi wenzangu Hamjambo? Yangu si mengi sana sababu naona inasemwa na nakuja kwa upande wa wajane sababu kusema kweli, wajane nchi yetu ya Kenya ni wengi na tuna watoto tuliwachiwa na hawa watoto hatutaki wawe chokora, sababu wakiwachwa tunaambiwa ni wale tu wanachiwa wawatunze, tena hawa hawa watoto wakiwa chokora ni sisi tu tutakuja kuchekwa watu Wakenya, tunauliza Tume sababu wako hapa nachoni petu, tunauliza kila mkoa tunawauliza watuwekee mashule sababu wakiwa mashule, hawa watoto watashikwa tu na kupelekwa kule mkoani kila koa, kila mkoa waweke mashule hawa watoto wakose kitanga tanga na wawe na elimu.

Tena kuna hawa wajane waliwachwa kuna wengine kama sasa tuko hapa settlement scheme hii ya Kenyatta tuliwachwa na kuna mwingine alikwenda akachukua loan, na loan aliyochukua hakumwambia mke wake sababu hajui, mtu hajui siku yake ni gani yakwenda, sababu sasa aliwachwa na sasa tunapewa miaka nasikia ni miaka saba, sasa huu miaka wa saba ukifika huyu

mama, yule mjane hana chochote yakulipa ile shamba sababu yake aliwachiwa watoto ni wadogo wengine ni wakubwa wanataka kula, wengine ni shule na anafanya bidii hiyo kazi yote anafanya lakini hii ya shamba inamlelea kwa hivyo Tume itufikirie hapo. Wajane, tena tunaona mazao yetu kweli tuna lima kama wakati huu kuna maembe na yote tukieenda pale Nairobi huwezi kuinunua moja shilingi, hapa kwetu ni shilingi. Tunaye tena bara bara yetu, tunawatii sababu mko hapa, tuna bara bara hii yetu si nzuri sababu tungekuwa tukijipekeya kwingine tuna komboa mimi na yule mwingine tunashikana hayo maembe tunapeleka mpaka Nairobi, tunapata pesa, mtoto anakuja kwenda University ambazo aliitwa, lakini akiitwa yuko nyumbani sababu hakuna pesa, na pesa ziko kwa mti lakini ni ile shilingi, mutufikirie hali ya bara bara, tukisikia kwa redio tunasikia redio ikitangaza ati kunatolewa pesa ya bara bara Fulani lakini huku kwetu hatuoni ikitengezwa na si mwaka huu wala wa pili, sasa pale tunaita mahali moja, sasa kama siku ya leo watu walikwenda na mguu sababu hakuna kusikika ama si hivyo?

Ni hivyo, sababu yakusema bara bara ziwe muhimu kwa mtu kepeleka vitu vyake hapo mtufikirie sana muktengeneza hiyo Katiba. Tena kuna ingine tuna huu mwalimu, mwalimu tulitufundisha sisi sote tuko hapa, na tukisikia walimu wanataka kugoma wakati tunasikia kama anakwenda sasa na anaanza kwenda kugoma tunaona ni vibaya sababu, mwalimu alikusomesha na akanisomesha na akasomesha wale wako juu hata Rais wetu alisomesha na mwalimu, maslaha ya walimu wafikiriwe sana na madakari tena wafikiriwe kugoma, sababu wakati wa El Nino waligoma na tukawa na shida kubwa sana, na kama walikuwa sasa Katiba iko sasa ingekuwa ni vizuri sababu Katiba ingewalipisha mara moja na kurudi kazini, yangu sina mengi ni hayo na Bwana awabiriki sana.

Com Hassan: Asante sana, asante na sasa tunataka Susan Wangari.

Susan Wangari: Asante sana kwa kupata nafasi hii na kulingana na maoni ya kina mama, wa mama wameonelea ya kwamba ni vizuri Rais awe mwana Kenya, na awe na

Com. Hassan: Susan tunataka uweke microphone karibu na mdomo yako halafu unaanza na jina lako, kwa sababu inakuwa taped hapo.

Susan Wangari Asante sana, kwa kupata nafasi hii, kulingana na maoni ya kina mamaInterjection,

Com. Mosonik: Taja jina kwa hiyo microphone.

Susan Wangari: Jina langu naitwa Susan Wangari.

Com. Hassan: Endelea.

Susan Wangari: Kulingana na maoni ya kina mama, akina mama wameonelea ya kwamba upande wa Rais ni vizuri awe na bibi na pia awe mzaliwa wa hapa na awe na birth certificate, na kitambulisho na pia awe ni Head of Government asiwe na mamlaka juu ya majeshi, na asiwe na chama chochote, asimame kama Rais, kwa hivyo ni vizuri Katiba ikirekebishwa, Rais asiwe na chama, asimame kama Rais tumchague kama Rais lakini asisimame kama an chama chochote pia akina mama wamonelea ya kwamba ni vizuri bwana akifa awe ana riidhi mali ya bwanake kuliko kunyanganywa ni familia, ndio hapo Katiba

ikirekebishwa irekebishwe hapo, pia tukisimama upande wa administration nivizuri watoto wetu wawe wakihudumiwa ki sawa sawa kwa mfano kama wakati huu mtoto wangu wakiingia ofisi ya Chief au assistant Chief anaulizwa mambo hayo na hayo, ni vizuri Katiba ikirekebishwa watoto wetu wahudumiwe ki sawa sawa katika ofisi za administration, kwa hivyo ni vizuri ikiwa ako na birth certificate na ako na kitambulisho ya mama na baba ni vizuri apate kitambulisho kisawa sawa.

Pia upande wa MP akina mama wamependekeza ya kwamba ni vizuri MP awa na degree na pia awe na miaka 35 hadi 70 na pia awe ako qualified na degree na awe ni mzaliwa wa mahali anapo taka kuchaguliwa, pia wanawake wahusishwe ikiwa ni kama kuna plot akina mama katika Kenya hii, ikiwa kuna mashamba ya Serikali akina mama wawe wana husishwa wanapatiwa ma plot ili mipango yao na mambo yale wanafanya wawe na pahali pakufanyia kwa sababu kama sisi tuna mambo mengi, tuna mifugo na tuna kuku na hatuna pahali pa kuweka sasa je Serikali ikiwa kuna pahali wanaweza kupatia hawa wanawake ni vizuri wapate sababu wanahangaika na Serikali iko yakujali maslahi ya wanawake.

Pia akina mama wanapendekeza ya kwamba, watoto wao wanaolewa America na wana zaa watoto pia tunashida moja hapo wanataka Katiba irekebishwe sababu huyu mtoto wake amezaa mtoto na bwanake ni muamerica huyo mtoto ako shida kwenda America sas akina mama wanaomba Tume wakirekebisha Katiba upande wa watoto hapo warekebishe ki sawa sawa sababu sisi tuna shida. Na kwa hayo machache Mungu awabariki.

Com. Hassan: Asante sana, thank you very much Susan. Simon Kamau, Simon Kamau

Simon Kamau: Asante sana kwa kunipa nafasi hii, wale wahakuwa majina yangu naitwa Simon Kamau, mkulima kutoka sehemu za baharini, kidogo sijui nilikuwa na point zangu hapa na nyingi naona kama zimepitiwa pitiwa na wenzangu ambao wanazungumzia lakini na naona bora tu ningepatiwa hiyo muda nijaribu kufafanua kidogo, kuhusu hizi points. Ya kwanza ni kuhusu uchaguzi, mara nyingi nchi nyingi tunasikia hasa hasa vita vinatokea kwa sababu ya uchaguzi kwa mfani Zimbabwe, Zambia juzi juzi tumesikia kulikuwa na mgogoro wa uchaguzi, sasa katika Katiba yetu ya Kenya, mimi ningependekeza ya kwamba kura zinapo pigwa pale pale katika kituo cha kupigia kura, kura hizi ziwe zinahesabiwa pale pale. Na agent ambao ni wa vyama hawa wagombea, watachukua idadi ya kura ya kila mgombea kwa sababu mara nyingi kura huwa zinapotea njiani, masanduku yanasafirishwa usiku na hata kule zinapokwenda kuhesabiwa mara nyingi tunasikia kuna ma agent Fulani huwa wanafukuzwa nje na kura zinabaki zinahesabiwa na ma agent wa vyama vingine.

Ya pili ni kuhusu elimu. Elimu kwa kweli tukiangalia katika shule za msingi mzazi amewachia kila kitu, mzazi anamnunulia mtoto daftari, mzazi ananunua vitabu ana jenga na katika Serikali kuna wizara ya elimu. Na wakati Bunge inaposoma yale makdirio mapato na matumizi, ile wizara ya elimu kuna pesa inatengewa, je zina enda wapi? Mimi katika Katiba ya leo ningepomba Katiba hii elimu itolewe bure, kuanzia msingi hadi sekondari kwa sababu hata Sekondari mzazi natumia maelfu ya fedha kumnunulia mtoto wake vitabu na hapo tunajua ya kwamba kuna ile wizara ya elimu na imetengewa pesa.

Ya tatu, ni kuhusu afya, siku hizi mara nyingi hospitali zimekuwa ni za malipo, ukienda Lamu wakati huu kama ni operation, unatoa shilling elfu tatu na ni hospital ya Serikali. Na katika nchi hii kinsa Serikali na kuna wizara ya afya na ina tengewa fedha, kwa nini hizi fedha hazinunui madawa, au hazitoi huduma ya bure? Kwa hiyo katika Katiba yetu, ningependekeza kwamba mambo ya afya Serikali itoe kwa mwananchi wake bure bila malipo.

Ya nne ni kuhusu Katiba hii ambayo tunabadilisha ningeomba Katiba hii iandikwe kwa lugha ambayo inaeleweka na kila moja hasa hasa angawaje nchi yetu ina wasomi, kuna baadhi ya watu ambao hawakusoma hawajui kiingereza ingefaa iandikwe kwa kiswahili na kiingereza ili kila moja awe akisoma na awe akikujua wakati anapokonya haki zake.

Ya tano ni kuhusu mali ya uma, mara nyingi tumesikia kuna ufisadi (corruption), mtu ni mkubwa katika ofisi, anaharibu pesa za uma au mali za nchi, lakini Mahakama haina uhuru wakumhukumu, hata kama anapelekwa Mahakamani kwa kweli hukumu inaotolewa si yakulipisha kulingana na kitendo kile kwa hivyo ningeomba Katiba hii ambayo unaibadilisha mtu kama huyu achukuliwe hatua kali na hata kama ni kufungwa na kufukuzwa kazi na anao utajiri mali yake iuzwe hizo pesa alizo chukuwa za wananchi zirudishwe katika hazina ya wananchi. Ya sita ni kuhusu cheo cha Rais, Rais anakuwa kila kitu ni yeye yuko juu ya sheria kwa kweli, mimi ningeomba awe chini ya sheria hata kama atakosea ashtakiwe. Juzi juzi tu tumesikia huko America Rais Bill Clinton alipelekwa Mahakamani na ile nchi kubwa katika dunia ina uchumi mkubwa Rais wake anashtakiwa kwa hiyo ningeomba hata Rais wetu wa Kenya ashtakiwe endapo atapatikana na makosa akiwa ofisini.

Ya saba ni kuhusu vyombo vya habari, radio na television ningeomba Katiba hii itoe huru kwa vyombo vya habari. Tukiangalia katika radio yetu wakati huu inamikiwa na chama kimoja na hadi nchi yetu ni vyama vingi, mara nyingi utasikia inatangaza tu habari ya chama kimoja, kwa nini isitangaze habari ya vyama vingine na hata viongozi wa vyama vingine wamefanya hivi hivi?

Tunasikia taarifa ya habari inachukua karibu robo tatu zinasomwa juu ya mtu moja kwa hiyo mimi ningeomba ya kwamba vyombo vya habari viwe na uhuru vya kutangaza kiongozi yeyote amefanya awe ni wa chama gani au chama gani kwa sababu hata yeye anashiriki kulipa kodi ambaye inaendesha vyombo hivi, magazeti mara nyingi waandishi wa habari wanakamwata kwa sababu yakuandika ukweli kwa hiyo ningeomba kuwe na uhuru huu wa vyombo vya habari.

Ya nane ni kuhusu fedha za nchi, mara nyingi unakuta kwamba kama wakati huu sura ya noti ni ya Rais huyu anayetawala wakati huu, mimi ningependekeza katika Katiba ambayo tunaelekea kuibadilisha, fedha zetu ziwe na sura ya Rais mwanzilishi wa taifa hili na hii kwa nini, hii ni heshima kwa huyu mwanzilishi wa taifa ambaye aliweza kupigania uhuru na nchi yetu ikawa huru, kwa hiyo, ningependekeza noti yetu ya taifa au pesa zetu noti, isiwe ikibadilishwa kila baada ya Rais huyu anaondoka mwingine anaingia anchapisha sura yake, tuchukue mfano kama marekani, dollar unakuta sura ni ile ile ya Rais wa kwanza kwa hiyo ningeomba Katiba yetu tuangalie mambo ya fedha kwa heshima ya viongozi wetu ambao walitulete uhuru na ukombozi katika nchi hii.

Ya tisa ni kuhusu Bunge, mara nyingi utasikia katika majadilioni ya Bunge badala ya Mbunge kuongea moja kwa moja katika radio, maani mazungumzo yake kurekodiwa tu na yanasomwa na mtu mwingine, mimi mara nyingi ni msikilizaji was redio na hata redio za nje nimesikia mfano wa ndugu zetu watanzania mbuga anaongea katika Bunge moja kwa moja na watu wale waliomchachagua wanamsikia kwa hiyo ningeomba hata Katiba yetu ya Kenya ambayo tunaelekea kubadilisha, Mbunge akiingia Bungeni awa akiongea moja kwa moja bila mazungumzo yake kumpitia mtu mwingine.

Ya mwisho nikuhusu mkulima, mimi ni mkulima si fanyi kazi popote isipokuwa kazi yangu ni kilimo, ningeomba Katiba hii itujali zaidi wakulima kwa sababu sisi watu wa Mpeketoni au watu wa Kenya ni watu wenye bidii wanalima na Mungu ametubariki tuna mvua nzuri na ardhi nzuri lakini bei inakuwa si yakuridhisha na hata Serikali haimjali mkulima unasikia Serikali inaongeza mishara kwa wafanyi kazi lakini mkulima hatajwi katika mambo hayo yakumfikiria kwa hiyo Katiba hii imfikirie zaidi mkulima kwa sababu mkulim huyu ndie uti wa mgongo wa taifa letu na hata Serikali yenyewe inamtegemea huyu mkulima kwa kupata fedha za kigeni na kwa hayo machache yangu ni hayo asante.

Com. Hassan: Asante sana mzee, thank you very much. Kennedy Omangi, ameondoka? John W. Kabira.

John W. Kabira: Kwa Tume wa marekebisha wa Katiba, wananchi wenzangu hamjambo? Yangu ni machache si mengi yakuhusu Katiba ile tunae, ma ile tunaelekea kurekebisha, kwa hakika Katiba ile tunaelekea kurekebisha kwa maoni ningependa Serikali ya Kenya iwe ya mwananchi, kuwa ya mwananchi, kuwa ya mwananchi ni Katiba isimamie mwananchi ipasavyo maana Katiba ndiyo mwananchi, mimi sina mengi yakuongea lakini nitagusia kidogo, kuhusu Ofisi ya Rais, Ofisi ya Rais mambo yote ya Rais iwe ni Rais tu peke yake, mambo si jeshi, mambao waziri mambo ya hospitali iwachiwe yule anayehusika naye.

Ya tatu ni kuhusu afya, kusema hakika sisi wananchi wa kawaida hana shida chungu mzima, sababu uende hospitalini ukiwa mgonjwa kwa hakika unaambiwa hakuna dawa, medical center pale unaambiwa enda ukatafute dawa wa sukari, tungependela hii Katiba yetu isimamie mambo kama afya, mambo kama elimu, mambo ya matumishi yote ya mwananchi maana Katiba ni yake mwananchi. Paispo mwananchi hakuna Katiba kwa hivyo ningeomba Tume ya marekebisha ya Katiba isimamie haki ya mwananchi, mimi sina mengi na ni hayo tu. Asanteni sana.

Com. Hassan: Asante sana mzee. Sasa ni Bwana Joseph Nyakundi wa Kanu, hayuko? Simon Njagi.

Simon Njagi: Asante sana Chairman, Tume ya marekebisha ya Katiba na wananchi wote. Nashukuru kwa muda huu ambayo nimepata kwa hakika mengine yamezungumzwa na hata nimefurahia maanake mengi kama yake ambayo nilikuwa na lengo nayo lakini kuna mengine labda hayajaguswa sana na ningetaka kuchukua nafasi hii kuyazungumza. Kwa majina ni Simon Njagi Kareithi – ni mwakilishi wa walemavu.

Ya kwanza hebu niseme katika jina ile ya walemavu uona kama ni matusi wakati wanasema viwete, kiwete hiyo si jina kabisa yakuweza kuita hawa ni walemavu ama watu siyo watu wasiyojiweza ni walemavu, uenda ikawa kuna mlemavu anajiweza labda kuna mwingine anayejiweza kama vile hata yule si mlemavu huenda akawa labda kuna wao ambao hawajiwezi. Hebu nizingumzie habari ya elimu ya walemavu. Ningeuliza katika Katiba hii mtu yeyote ambao ni mlemavu yapaswa apewe elimu ya bure kwa masomo yake yote kwa kuwa wakati mwingine huwa wanawekwa kando hawapati watu wakuwa simamia hali ya masomo. Kwa hivyo, Serikali iwe inaona kabisa mlemavu hata afike mahali gani masomo yake iwe ikisimamiwa. Ikiwa kuna mtu yeyote ambaye anatumia njia yeyote yakuzuia masomo ya mlemavu, ningeona Katiba hii itoe hukumu ya kwamba achukuliwe hatua ya kisheria.

Katika District zote kuna umuhimu kuwe na kituo vya wale ambao ni mentally retarded, na wale akili punguani na wale completely retarded, disabled wale ambao hawajiwezi kabisa kwa walemavu, ili kusije ikiwa na hii safari za kuwapeleka watu walemavu katika vituo vya mbali ambavo wakati mwingine wazazi na wale wanahusika wanashindwa na kuwapeleka. Tena katika haki ya matibabu ufanye mbinu yeyote hawa walemavu iwe matibabu yao iwe hayalipishwi kuonekana itafanyika namna gani ili mlemavu katika kila njia apewe matibabu ya bure.

Kwa ajali ya mambo ambayo inahusika na rasilimali, walemavu huenda wakawa wako na kuna vitu kama biashara na vitu vingine, ningeuliza katika Katiba hii Serikali ione ya kwamba haitozi ushuru wowote ama kodi yoyote katika vitu vya walemavu, iwe ni biashara iwe ni property ya aina yeyote iwe ni tax free kwa walemavu. Tena katika manyumba yeyote ambayo ni ya uma public houses iwe accessible kwa mlemavu, iwe inaweza kuingika ni mlemavu yeyote, hakuna haja mtu akuja na wheel chair halafu katika hapa hawezi kuingia kwa sababu kuna stair, kuwe kuna sheria yakuona kumefanyika njia yakuweza kuwa mlemavu anaweza kaingina kama ni kanisani, popote amabapo ni pa uma ama kama ni shule, iwe kuna mambo kama hayo ambayo mlemavu naweza akaingia.

Tena ikiwa ni wale ambao kuna mashamba na mambo mengine, Title Deeds zao zisije zikawa zikilipishwa, maanake labda mlemavu anakuja labda (inaudible) tena anaendelea kuonekana mambo yake inaendela awezi, kwa hivyo ikiwa atapewa Title Deed awe ndiyo Serikali itaona ya kwamba huyu mlemavu, aendelei na nakunyaangamizwa katika njia ile.

Tena kitu cha maana sana ni wakati hawa physical planners wanapo fanya plan katika towns waone ya kwamba, wame set aside hata kama labda hakuna watu wakutetea kwa wakati ule, plots ambao labda huweza ikapewa (inaudible) with disability kwa ajili ya maendeleo yao, ama ikapewa kila association ya walemavu kwa ajili yakujenga mashule kama ambaye tumesema ama vile nimesema, kwa hivyo uwe ukionekana hata kama hakuna nini utengwe vitu kama hivyo.

Na watoto nao walemavu maanake walemavu wana watoto wao lakini wakati mwingine kuwasomesha inakuwa ni shida ningeuliza katika Katiba hii watoto walemavu wapewe elimu hadi kufikia kisomo cha university ama college, ili wale watoto waweze kumsimamia yule mlemavu katika hali hiyo.

Kitu ambacho ni kwa upande wa walemavu ningetaka kumalizia nacho ni upande wa nitaita nini discrimination yaani ubaguzi, ubaguzi umewaka sana katika upande wa walemavu, utakuta kwa ajili ya kuajiriwa makazi, masomo na mengine wanabaguliwa. Hata si ajabu utakuta labda ijapokuwa kuna watu ambao wangeweza kufanya kazi utakuta hata kama wale unafanya kazi hapa hakuna mlemavu utakaye muona hapa.

Kwa hivyo ni Serikali ione ya kwamba ime condemn ama imetupilia mbali ile habari yakubagua malemavu, maanake hata kama ni wakati watu wanapewa ma plot kama hapa, utakuta maanake mtu mlemavu hawataki si sana awe considered, ama atakaa kama ile group inataka vitu kama vile, inaonekana tu ni walemavu. Kwa hivyo walemavu wanaonekana kama hawana chochote ati wakafanya.

Kwa hivyo katika hali hiyo nikiondoka kwa upande wa walemavu. Mambo ya basic right, mambo kama hii health care, maji, elimu na mambo mengine ningeonelea kabisa katika Katiba mambo yale yawekewe maanani kabisa ili iwe watu wanapatiwa ile haki ya kimsingi. Na sasa ukiangalia upande wa hospitali wakati mwingine unakuta mambo mengine watu wanaweza kufia pale na hospitali iko maanake hana pesa, kuwe kuna jambo lakufanya mambo haya, mengine yametokea kwa kuwa labda watu wanaenda kufia pale na hospitali hiko maanake hana pesa. Kuwe kuna jambo lakufanya mambo haya, mengine yametokea kwa kuwa labda ni kama vile moja alisema kule kuunganisha kazi nyingi, yule daktari yuko katika hii hospitali ndio mwenye clinic yake pale. Kwa hivyo inaonekana kama ingewezakana wale ambao wanasimamia ma hospitali wawe hawana mambo mengine kule nje.

Na upande nao kama ule wa Judiciary ningeonelea katika hali yake avoid wale ma staff wa Judiciary, kuwe kuna kamati ambao limeteuliwa na Bunge kwa ajili yakuchunguza ama kwa ajili yakuavoid ma Judges hii ikiwa na maJudges, ambao hawapendelei upande wowote ili waweze wakasimamia mambo kisawa sawa. Lakini kuna mengi nilikuwa nimeandika lakini badala ni watu wengine nafasi kwa kuwa mengi nimeona imezungumzwa na nitwacha hii ripoti hapa nashukuru kwa hiyo nafasi nimepewa na Mungu abariki sana.

Com. Hassan: Asante sana bwana Simon, tafadhali tupigie kidole hapo register na u sign hiyo memorandum. Tutakuwa tuki break ikifika saa saba, we shall break for lunch at one o'clock tutarudi saa nane tena kuaniza. Kwa hivyo nataka mujue lakini imebaki bado dakika ishirini tunaweza kuendelea, lakini mujue tuna break for lunch at One o'clock kwa hivyo Peter Njihia, atafutiwa na Maina Kairuki, kama hayuko Jacklyne Mutulu, halafu Alex Kitetu Wahiti, nafikiri hawa watu wote wanaweza kusema by 1 o'clock.

Peter Njihia: Thank you very much jina langu Peter Njihia I am here for the labourers, wafanyi kazi wa shamba (inaudible) na pia the very poor. The landless, housemaids and those (inaudible) First please allow me to criticize the Constitution Review ile ambao tunafanya kwa sababu one thing, hii Constitution review inafanywa kama most of the people hawaelewi what the

Constitution is, sasa tunaambiwa tutoe maoni kwa kitu ambayo siyo kitu original ni kitu ambayo tuna review na hatuielewi sana.

Second, I also criticize it kwa sababu much of the Constitution ilipatikana kutoka kwa foreign countries mostly copied from British na pia utapata some elements za America ambazo hazikuwa zina incorporate tradition za Africans na watu wengi wa Kenya. Kutoka hapo Kenya is in a transition, mbeleni tulikuwa tunaishi maisha ya ki utamaduni kama wa Africa. Tuko kuna zile njia wa Africa walikuwa wanaishi na hayo uchumi ya ki Africa haikuwa kama ile ya wazungu ambae imeletwa na ukiangalia Constitution imetetua katika uchumi za kiuzungu na sisi bado hatuja weza kuingia zile uchumi kabisa, so we are settling on something ambayo si original sana ya kikwetu lakini tunaangalia sana, yaani we are on a transition. Kwa hivyo hatuwezi tukatoa kitu original kama vile tungefaa, tutoe kama completely independent. Sasa jambo lingine la kwanza sasa kwa Constitution (inaudible) on citizenship sasa nitasoma kwa haraka haraka ndiyo nimalize.

Com. Hassan: Hapana uwezi kusoma yote mara moja, sitaki usome neno kwa neno hiyo submission jaribu tu ku highlight ile mambo muhimu kwa hiyo, tukakaa hapa mpaka jioni.

Peter Njihia: Kuhusu uraia.

Com. Hassan: Ngoja, umenifahamu kwanza?

Peter Njihia: You are telling me to summarise

Com: Hassan: Yes please.

Peter Njihia: Kuhusu uraia, kila mwana Kenya anafaa apatiwe pahali pakuishi, ambako hatawai itishwa rent ama kuogopa kuondolewa. MKenya yote anafaa awezeshwe kuishi katika nyumba ambao iko decent. MKenya yote anafaa awezeshwe kuweza kupata mapato kwa sababu wakati wengine ukiangalia hakuna employment wakati mwingine mtu hana watu wakutegemea so inakuwa ni very ...(inaudible)... for somebody to get subsistence. Sasa pia kuna ile ambayo ni obligation of a citizen, every citizen in Kenya should be obligated through enforceable law to develop Kenya by engaging in constructive work, using ones resources (inaudible) Kenyanization.

Every Kenyan citizen should be obligated through enforceable law to protect Kenya by among other things, one protecting Kenya from degradation by environmental pollution, receiving bribe and immorality, protecting Kenyan ...(inaudible)... Protecting Kenya from its wealth through waste or theft, protecting Kenya from unfair exchange of its wealth with other Nations.

Na kama hapa hivi nazungumzia kuhusu kama wale watu wanaenda kuajiriwa nje unaweza pata mKenya ametoka hapa ako na ujuzi mwingi lakini anaenda kuajiriwa kama South Africa au U. S. au kwingineko, hiyo akili yote inaenda kupotea kule, lakini sisi wa Kenya hatufaidiki kwa ile akili, na kwa vile yule ni wetu yafaa sisi pia tukifaidika. Hatujui kama wakileta taxes or whatever they do.

Sasa kuhusu mambo ya ardhi, kuna ile Ownership of Land : Owersnship of the land should belong to the State kwa sababu you find that there are some Kenyans who own ten thousand acres, others 50,000 acres and there so many Kenyans ambao hawana ardhi yoyote, sasa itakuwaje mtu anasema ni mwana nchi wa Kenya hata una pahali pa kuishi, hata namna yakupata pesa, yaani chakula ya kila siku halafu we utasema ni mwana Kenya na mwingine ako na mali nyingi kupita kiasi chake. The State should have the power to control the use of land, tuseme wakati mwingine mtu anaweza kuwa ana acre mia moja lakini zile acre hazitumii vizuri, kule ndio wanayama wanacheza au pengine kwa hivyo vile ako ni ile ardhi haifaidishi Kenya kulingana na vinavyo faa.

Wale ambao si wa Kenya (non-citizens), should not be allowed to own land in Kenya, unless through proxies, who are Kenyan citizens and strictly for the purpose of business or habitation. Unaweza kupata mtu ambaye si wa Kenya amekuja kwa vile ako na pesa mingi ana nunua ardhi kubwa lakini hii si mzuri kwa wana Kenya. The independent land treaties and any agreement that have been passed todote that do not maximize land production should be cancelled and declared null and void. Utapata kuna agreements zilikuwa hapo mbeleni, unaweza pata kwamba kuna agreement imesemakana sijui kutoka wapi mpaka wapi huko ni kwa wa Masai, hiyo siona kama iko na faida kwa wanaKenya ambao wanaendelea. Utakuta pia watu wengine wanasema tuseme Coast Province hiyo ilikuwa ni land ya Sultan, kusema land ni ya Sultan haifaidi, lakini kudevelop ile land so that inakuwa production yake inasaidia Kenya naona kama hapo ndio kuna faida. Halafu Constitution should only guarantee access to land for every Kenyan for the purpose of (inaudible)

Ingingine ni Insurance Policy for farm produce ama land production, wakati mwingine unaweza pata we ni mkulima ile mazao unazalisha baada yake kuzalisha ile mbegu unauza haupati chochote, sasa inawezekana hata hutaweza kuendelea na kilimo sana, sasa mimi naona Constitution inafaa create an Insurance Policy whereby ukipatiwa land u develop au kutoa production ile insurance covers of the lands which you are using, such that hata ukienda hasara itabidi utaweza kuanzisha tena. Pia if the Government iko na ile obligation, yakupatiana insurance katika ile uzalishaji wa ardhi itaweza pia kutafuta soko ya ile mazao itatoka kwa ile ardhi.

Kutoka kwa ardhi kuna mapato mengi ambayo huwa inapatikana na unaweza pata kama hapa kuna maembe mingi sana lakini hakuna factory hata moja yaku process maembe, zote zinaenda kuwa processed Nairobi au kwingineko, sasa mimi naonelea Katiba inafaa isisitize kuwa kama sehemu fulani inatoa kitu fulani kwa wingi, zile factory za ku process hiyo mali ziwekwe kule na ndiyo hata wale watu ambao wanazalisha hiyo mali wanufaike zaidi.

Sasa kuna jambo moja nilikuwa nimeruka pale kwa citizenship, inafaa Constitution isitize kuwa raia wa Kenya ni mtu muhimu sana, siyo mtu wakwenda kuteswa na polisi, siyo mtu akipita pita usiku anakuwa harassed, siyo mtu akitaka hata kula huwezi ukapata chakula kwa sababu hakuna njia zakujipatia, hakuna kazi, hakuna nini, so Constitution inafaa i create hiyo nafasi kuwa a Kenyan is the most important person in the Constitution.

Com. Hassan: Thank you very much, I can see you had a written submission, but here in the register you wrote oral, I wish you had written here also.

Peter Njihia: Yes.

Com. Hassan: You are Peter Njihia, then I am replacing it to written, Maina Kariuki, Jackyln Mutulu, hayuko? Alex Kitetu, hayuko, Alex Kitetu, are you Alex, you will be the last one to give views for lunch, we are going to break for lunch.

Alex Kitetu: Jina yangu kama vile mulisikia ni Alex Kitetu, kwanza na naanza na upande wa mamlaka, na mamlaka nikueleze (inaudible) katika Serikali yetu unakuta mamlaka ni kama iko kwa mtu moja, ikiwa ni Ofisi ya D.C. unakuta mamlaka ya District mzima, kwa mfano umeenda kwa D.O. unashida huyo D.O. anakuambi hii shida nilitua namna hii yule juu yako nilimfuta kazi, sasa sisi wananchi tunataka hiyo iondelewe kabisa, kama ni mamlaka iwe ni ya D.O. ikiwa kesi mambo ni kuamuliwa kwa D.O. siyo isukumwe mbele. Mamlaka kuna kesi ambayo imetokea mwanamke moja alikuja akafa, no bwana ya mtu akafa, sasa inasemekana yule anazikwa na family yake, lakini si tungependa ikiwa bwana amekufa yule bibi ambaye atabaki awe na mamlaka yakuzika bwana yake na ile mali atuae lakini si kama mimi nimeoa, mimi nimemuoia kwa mfano mimi nimeoa msomali, mimi nikifa yule Msomali hana haki yakunizika naye ni bibi yangu inafaa iwe kama nimekufa yule msomali anizike maanake yeye ni bibi yangu ndio ile mali ibaki kwa watoto wangu.

Ya pili kuna hii mambo ya ulinzi unakuta (inaudible) ingine ile laini ya ulinzi ni members wa Human Rights ikiwa ni Army, ikiwa ni Polisi au ni G.S.U ni members wa Human Right wakati anavotumwa hata wakuhudumie akifika kwako, siyo atumie excessive force anatumia ile force akiogopa kuwa huyu (inaudible)

Ya nne pia hii Katiba mpya ikibadilishwa tunataka kila mwananchi awe na haki yakula matunda ya nchi yake ikiwa mimi nimelima pamba, na mahali hiyo pamba inapelekwa kilo ni shilingi mia, hiyo shilling inifikie siyo nifikie na shilingi ishini hii ingine themanini inakuwa imeenda wapi?

Ya mwisho ni kuhusu vyama mambo ya vyama hapa imezungumzwa sana, na mimi ningependekeza kuwa vyama tubaki na vitatu peke yake. Ndio hii mambo ya ukabila iweze kwisha. Maanake vyama vilivyo anza niliona kila moja ikitoka na mimi na changu, na mkamba anaenda kwake ni mjaluo anaenda kwake tunatakiwa tubaki na vyama vitatu na wale ambao vyama viao havina nguvu waunge wale wengine mkono iwe tuunde vyama vitatu ambao nguvu sawa ipatikane na kila mwananchi aridhike.

(inaudible)

Com. Hassan: Asante sana. Thank you very much Alex Kitetu huyo ndio atakuwa mtu wa mwisho kutoa maoni kwa wakati huu kama vile nimesema tuta break for lunch na tutarudi saa nane, nafikiri tutarudi saa nane na nusu kamili kwa sababu kuna wengine wataenda mbali, so we will break now for lunch and will come back at 2.30. Thank you very much.

Dr. Mosonik: Unajua maoni ni kwa Tume.

Com. Hassan: Kaa kwanza, naonekana wewe unahitaji kidogo kupewa masomo kidogo

Peter Kariuki Wanjohi: Masomo ya hawa wengine?

Com. Hassan: Hapana vile tufanya kazi, leo ni kikao hiki ya Tume yakurekebisha Katiba tumekuja Lamu West Constituency, jana tulikuwa Lamu Town, leo tuko Mpeketoni na tunachukua maoni ya watu, so that tukishindwa tunachukua maoni tunaandika, pia tuna record kwa tape, kwa hivyo wewe unatoa maoni kwetu siyo kwa watu wa Mpeketoni. Sasa sisi tunaanza kikao cha jioni cha afternoon session, tutaanza na wewe utatupatia jina lako ndio tuaanze na wewe, utatupatia jina lako,

Com. Mosonik: Mwambie andike jina kwanza

Com. Hassan: Umeandika jina yako hapa kwa register?

Peter Kariuki Wanjohi: Nimeandika pale nje.

Com. Hassan: Oh nje? Okay sawa

Peter Kariuki Wanjohi: Naitwa Peter Kariuki Wanjohi, Sasa yale maoni ambao niko naye katika Constitution Review, kwamba Constitution should say that it belongs to the people of Kenya as its preamble ambao ina recognize the (inaudible) and the will of Kenya. Na ya pili ni ya kwamba Constitution should (inaudible) the the organs of the Government. The Constitution
Future and objective and democratic (inaudible) that Kenyans should be committed to.

Com. Hassan: Interjection (inaudible)

Peter Kariuki Wanjohi: Kwa hivyo nianze tena.

Com. Hassan: No no sawa endelea.

Peter Kariuki Wanjohi: Injine ni kwamba the Constitution should remind Kenyans, the duties of the Head of the State and the Head of the Government, plus who qualifies to this post. The Constitution should provide clear checks and balances of the the three arms of the Government, the Constitution provide clear checks and balances of the three arms of the Government Ni endelee na hiyo?

Com. Hassan: Si hiyo utatupatia?

Peter Kariuki Wanjohi: Ndio nitawapatia, sasa hapa the three arms should incorporate serving the wananchi but not (inaudible) or depending on one arms for the decision making. In any event all the powers should not be vested to the President. If we talk (inaudible) appointing of our Executive, MPS, Cabinet Minister, Attorney General, hii yote mimi singependa iwe ni President ana appoint. The Constitution should provide the respect and the rules of the law, nobody should be placed above the law e.g. President Moi in the Kanu Government.....

Com. Mosonik: Interjection, excuse me you said President Moi?

Peter Kariuki Wanjohi: The President of Kenya.

Com. Mosonik: Because if you are dealing with Moi then it is not the same thing as President of Kenya.

Peter Kariuki: Oh Constitution, the President of Kenya.

Com. Hassan: Don't name individuals.

Com. Mosonik: Afisi, Afisi siyo mtu.

Peter Kariuki Wanjohi: The President of Kenya. The Constitution to set good mechanism of checking the abilities of the President of the ruling ...(inaudible) ... that is to say he should not ...(inaudible) health, physical of mental. All the members of the Judiciary should be covering security of tenure for them to be impartial. Secondly a good salary for them (inaudible).

Com. Hassan: Thank you Amemaliza?

Peter Kariuki Wanjohi: Also we need an independent Electoral Commission, kuna hii injine ya Human Rights, rights to education, good health, physical environment, freedom of movement, owning property anywhere in Kenya, the right of

assembly and association and good shelter nafikiri yangu imefika hapa.

Com. Hassan: Asante sana. Thank you very much Mr. Kariuki please sign for us the register, and have you signed the submission?

Com. Hassan: Just bring it back. Our next person Mohamed O. N. K.U.

Peter Kariuki Wanjohi: mimi nina maoni mengine kidogo ya mwisho.

Com. Hassan: Hujamaliza?

Peter Kariuki Wanjohi: Bado sijamaliza kabisa kuna kitu nilikuwa nataka sema Commissioner. Pia nilikuwa nikitaka kusema tu juu ya Commissioner mimi naona mnamefanya kazi mzuri, lakini mimi naende kuomba Prof. Yash Pal Ghai is not a Kenyan, nyinyi Commissioners mumechaguliwa hapa katika Kenya nyinyi ambaye ni watu wetu ya waKenya wote kwa hivyo, anything ambayo inaweza kwenda vibaya (inaudible) for Mr. Ghai, hata mkifanya vizuri mnaafanya vizuri kwa sababu ya wa Kenya wote 30 million.

Com. Hassan: Nilikuwa nikitaka nikufanyie correction moja, Prof. Ghai ni MKenya, amezaliwa Ruiru, lakini ni vile tu haja kaa Kenya kwa muda mrefu sana, lakini kwa kweli yeye ni mKenya pia wa kuzaliwa hapa.

Peter Kariuki Wanjohi: Sawa kama ana julikana hivyo ni sawa.

Com. Hassan: Okay now Mohamed N. Kejo yuko, kuna mama hapa anajaribu kutoa maoni, wewe, anza na jina.

Bariki Athmani:- Kwa jina naitwa Bariki Athmani - Kanu Chairlady Witu.

Com. Mosonik/Com Hassan: Ulikuwa umejiandikisha, umejiandikisha?

Bariki Athman: Ndio nimejiandikisha.

Co. Hassan: Bariki Athmani:

Bariki Athmani: Ndio- Nakifiri Commissioners wananchi wote wa Lamu, habari zenu? Nimesimama hapa mimi leo, sina madhumuni yakuzungumza maneno mengi kwa sababu maneno mengi nimeandika kwa hii kitabu na nitwaachia Commissioner

wataenda nacho. Lakini nataka kuongezea kidogo, madhumuni ya Katiba yetu tutakayo kuirekebisha leo, tuirekebishe vilivyo, (inaudible) mambo mengine mengi yatakaa kutilia uzito; kama mambo ya ardhi,hati ya ardhi na mali, kifungu ya ardhi na mali, hati ya ardhi na mali sisi huku watu wa Lamu ni wakulima hatuna kazi nyingine hatuna mafactory hakuna kitu chochote, kazi zetu kubwa factory yetu ni jembe na mchanga, leo hii mchanga Serikali inatupatia settlement. Tumepewa kweli, lakini tumewekewa vikwazo vya kulipa pesa nyingi, mwananchi wa kawaida(inaudible) tukilipa, kulipa ile (inaudible) ya Serikali.

Kwa hivyo tunataka katika Katiba ijao, mwananchi apewe ardhi ambae ni haki yake, pahali amezaliwa hata kama hakuzaliwa, madama anajiita Kenya amepewa...(inaudible)...amepewa asiwe anadaiwa pesa nyingi saa zote mpaka ashindwe kulipa, (inaudible) kila kitu. rasilimali yangu na watoto kwa watoto wangu na family yangu, kisha shamba hile hile ambibiwa kama nimeshinda kulipa shamba ya ni ya Serikali. Kwa hivyo lisiwe shamba ni ya Serikali, shamba madam nimepewa ni langu, kulipa ...(inaudible) ..kidogo ambao haki ya Serikali tusaidiane ni toe kitu kidogo, lakini siyo kuwekewa vikwazo kama kwetu Witu saa hii ukipewa shamba unalipa, thelatini na tano elfu. Sasa na hali zetu ni hali mashamba yetu bado ni pori kwa hivyo hali ardhi na mali katika Katiba iwe mwananchi wa kawaida anapewa shamba bure.

Halafu katika hiyo hiyo, ardhi utakuta saa nyingine umekaa nyumbani na sasa sisi ni viongozi utakuta watu wa settlement au idara fulani wako mashambani wanafanya kazi fulani bila kujulisha (inaudible) hawajui chochote...ukiwa kama ofisi unapewa hiyo kazi ofisi. Kusifanyike kitu chochote katika Katiba ijao tunataka kusifanyike kitu chochote kuhusu habari ya ardhi mpaka tushirikishwe sisi wenyewe turidhike nani (inaudible) fulani atapewa shamba na mdomo wetu.

Halafu jambo jingine kuna habari ya katika Katiba ingine tukirekebisha leo kuna hii habari ya Katiba iangalie sana na nyinyi Commissioner mfikirie sana mukienda katika hali yaku kaa kugau kagua haya maneno tuzungumzayo msichukue moja kwa moja sababu kuna na upande wa dini, kuna na upande wa mila, leo hii msichana akishakupendana na mvulana wao (inaudible).....sababu kuna na dini, dini yako haikuhurusu kupendana na fulani kuolewa ovyo, ovyo mpaka tutie dini ndani kwa hivyo muangalie uhuru wa dini. Katika Katiba tuwe na uhuru wa dini ki sawa sawa dini ziangaliwe zote siyo dini ya Kiisalamu peke yake. Na mila ya binaadmu isi...(inaudible)..watu pia iangaliwe ki sawa kwa hivyo mimi mambo yangu yote tumekaa katika Witu Division tume pendekeza, Tumesoma kitabu ni mimi nilikuwa mojawapo wa kufundisha na tumeamua sasa maelezo yote yako humu na wakati nikama imekosea vile (inaudible) Kwa hivyo asanteni.

Com. Hassan: Asante mama, tafadhali utupigie sahihi kwa kitabu chetu na hii pia sign. Gitau A. Kamau.

Hadija Mohamed Bashir: Nilikuwa naomba hata mimi niandikishe kwa sababu kuna safari

Com: Hassan: Unaitwa nani?

Hadija Mohamed Bashir: Hadija Mohamed Bashir.

Com. Hassan: umejiandikisha? Haya sawa, Hadija

Hadija Mohamed Bashir: Ma Commissioner

Com. Hassan: Anza na jina lako

Hadija Mohamed Bashir: Kwa jina naitwa Hadija Mohamed Bashir, Ma Commissioner, wananchi wenzangu wote, je kina akina mama hawa wawili hata kama...(inaudible).....hamjambo? Mimi naitwa Hadija Bashir na nimetoka Witu Division, Mwenyekiti Maendeleo ya Wanawake, Witu Division - nataka nimujulishe maanake kupata nafasi saa zingine kujua vizuri. Katika kurekebisha hii Katiba yetu ya Kenya nilikuwa napenda kuzungumza juu ya mambo ya Kadhi, Kifungu cha Kadhi, ningependa kwanza Khadhi asichaguliwe na Rais Khadhi awe atachaguliwa na Waislamu, kwa sababu Kadhi ni mtu ambaye anatuhusu sisi Waislamu, kwa hivyo (inaudible).....atachaguliwa na Muislamu.

Na pia kwa Ofisi ya Khadhi kuwe na pengine msaidizi wa Khadhi awe ni mama, kwa sababu sisi wakina mama tukienda pale kwa ofisi ya Khadhi kwa malamishi yetu, mara nyingi mambo yetu huwa pengine huwa tunaona haya kuzungumza ama nini mambo kama hayo kwa sababu tukiwa na ule mama tunaweza kuzungumza na yule mama mwenzetu yule mama naye atamueleza yule Khadhi. Ningependa kwenye Katiba hii yetu iwe inahakikishwa kwamba kwa ofisi ya Khadhi, kuwe na mama moja ambaye atakuwa msaidizi wa Khadhi.

Na pia ningependa kuzungumza kuhusu wa kina mama naona mambo mengi ni kuhusu wa akina mama mnajua mimi nina wazungumzia akina mama wote, lakini hawa Waislamu ningependa (inaudible) naona kidogo mambo mengi hayakuzungumziwa. .Kwa upande wafanyi kazi, sisi wafanyi kazi, sisi wanawake wa Kiislamu huwa tunafanya, tukiwa tunafanya kazi kwa ofisi pengine napata msiba bwana yako akifiriki, huwa tuna kuwa ile sheria ya kidini, tuna miezi nne na siku kumi ambako ni muhimu sana, lazima tuwe hatuonekani kwa sharia ya dini, hata ningependa hii maneno ifikishwe kwa hii Katiba yetu, iingizwe hii Katiba yetu. Sisi ni wafanyi kazi wanawake wa Kiislamu hatuwezi kufanya, amepata msiba kama huu iwe ni lazima atapewa miezi mitano mapumziko na awe atanagaliwa kama kawaida. Hiyo nafikiri tulikaa chini tukaona hiyo tunakaa chini hiyo tunaomba hiyo tunaomba iwe kwa Katiba yetu ambaye tunairekebisha .

Jambo jingine nilikuwa ninazungumza kuhusu mambo ya hivi vyama vyetu wajua sisi Kenya tuko na vyama vingi sasa kusiwe katika hii Katiba yetu kuna chama kimoja hata kama sisi tunajua chama tulicho nacho kwetu nyumbani ni KANU lakini kisiwe ati KANU ndio inatambuliwa zaidi kuliko chama chingine. Kwa sababu ni (inaudible)...mtu kama pengine ni Chairman wa KANU mfano amekosea mtu ameenda kwa Polisi ameweka ripoti inakuwa sasa hawezi chukuliwa hatua yeyote kwa sababu yeye ni KANU Chairman, je DP naye ana Chairman wake FORD naye si anaye mbona haifanyi hivyo.

Kwa hivi vyama vyote, viwe ni sawa hata kama hatukatai KANU iwe nichama kinanchotawala lakini isichukuliwe hivyo kwa sababu si kufanya hivyo ni kunyanyasana mimi nimeone hivyo haswa mtu ana nyanyasa mtu ukienda kwa sheria kwenda kuelepeka ripoti sababu mtafanyiwa haki mtaangaliwa ki sawa ninambiwa aa kwa vile huyu ni KANU Chairman amefanya hivyo hata hawezi kupelekwa kortini inakuwa pengine kama watu nifanyie mambo yangu ikifika kwa OCPD, OCPD anarudisha hii maneno irekebishe maneno huko kwa sababu huyu ni KANU Chairman kwa nini nataka vyama vyote iwe ni sawa hiyo maneno isiweko, vyama vyote vionekana ni sawa. Asanteni.

Com. Hassan: Asante sana. Hadija tafadhali utupigie signature hiyo form. Ndegwa Ngechu, hayuko? Alfonse Moki, Fredrick Mugo, Paul Wachira, nani, Fredrick Mugo, haya

Fredrick Mugo: Jina langu ni kama hivyo umesikia ni Fredrick Mugo Githinji mkaaji wa Mpeketoni na mimi katika kutoa maoni unajua mengi yamezungumzwa wa wale waliotangulia lakini hata hivyo nitaongeza mawili au matatu.

Kwanza nataka au napendelea Katiba mpya ikatilie mkazo katika kufungua Ofisi za wabunge, Secretariat Offices kwa kile Constituency, mahali ambapo wakaaji wa eneo ile wataweza kupeleka malalamishi yao ile naye Mbuge akaweza kuyapeleka katika Bunge. Vile, vile hawa waBunge amabao wanatuwakilisha kule nimeona ya kwamba sehemu zingine za wakilishi Bungeni ziko na watu wengi kupita zile zingine na kwa hivyo representation inakuwa ni sawa, kwa hivyo napendelea Constituency ikawe demarketed au area of adjudication ya Constituency ikafanywe kulingana na idadi ya watu walioko katika eneo hile.

Kitu kingine ni ya kwamba siku ya uchaguzi ambao ni siku muhimu kwa sisi raia wa Kenya kutelekeleza demokrasia yetu ningonelea ikawe inatengwa na watu watajuwa kwa muda ili wakaweza kuji tayarisha katika kuenda uchaguzi. Vile, vile Tume ya uchaguzi Electoral Commission ambayo ni mmojapo ya Tume muhimu zaidi iwe na nafasi sawa au wakapate nafasi, au wakapate nafasi yaku appoint wale Commissioners.

Kitu chingine ni kwamba kuna kile chama cha wafanyi kazi Cotu, nataka au napendelea katika Katiba mpya wale ma ofisa ya ngazi ya juu wakachaguliwe na vile wale wanao husika lakini isiwe ni Serikali ambayo ita appoint. Secondly, next upande wa mawaziri, Ministers to be appointed on basis of profession. Walemavu, katika ofisi za raia au zile ofisi ambalo, kama ofisi ya D.O. naonelea ki Katiba kila ofisi zikawe zimejengwa au iko katika hali ambayo hata walemavu wataweza kuingia bila shida, accessibility to the public services.

Na mwisho ni kwamba kuna hawa Forces, Kenya Army, Kenya Air Force na Kenya Navy na maafisa wengine wa ulinzi ninapendelea wakawe recruited proportionally on basis of District, ikiwa ni wilaya ya Lamu wanapata watano, Tana River wanapata watano ili isiwe kwamba majeshi wote askari wote wametoka katika wilaya moja au jamii moja. Na kwa hayo ninashukuru kwa nafasi hiyo.

Com. Hassan: Asante sana. Thank you very much, can we have David Wainaina, David Wainaina hayuko? Omar Awadh, Paul Waithera, Mohamed Rashid, Ali Barak, Monica Maina

Monica Maina: Kwa majina yangu mulivyo sikia naita Monica Njeri Maina mkaaji wa hapa Mpeketoni nina furaha sana kuwaona watu wa Katiba hapa. Yangu ningetaka kuzungumzia kuhusu single mothers, yaani wa mama ambao wanapata watoto na pia hawana mabwana lakini wanapata watoto na pia hawana na bwana lakini wanapata watoto. Ningetaka kujua hawa watoto wana patwa aje? Na hawa watoto wanapatwa walee na nani? And yet hawana mababa zao, tungetaka Katiba ichukulie hatua kali sababu hawa watoto inabidii waandikwe maids, na wengine wawe ma street girl ama ma street boys, kwa hivyo tungetake kuchukulia mtu yeyote ataye weka msichana wa wenyewe mimba achukuliwe hatua kali yakulea huyo mtoto.

Tangu mimba ikiwa changa anatakiwa kumpeleka clinic tangu hapo mpaka mtoto akiwa mkubwa. Hapo imeleta shida kwa sababu ya kwamba utaona wanawake wanataka kuuza mtoto wetu wa kike ndipo hawa mabwana wana taka kuja hapa kusimama kuchukua mali. Na ina gawanywa kati kati na hakuwa ana anajua (inaudible).imetoka kwa hivyo hiyo tunaona itekelezwe vikali sana kwa sababu hiyo imekuwa ni mtindo wa hapa. Mtu akishika mimba bila bwana, bwana hataki kujitangaza anajiandikisha kwa Chief, ilu huyo mtoto atekelezwa na huyo mzazi, ili mama yake akifa huyo mtoto anaacha kuitwa yatima hali anaitwa mama kwa baba fulani, mtoto wa baba fulani lakini si mtoto yatima.

Pia ingine ningetaka kuzungumzia kuhusu sisi wanawake vile pengine wewe unabwana umefukuzwa ukifukuzwa utakuta umefukuzwa wewe na watoto wako unaambiwa uende nyumbani, wewe ukienda nyumbani pengine wazazi wako walikufa kitambo ukifika huko hauna makao, inabidi uende kitu inaitwa biashara haina licence, biashara inaitwa prostitution, na hiyo haina licence kwa hivyo hatutaki biashara kama hiyo, sasa inabidi watoto wetu pia wote tunazaa wanakua watukwa maid ama wanakuwa street girl kwa hivyo hiyo kitu tuaangalie kabisa.

Jambo lingine ni kuhusu kama sasa kuhusu hizi District mnao gawanya, mumeongezea ma District mengi sana ambae tunaona kama yana cost pesa nyingi sana, kwa sababu lazima kuwe na Chief katika District, lazima kuwe na D.C, D.O. ambao hivi District zinaongezeka na faida gani tunaona kama ni kuzorotesha uchumi. Kwa hivyo ningepomba Katiba itekeleze hivyo naona Katiba asanteni sana.

Com. Hassan: Thank you very much Monica, tafadhali unapiga signature hapo. Huyo alikuwa Monica Maina, sasa ni wakati wa Danson Mwangi, hayuko, Joseph Gikonyo, naona alikuwa na written submission, kama kuna wale walikuwa na written submission na wanaona (inaudible) tafadhali mutuachie hapa hizo submissions kabla hamjaondoka. Lucy Gucheru, Philip Kimani, Philip Kimani Yuko?

Philip Kimani: Niko.

Com. Hassan: Philip Kimani yuko.

Philip Kimani: Asante sana kwa majina kama mulivyosikia ni Philip Kimani, na niko hapa mbele yenu ili kuchangia kwa hayo maoni ya Katiba. Mwanzo ningependelea kutaja mojawapo ya hali ya tuseme biashara tunafanya hapa. Tunaomba (inaudible) sokoni, pengine kuna kitu una lima unaleta katika soko, hapa pengine tuna hakika kulima vitu vingi vikawa ikawa kutoa hapa kuelekeza mahali kama Mombasa ama kule mbele kutafuta senti ambazo zitasturi lakini ajabu ni kuwa Mwanakenya. Na hali ikiwa ni Mwana Kenya na hilo ni jasho lako ambako umefanya na mkono wako halafu uje utoe ushuru, ambao unaambiwa ushuru umezidi, na County Council wale ambao tuko nao hapa nafikiri katika hii Mpeketoni tumekuwa nao hapa nafikiri wametufanyia kazi kusafisha ama cleanliness ya hapa mjini, sasa imekuwa kila siku itabidi yule anauza hata kama ni kuku kuna shilling kumi na tano tunatoa je kwa mwaka utakuwa ni pesa ngapi?

Hapo awali wakati wa enzi za Mzee hayati nafikiri kulikuwa na off licences ambako tunatoa hata kidogo ile uweze ili uweze kujistarehe na hii biashara yako. Vile vile hawkers licence, hizo ilikuja ikapotelea kabisa sasa mimi ningeliza katika hii Katiba ambayo inaundwa upya, irudishe zile ambayo zilikuwa hawker licences ama zile hawker licences hata kidogo inatoa ili iliuniweza kuendelea biashara zako ziweke ili uweze kujimudu.

Ya pili ni kuhusu, katika hii Kenya yetu nafikiri kila moja atanipa mkono kama huku mauaji imekuwa mengi yasiyokusudiwa si ugonjwa. Tumewachana leo na wewe kesho msikie siko nimekufa na hii ni kazi yakuweza kutoshana pesa mimi natoa senti ili uondoleewe kulijana na mabishano kwa jambo fulani ama kibiashara ma kwa (inaudible) ...mimi ningepomba katika hii Katiba ambao inundwa upya, iwe macho ili tuweze kuweza kuondoa huu maafa haya yasiyo na njia ama yasiyo na msimamo.

Ya tatu ni kuhusu uhuru wa kuabudu, kusema kweli hii ni kitu imekuwa wazi kwa kila moja ambako anasikia kuabudu lakini kwa njia inginewapo ina kuwa sasa ni tumepata njia zinazoweza kukashifiana ama matusi inazidi, kwa hivyo katika hii Katiba ambayo inaundwa mpya ningepomba iwe na limit ya kuabudu ili tuweze kwamba standard yakuweza kuheshimiana kuliko kuwa tunakashifiana ama matusi na hali ni Kanisa. Asanteni.

Com. Hassan: Asante sana bwana Philip, tafadhali piga signature hapo. Josephat Kagunya, Mary Kibe, James Kariuki

James Kariuki: Kwa majina ni kama vile mumesikia ninaitwa James Kariuki mimi ni mkulima, hapa Mpeketoni. Mimi mazungumzo yangu ni kidogo ni kama imetajwa hapo mbeleni lakini ningesema kitu kidogo juu ya sector ya kilimo, Industrial sector na Public sector na Private sector ambaye hiyo ndiyo backbone ya nchi hii, tunajua katika Kenya miaka ya sabini na nyuma huko tulikuwa tunasome tunaambiwa katika nchi hii uchumi ya Kenya inategemea kilimo.

Ya pili inategemea tourism yaani wageni wanakuja hapa halafu kuna industrial sector ambayo hiyo ndiyo breeding ground ya

wafanyi kazi, yaani job creation, nafasi za kazi. Lakini kwa sasa tunasikia uchumi ya nchi it is rotten, ...(inaudible)... ambaye imeleta economic crisis kuharibu uchumi. Na hiyo yote kutokana na kosa ya kitu inaitwa integrity, yaani wewe umepewa kazi lakini hauna imani naye, kwa hivyo kitu kama hiyo kama Katiba ambaye sasa wengi hawajui hiyo nyingine inasema aje, pengine kuna kurasa kwa njia moja zaidi ya mia pengine na mbili ama tatu ama kumi ile Katiba, inaanza section I mpka mia moja na sitini na kumi moja nime sahu kidogo.

Lakini watu wengi hawajui section one inasema nini mpaka ya mwisho. lakini kwa kuwa wakati umefika watu ambaye wale hawakujua hii mambo ya masomo ya Katiba kama Civic Education, ambaye ya kusomesha raia Katiba ilioko ilikuwaje? Wengi hawakuelewa, hawajafikiwa kwa hivyo pengine kuna phrase ama kuna sehemu ambaye watu wengi hapa, hata hawakuelewa ni nini ilikuwa mbeleni.

Lakini sasa kwa kuwa wakati umefika mimi nikisema mambo ya kilimo tumesoma magazeti tumesoma dictionary vile uchumi imeharibiwa na watu ambaye wana uwezo wa kikazi, economic sabotage yaani kuharibu wa uchumi wa nchi ili watu wapate manufaa yao.

Katiba ya sasa ambaye inatayarishwa na wananchi na wasomi na wananchi pamoja, ihakikishe yeyote anaye pewa kazi, apewe kazi kulingana na uwezo wake, your ideas must be exploited, maarifa yako (inaudible) kila mtu ambaye yuko katika Agricultural sector, Public sector, na hii Private sector ambaye sasa zina kama industrialization, hii mambo, kiswahili sielewi sana kidogo.

Com. Hassan: You speak English?

James Kariuki: Hiyo kitu Katiba I protect mali ya wananchi pande ya industry.

Com. Hassan: kama uko na shida na kuongea kiswahili unaweza kuongea kiingereza ama hata Kikuyu.

James kariuki: Hata Kikuyu, anyway the problem,

Interjection: Laughter

James Kariuki: lakini sasa, saa zile tukisema in summary form kwa sababu watu wengi wanaongoja, mimi nisema kama sasa. Marketing ya ukulima, wizara ya kilimo ambaye wakulima wana.....

Com. Hassan: Tunyamaze tafadhali kidogo, tunyamaze

James Kariuki: wakulima wanatumia pesa nyingi kuendeleza kilimo na baada hayo hivyo vitu vinaenda to waste, sasa

unakuwa dictated na middle man. Zamani wewe unapeleka vitu yako soko market process ndiyo ina dictate price lakini sasa na ima hapa kwa mfano, cotton ndiyo kilimo ya juu hapa, mahindi lakini wakati ya kuuza sasa ndiyo inatokea middle man to control the prices of items.

Sasa hizo Katiba ya sasa inatakiwa iangalie sana mapato ya mkulima wa chini, small scale farmers, ili naye aweze kujimudu kimaisha. Kwa sababu hapa tukienda mambo ya bidhaa ya kilimo, pesa ghali, lakini ukienda kuuza hii kitu yako unaambiwa hii tutakutumia hii kwa hivyo Katiba ya sasa iangaliwe I address problem on the part of industrialization, upande ya ukulima na upande ya kibiashara, Private sector, hasa to create nafasi za kazi kwa watoto wetu. Katika Kenya nafikiri (inaudible) Kuna watu wengi wamesoma sana lakini wengi wame resort to criminal activities kwa kuwa alisoma alipata degree yake hakupata kazi, alienda Diploma hakupata kazi na anataka kujimudu kimaisha, lakini uchumi iliharibiwa ambaye angepata kazi, wale wenye kuandika hiyo Katiba kama ni industrial sector ipewe masharti gani itaendesha kazi yake, kama ni hiyo upande ya kilimo hiyo bidhaa zote mkulima wa kawaida na ile large scale farmers wawe wote wamekuwa incorporated, kuangalia soko ya mali yao, ili tusije kusema kama iliyo endelea kama America, unasikia unememployment 3%, London unememployment 2%.

Tax payers money hiyo ilindwe that is public finance, ilindwe ili inue hali ya maisha ya wananchi wote. Na vile vile ningependa hii Katiba ilimishi pande ya unity, yaani umoja, free association, yaani watu wakae kama wandugu hata kama wanatoka makabila yote. Isiwe ukionekana wewe ni Mkikuyu, siyo Mjalu siyo nini kama sasa hiyo ikingia ki ofisi hii haiwezi kuwa kwa sababu sasa watu watangalia laini yako, (inaudible) ukiwa ofisi unafanyia taifa kazi, kwa haya machache nimeshukuru sana.

Com. Hassan: Thank you very much. Tafadhali wale wanakuja tunataka mtoe mapendekezo, mtupatie recommendations ambaye mnataka iwe kwa Katiba siyo muanze kutupatia shida ambae zile ziko na ma story mingi, kwa sababu kile kitu tumekuja kusikiza ni kutoa maoni na mapendekezo, recommendations, so please make sure that you do that. Okay Samuel Mwangi, ni wewe?

Samuel Mwangi: Kuria Gikuyu, na Gethwairi Tonde.

Com. Hassan: Ngoja, mzee unaongea Kikuyu?

Samuel Mwangi: Najua Kikuyu hata Kiswahili najua,

Com. Hassan: Ngoja, nataka ku translate

Samuel Mwangi: rio nie na ndakena tondu nekokoro gakare Gatiba kekua, kindu kiria ngo'mwera ati ithewe andu aria maroweri weyathe ouo tuwena'guo nitwariganere.

Translator: Wale watu waliopigania uhuru, uhuru ambao mnayo.

Samuel Mwangi: tulisahauliwa, hakuna hata mtu hata moja tunapewa heshima naye, na nyinyi mnaona mfanyi kazi na hiyo ni sababu ya damu yetu, tulimwaga nyingi sana, mali yetu ilienda ika...(inaudible) lakini tunataka kukiwa namna hii muchunge hii Katiba ya kwanza mimi nikichangia maneno ile ina muelekeo,

Com Hassan: Interjection, put that one off.

Speaker: I have it off.

Com. Hassan: Okay.

Samuel Mwangi: mimi nasema hivi, kazi ya uchaguzi, nitachangia pahali ya uchaguzi, nataka kama uchaguzi (inaudible) Bunge invunjwa, inavunjwa kutoka juu mpaka chini, Rais naondoka kabisa, halafu kama wale wengine wabunge wanachukua baiskeli waende wakafanye campaign, hata yeye achukue baiskeli, lakini siwezi kuja na ndege ati uu anakuja ati ana kuja kufanya campaign anafanya hiyo ni Crown.

Ya pili Bunge ikivunjwa ule ataweza kusimamia ni Speaker ama ni Mkuu wa Sheria. Sasa hawa wengine wote wawe wanaondolewa, haya hiyo ni uchaguzi. Ya tatu tunasikia kwanza tunasema hivi, ya mbele tukumbukwe yaani wale watu walipigania uhuru maundike Katiba ya leo ikumbuke hawa watu sababu ya mbele, (audible) wale watakuwa wamewachwa wapatiwe heshima kidogo. Ya nne Katiba ikivunjwa Bunge na hata Rais aondolewe.

Ya tano mimi nimesikia mtu moja hapa akisema watu wale ma Chifu at tuwachaguage, Chief achaguliwe ni watu, huyu bado kumbuka ni nini hata hawa watu waliandikwa kama askari kwa sababu gani, tulikuwa tunachagua mbeleni siku ya Kenyatta. Tulikuwa tunawachagua lakini walitufanya upuzi sana wanakuwa mfisadi, wafisadi ukitaka kitu kwake ni mpaka pesa sababu wewe huwezi kumfukuza sababu alichaguliwa ni watu. Sasa kukaonekana afadhali waandikwe na Serikali, wakifanya vibaya anaondolewa kama askari. Lakini kuwa ati anachaguliwa ni watu.

Com. Hassan: Hiyo tumefahamu.

Samuel Mwangi: Ya sita tunataka hawa Katiba ya Kenya leo iandikwe wazee wakifikisha miaka sabini wakiwa wakiangaliwa na Serikali kama. . .

Interjection: Clapping and Laughter

Com. Hassan: Tafadhali mpatieni mzee Mwangi nafasi yakutoa maoni yake, tafadhali tunyamaze kidogo tumpatie nafasi analize muda wake.

Samuel Mwangi: Ya saba mimi ninamkata mwanamke moja alikuwa hapa anasema yule mtu anazaa yule mtoto angaliwe sana, yule mtoto watu wana fanya watu kama mbuzi, nakwenda na mwanamke anakuwa mimba unamtupa hata kumuona akuja kwako unam... (inaudible). Mimi huyo mtoto sasa hawa watoto wanakuwa wanahangaika. Sisi wazazi ndiyo tuna mzigo mzito sana, Kenyatta alikuwa anasema ukiwa mwanamke akikuambia huyo mtoto ni wako mpaka umlee huyo mtoto na kumsomesha, na kulikuwa kizuri sana, kulikuwa hakuna mambo kama haya iko sasa. Kwa hivyo hiyo Katiba yajengwe hivi vile ule mwanamke alisema kuwe namna hiyo muandike hivyo.

Com. Hassan: Okay sawa, asante mzee. Asante sana mzee Mwangi kwa hayo maoni yako. Naftali Kitonga, Wilfred Maina,

Wilfred Maina: Constitution Review Committee na wa Kenya wenzangu hamjambo? Sasa

Kwa jina ni Wilfred Maina na tumekuja na maombi kidogo hapa, kulingana na vile tulivionea Katiba yetu na vile ningependa pengine tufanye marekebisho. Kitu ya kwanza kwa Katiba ile iko, kweli kumekuwa na ... (inaudible)... kwa hivyo hapo hakuna mambo mengi.

Nguvu za Rais zipunguzwe, na katika hiyo kuwe na kunyanganywa kwa the two posts that the President is holding, that is Head of State and the Head of Government, yaani kiongozi wa nchi na kiongozi wa Serikali, hizo mambo mawili kwanza yatenganishwe, tuwe na kiongozi wa nchi ambayo ni Rais halafu kuwe na kiongozi wa Serikali. Kiongozi wa nchi ambayo ni Rais asiwe na chama chochote, halafu kiongozi wa Serikali ambaye ni Prime Minister awe amechaguliwa na wananchi na ana chama chake. Na kiongozi wa Serikali asikose Bungeni.

Kitu cha pili kuna huyu anaitwa sijui kwa Kiswahili, Controller and Auditor General, Controller and Auditor General kwa sasa anachaguliwa na Rais, kwa hivyo Controller and Auditor General anashugulikia pesa za Serikali na mambo kama hayo, kwa hivyo wakati huu katika hii Katiba tunataka kutengeneza, hii mambo ya ku appoint the Controller and Auditor General irudishwe kwa Bunge, Bunge iwe ndiyo itamu idhinisha Controller and Auditor General, ili kwamba maswali yote atauliza na Bunge ajibu kwa Bunge, lakini si kwa mtu moja binafsi. Yeye mwenyewe pia ndiye atapitisha matumizi ya pesa za Serikali, i.e. to approve the expenditure na hiyo pia ili matumizi hayo ya pesa za Serikali isifanywe na watu kadha au watu fulani, hiyo kupanga ratiba ama kupangilia utumuzi wa pesa za Serikali ambayo ni mambo ya budget ishugulikiwe pia na Bunge pamoja, ili isiwe budget inakuja kusomwa Bunge na hata wabunge hawajui ni nini hicho ambacho kimekadiriwa tayari. Kwa hivyo, Bunge pia ishirikishwe katika kuunda budget.

Kitu ya tatu Controller and Auditor General awe empowered that he can prosecute anybody who is accused of misappropriating the public finances, pesa ambazo zimekadiriwa kama mtu kweli amepatikana ako na makosa, amekashifiwa yeye awe na uwezo

wa kumshtaki halafu baada ya kuwa amemshtaki na huyo mtu amepatikana kweli, ushahidi uko kwamba alifanya makosa yakuvuja pesa, huyu mtu kusiwe na mambo ati ahamishwe hapana, afutwe.

Ya nne ni mambo ya Serikali za Wilaya that is the Local Authorities, kwa muda mrefu Serikali za wilaya zimekuwa pamoja na inashirikiana pamoja na Serikali kuu, kitu ya kwanza ningomba let us delink the Local Authorities from the Central Government, yaani tutenganishe Serikali za wilaya na ile Serikali kuu.

Serikali za Wilaya ni kama County Councils, Urban Councils na kama hizo, ili kwamba pesa ambazo sisi kama wanabiashara wa Mpeketoni tunalipa kwa Council hapa shilingi kumi na tano kila siku na zile zingine kwa wale wana permanent businesses kuna zile kiwangu inalipwa kwa mwaka, hizo pesa zisiwe kwamba ni shilling kumi na tano kila siku halafu kwanza hizo pesa zipelekwe na County Council sijui ziende zifanywe nini sijui zikaili kujulikane ni ngapi itatumika tena Mpeketoni.

Hii ndiyo tunalipa shilingi kumi na tano kila siku hata ile wheel barrow inatumika kutoa taka taka yenyewe hata haijiwezi, yule anaye patiwa hiyo kazi havezi kulipwa kwa nini sababu zile pesa zinatolewa hapa haziwezi kutumika kwa sababu ile enda. Zile pesa ambazo zinatolewa hapa zibaki hapa hapa kama ni makadirio yafanywe hapa hapa ile yale mambo ambayo inafaa kufanywa katikaya Mpeketoni yafanyike kuligana na vile inafaa. Isije ikawa uzito hata kulipa wale watu wanaofanya hiyo kazi. Kitu ya tano, Mayor achaguliwe na watu, the Mayor should be elected by the people not the Councillors. Mayor achaguliwe na watu.

Ya sita ni mambo ya Mahakama that is the Judiciary, Chief Justice and the Judges of the Appeal of High Court, yaani Judge Mkuu na Majaji wa Rufani na wengine kama ma Magistrate and all that wawe approved by the Parliament. Yaani Bunge ndiyo iwe itawapitisha siyo wawe watachaguliwa na Rais. Mahakama ifanye kazi ikiwa huru, the(inaudible) Separation of Powers.

Mambo ingine ni uchaguzi, Commission and the Commissioner of the Electoral Commission should be approved by the Parliament, isiwe ni Rais anafanya hiyo kazi. Halafu kwa maoni yangu nilikuwa nimeona the ballot boxes ambazo tunatuma hizi za chuma sijui ziko vipi, kwa maoni yangu naonelea let us try and use the transparent ballot boxes.

Nikiingia kwa upande ile ya Katiba ile tuliyoko naye kwa sasa, lugha iliyotumika katika ile Katiba tuliyo nayo sasa ni lugha ngumu kweli, nilikuwa na jaribu kupitia katika Kenya, kwa kweli kuna maneno inatumika magumu sana, nikajaribu kufikiria maana nilipogunduwa katika hiyo kitabu kuna kama misdemeanor penal code wanayoitumia, nikajaribu kufikiria maanake nikiona siwezi kupata I have never heard such a word. Nilipoenda katika ile (inaudible) maneno yametumika nina jaribu kupeana ili neno misdemeanor wanasema kwa definition it is (inaudible) mistake that is confers to be misdemeanor, sasa hiyo, haikupatii ni nini, wewe ni nani mimi ndiye (inaudible), kwa hivyo ile lugha inayotumika wacha nielezwe ili kwamba hata mtu anayesikia hiyo Katiba kwa mara ya kwanza atajua hii section inaongea juu ya hii.

Ya mwisho nikimalizia ni kuhusu Natural Resources, mali ngapi, tumesikia mambo mengi sana kuhusu msitu, Karura Forest na kule kwingine kote, at least tulikuwa tuki (inaudible), msitu yetu inaharibiwa kila wakati sasa hii shida itatokea na hatupati solution. Kwa hivyo kile maoni yangu nimeona let the Parliament itself formulate a policy for the management of the Natural Resources, Bunge enyewe iwe ndiyo itatuandikia sheria za vile mali ngapi tuliyonayo hapa nchini, kama ni madini, kama msitu kama ni chemi chemi za maji na kila kitu, wao ndio watatoa ratiba na sera za vile (inaudible)...itatumika ili kwamba kusiwe na wengine watatumia kama ni yao, kwa hivyo asanteni hiyo ndio maoni niko naye.

Com. Hassan: Okay thank you very much. Anne Nguru, Christopher Moki, hayuko, Kenneth Githinji, Susan Gaitho.

Susan Gaitho: Mimi kwa majina naitwa Susan Gaitho ningetaka kutoa maoni yangu kama yafuatavyo. Maoni langu la Kwanza ni kuhusu mambo ya Electoral Commission, tungeomba kuwe kuna Tume huru yakusimamia uchaguzi ndio tupate uchaguzi wa haki ambako tutakuwa tunaridhika nao.

Ya pili pia ningeomba wakati wa uchaguzi tuweze kupata ballot boxes ambazo ni transparent kwa sababu kumekuwa na shida nyingi sana, watu wanasema hizi boxes tunaletewa mara ni za mbao sijui ni chuma, ni nzito ambako huwezi kuelewa kama kuna kitu zingine zimetiwa ndani, kwa hivyo tunakata kitu ambacho ni transparent ambako mtu wa kwanza akianza kupiga kura atajua mimi ndiyo wa kwanza nimepiga kura ya kwanza.

Inginge pia nimeambiwa kwamba katika ile Katiba ilioko sasa kuna uhuru wa kuabudu, katika hiyo mambo ya uhuru wakuabudu, mimi ningeomba katika Katiba mpya kuwe kuna limit of worship kwa sababu imekuwa vile kumekuwa na uhuru wakuabudu watu wamaendelea mpaka ikabidi mumefika kiwango cha kuabudu sheitani mpaka inafika inakuwa ...(inaudible)...kula binaadamu, kuna human sacrifice zinatolewa katika kule kuabudu mashetani, kwa hivyo tungeomba kuwe kuna kiasi kile cha kuabudu.

Na pia ikiwa watu wengine wanaabudu kama ni sect fulani iwe inachunguzwa kabisa kwa sababu munaona kikundi kama cha Mungiki wanajiita ni sect fulani watu wa makanisa ambako ukiangalie kile kitu wanafanya kama kutoa wanawake nguo yaani mtu amevaa mini skirt, sasa unashindwa mtu akiwa amevaa miniskirt and sasa zile umemtoa amebaki uchi what is bad, si ni hiyo umemtoa nguo ukamwacha uchi, sasa unaona ile mambo wanafanya pengine sasa wakimkuta mwanamke njiani wanaanza kufanya mambo ya tohara kwa lazima mambo kama tunaona yaani mambo yakuabudu iwe ina kiasi yake.

Pia mambo ya kitambulisho tunaona wengi wana Kenya unaenda kwa Chief kuchua form kama yakuchukua kitambulisho mara ukienda kuandikisha kitambulisho unaambia ulete kitambulisho cha baba yako, ukisha leta kitambulisho mara unaambiwa ulete certificate, ukisha leta hiyo unaambiwa ulete birth certificate, sasa na hiyo yote inaonyesha kama baba yako akipewa kitambulisho yeye si mKenya? Inahitaji nini ingine wewe upewe kitambulisho, ikizidi ikifika ni wakati wa kusafiri kwenda

ngambo watakiwa Passport, unaweza kusumbuliwa unaweza kuambiwa wewe waenda kwa nani? Leta barua ya invitation, unaanza kusumbuliwa mambo mengi hali wewe ni mwana Kenya na unataka pengine kwenda for further studies uje uendeleshe nchi yetu vyema. Sasa tunegeomba kama ni wakati wa kupeana Passport at least kuwe na laini ambao iko easy ya mtu kupata hiyo Passport. Mtu asije anasumbuliwa. Watu wengine wanasumbuliwa mpaka ile ni masomo wanaenda ina bidii waiache.

Pia tunegeomba mambo ya decent salary, katika hii Katiba mpya tunegeomba kuwe na kipengele. Kitasimamia mambo ya mishara kuhakikisha kwamba wafanyi kazi wanapata mshara yakuwatosha kwa sababu tunaona kama ni askari wetu wanapewa mshara kidogo na huyo askari kama anafanya kazi hapa Mpeketoni pengine kwao ni Nyanza, huyo askari una expect family yake iko Nyanza ita exist na ile mshara kidogo anapata na yeye huko, yuko peke yake huku, sasa inambidi yule mfanyi kazi ile pesa anapata inakuwa ni ndogo, hata akituma nyumbani na yeye anabaki huku hana pesa za kutosha, inabidi mpaka akiona gari ikipata asimamishe mpaka aandike hile gari, apate kitu kidogo.

Sasa ndiyo kuzuia ile mambo ya kitu kidogo, mtu apewe mshara yakumtoshea. Kama ni ofisini ukienda unaambiwa kama pengine wataka kama Passport unaenda unaambiwa njoo kesho, njoo kesho kutwa, kama yule mtu angekuwa na mshara yakutoshea haswa hangekuwa anakusumbua hivyo, ungekuwa unaenda lakini kwa sababu mshara hautoshi, mtoto wake anataka asome vizuri, anataka bibi yake avae vizuri, inambidi mpaka akuitishe kitu kidogo.

Pia tena nataka kuzungumzia mambo ya kina mama, hayo yamezungumzwa sana na wengi, kina mama na watoto, si unaona kama sasa kuna watu wengi unakuta single parents ni wengi sana. Sasa unakuta mtu pengine uliolewa umepata watoto wanne, watano au watatu, bwana amekutupa yeye ameona manyaga mwingine huku ameanza kushine nayo, wewe utakuwa umeezeka kadi zake zinatupwa. Sasa inafika wewe unanzigo watoto ni wako, bwana hataki kusikia mambo ya watoto. Sasa tunegeomba katika Katiba mpya kuwe (inaudible).....kusimamia hayo mambo, kuhakikisha kuwa bwana akimuoa bibi hata akimuacha wale watoto ni juu yake. Kwa sababu hiyo unafanya hata kama ni wewe bwana hata kama unataka kuoia bibi watano lakini utakuwa na(inaudible) watoto kwa sababu utajua nili zaa na fulani wangu, wale nilizaa na fulani wako juu yangu. Huwezi kulea watoto ishirini kwa hivyo itakubidi uzae watoto ambao utajua utaweza kulea. Asanteni.

Com. Hassan: Thank you very much Susan. Rueben Karanja,

Rueben Karanja: Kwa jina mumesikia Rueben Karanja – Councillor Magarini Ward. Mimi kwa maoni yangu kuhusu Katiba mimi nina machache kwa kuwa mengi naona yameongewa, ya kwanza ningependa kutoa pendekezo kuwa Serikali iwe ikiundwa na vyama vyote, iwe ikiundwa na vyama vyote na ugawaji wa ma Minister utegemeo kuwakilishwa vile chama kimeakilishwa Bungeni. La pili ningependa kutoa maoni kuhusu, tafadhali naona sioni vizuri, lakini ningependa kuingia katika uchaguzi. Mimi ningependa katika uchaguzi kuu uwe baada ya miaka mitano. Upande wa Rais nao ningeingia ningependa Rais awe na mihula miwili tu, ilo lingine ningependa Rais awe akipita na kura zaidi ya 50%. Hapo pengine nako ningependa Bunge, Mayor, Diwani wawe wakipita na kura ilio juu ya wenzio ile ameshinda wengine nayo.

Hiyo lingine ningeonelea qualification, qualification Rais awe ana degree au ametimu masomo ya chuo kikuu, naye pia Mbunge ningeonelea awe ameanzia form 4 nakuendelea. Na Mayor pia ningeonelea awe na form 4 na kuendelea qualification. Naye Diwani ningeonelea awe na kujua kusoma nakuandika kiswahili na kiingereza.

Hapo kwingine nikiendelea nikionelea ningependekeza au ningeonelea campaign iwe huru popote pale mgombea anaye husika kama ni Rais awe uhuru kugombea nchini yote, hapa mjini kote, ikiwa ni Mbunge Constituency yake awe na uhuru wakuenda mahali popote kwa vile mambo yataongowa ndio naenda haraka, haraka.

Hapo pengine ningeonelea utawala, wale wako katika utawala kuanzia P.C., D.C., D.O, Ma Chief Ma Assistant Chief wawe wakichaguliwa na wananchi kuna tofauti ikiwa mtu ajachaguliwa na wananchi(inaudible) kidogo ingekuwa ni vyema wawe wakishirikishwa katika kuchaguliwa na wananchi.

Hapo pengine nikiendelea ningeonelea Rais awe akitengemea Bunge kwa uwezo wake wote awe anategemea Bunge na awe na mamlaka tu ambavyo ni yakusimamisha mambo ambavyo inangoja idhini ya Bunge, lakini lolote lile atafanya liwe linaongewa na Bunge na ina idhimishwa na Bunge. Hapo pengine ningependekeza, Mayor au Chairman wa Council ategeme uamuzi wa kikao vya madiwani au nafasi yeyote au full Council ya mji au ya wilaya. Sasa au pengine ningependa kutoa mapendekezo Mahakama, kesi ikiwa katika Mahakama isizidi miezi sita na ikiwa itazidi miezi sita iwe na sababu kamili na iwe imetolewa hiyo sababu kwa njia iliyo sahihi.

Hapo pengine ningependa kuongezea kuwa Bunge iteue kundi ya kuajiri watu wa idara zote, Bunge iwe ina teua body ya kuajiri watu wa idara zote, kusiwe na watu wanaajiriwa na watu au uwezo wa mtu. Hapo pengine ningependelea kusema kila idara iwe ikisimamiwa na Minister ambayo anaweza wa kutoa directive ya Idara yake. Hapo pengine ningependa kusema kila idara iwe na Councilor yake ambayo iikiukiwi na mtumishi mfanya kazi katika idara hiyo. Hapo pengine ningependa kusema mwananchi awe na uhuru wakukaa popote atakapo au kuzalisha mali popote pasipo kipingamizi.

Com. Hassan: Jaribu kumaliza, wakati wako umemaliza, jaribu kumaliza.

Rueben Karanja: Asante, sasa hapo pengine ningependa kupendekeza upande wa kilimo, kilimo kilindwe na Serikali kwa ku import vitu kutoka nje au ku export vitu, iwe ni vitu ambavyo kinasaidia kilimo lakini siyo kua kilimo. Hapo pengine ni kukata kata kwa vile mambo yameongewa sana. Hapo pengine nikimalizia ningependa kupendekeza mishara iwe inategemea uchumi wa nchi. Kuna mambo ambayo tunaona katika assessment ya nchi inakuwa matatizo munaona mtu mwingine anadai mshahara ya mia moja na ishirini bali kuna mtu mwingine ana shilling elfu tatu katika idara hiyo hiyo, hiyo assessment tunaona inataabu sana kwa maana wale watu wanatumia vitu ambayo wana nunua sawa sawa kwa maana ngano ni sawa, sukari ni sawa na vitu vinginevyo ni sawa. Sasa hapo pengine yale ningengea imeongewa kuhusu merit kuhusu ni hapo ningependa kutoa

pendekezo hizo asante.

Com. Hassan: Asante sana mzee tafadhali tupigie sahihi na hiyo barua nafikiria utatuwachia, hiyo barua utatuwachia. Our next person is..tunatarajia kufunga kikao saa kumi na nusu kwa hivyo na tumesikiza watu wengi, ikifika saa kumi tutakuwa tukifunga.

Bw. Peter Ngugi yuko?

Peter Ngugi: Kwa jina ninaitwa Peter Ngugi na nina maoni yafuatao, kulingana na shida tulizo nazo katika nchi yetu kuhusu migomo, kwa ajili ya mishahara ya wafanyi kazi na ningependekeza ya kwamba katika Katiba hii ambayo tunaandika wakati huu ili kuondoa migomo hii mishara inaotolewa kwa wafanyi kazi wote itolewe sawa kulingana na kiwango cha elimu na pia wale wanapata mishara minono wawe na maduka yao watakao nunua vivaa vyao katika maduka hayo kwa bei ghali kwa sababu wanapata mishara nikubwa. Hao wanao pata mishara midogo wanunue katika maduka haya ya kawaida na uwe na kibali yakuonyesha kwamba unapata mishahara aina gani. Kwa sababu mtu akisema hivyo kwa sababu Serikali imeshindwa kuongeza mishara, lazima nasi tutafute mbinu ingine yakushika Serikali.

Jambo lingine, oni la pili ni kwamba uhuru wakuabudu, Katiba ya sasa haijafafanua vizuri ni nani anafaa kuabudiwa katika nchi hii yetu, ni ule uhuru tu iwachiliwe mtu abudu leo hii nikiamua kwamba katika ibada yangu nitakuwa nilika vichwa vya watu watano ndio ibada yangu yakutoa tabibu yangu Katiba ya leo haijakataza chochote, kuchinja watu watano upate vichwa ufanye ibada, imagine nikiwa na washirika wangu elfu moja kila siku ni vichwa vingapi vitakwenda. Kwa hivyo Katiba ya sasa ifafanue ni Mungu gani au ibada hii itafanywa namna gani, kwani wakati huu ni uhuru tu wakuabudu maana tumepata mashetani watu wanao ua watoto na nini na mambo kama haya. Kwa hivyo Katiba ya sasa ifafanue vizuri katika nchi yetu tutakuwa na watu aina gani au tutakuwa tukiabudu nmana gani?

Pia kura za kila eneo hii imetajwa lakini pia mimi ningependekezo zihesabiwe kama ni hapa kwetu Mpeketoni zihesabiwe siku hiyo hiyo wabebe idadi ya zile kura sikubeba kura na masunduku, ni kipi raisi kubeba kura au kubeba idadi? Idadi, kwa hivyo ifanyiwe hapa na (inaudible).

Jambo ingine, Wizara zifuatazo katika Katiba hii zitiliwe mkazo sana, au zitengewe pesa za kutosha, wakati tulipata uhuru, wale waliotuongoza katika uhuru walisema ya kwamba wanakuja kuondoa ujinga, maradhi na nini ingine? Na umaskini. Na mambo haya ndio uti wa mgongo wa nchi hii. Elimu, Serikali itenge pesa nyingi zakutosha katika budget hii kuhusu elimu ili ipate kununua vitabu, na vifaa vinavyo takikana kwa watoto. Katika afya madawa yawe free, siyo kama sasa tunaona hii shilingi ishirini, na hiyo shilling ishirini mzee kama huyu pengine hana chochote, na pengine hajala kitu tangu asubuhi na amepata ugonjwa saa hii, akienda pale aitishwe shilingi ishirini, katika afya madawa, operation kule kwenye theatre iwe free na pia kupiga picha iwe free, kwa sababu hii ndiyo imeumiza wananchi sana..

Agriculture pia, hiyo pia itengewe pesa zakutosha na wakulima ili waweze hiyo pesa zitakazo tengwa si za kununua magari

makubwa au nini bali kutunulia ma fertilizer na madawa na mbengu za ku saidia wakulima ili uchumi upate kuinuka, kwa sababu hilo ndio uti wa mgongo wa nchi hii katika uchumi wenu. Na Katiba ifunzwe mashuleni kutoka Primary hadi University.

Serikali pia itenge pesa kwa wazee wakongwe na waweze kuwekewa miaka ni miaka gani, kwa mfano mzee, hata biblia yenyewe inasema hivi, hata biblia wale wanaitwa wajane ni wale wana miaka sitini hapo kwa hivyo wale wazee wa miaka sabini, wa mama wa miaka sabini pamoja na wale walemavu, watengewe pesa kidogo hata kama watakuwa kila mwisho wa mwezi wanaenda pale kwa benki wanachukua shilingi elfu mbili wanajisaidia hiyo itakuwa imewasaidiya sana hawa wazee ile kwa sababu sisi tunaona yule ambaye anasaidia sana walemavu waze ni Catholic tu, Catholic inazunguka kila siku na gari katika nchi yetu kuwasaidia, kuwapatia mikebe ya unga miwili mitatu. Lakini Serikali yetu je huyu mzee akienda kuuza korosho, akiuza pamba anakatwa taxed, lakini hapewi kitu kwa hivyo Serikali itenge kitu kama hiyo.

Pia Bunge nchi yetu, nchi zingine kama Tanzania, wakati wa taarifa ya Bunge huwa inazungumzwa moja kwa moja, mimi pia ningependekeza na kuunga mkono yule amezungumza hapa ya kwamba iwe ikizungumzwa Katiba ya sasa ipitishwe Bunge, iwe ikizungumza moja kwa moja kila moja anasikiza kwa lugha ambao inaeleweka asante.

Com. Hassan: Thank you very much Mr. Peter Ngugi, after Peter Ngugi we have Khadija Bashir, Khadija ametoa, Amos Waweru.

Amos Waweru: Kama vile umesikia majina ni Amos Waweru ni Chairman – Mpeketoni. Ningetaka kutoa maoni yangu kwanza kuhusiana na education, education katika District ambayo tumeona katika Kenya yetu kuna kitu kimekuwa kina babaisha watoto wengi sana, mean score, mean score katika ujinga wa kutoa mtoto kutoka chini mpaka kumuendesha mpaka pahali ambapo atafuata na akili zake na kujua masomo, mean score ingine imepata watoto wetu wakaacha mashule.

Kuna District ingine tunataka kuiga mfano wa District mengine kuhusiana na elimu ama maendeleo pale imeanza Nairobi, na kama Lamu yetu, sisi watoto wetu wametoka wanalinda wanyama, msituni ama nini lakini utapata officer ambae yuko hapa anataka kufananisha ama kuiga mfano wa Nairobi, utaona watoto wengi wanarudishwa katika mashule wana ambiwa hamja fika hata standatd 7, standard eight kuenda kule ukifika pale ile mean score wanataka kuiga ile mfano unaona school mean score inakuwa District unasikia kama Lamu juzi ilikuwa namba ishirini lakini hiyo tech ambazo watoto hivi wamewacha shule sababu yakurudishwa kurudishwa wakaona hapana, wengine wanaachishwa katika (inaudible)...kwa hivyo hii Katiba ikija za mtoto ili apate certificate yake akimaliza, atoke standard one mpaka standard 8 afanye mtihani wake kama ni kwenda aende akifaulu apite kwa vyuo vingine.

Lingine tunaenda hapo kwingine ni Police katika sehemu zetu za Kenya. Katika Kenya utaona ukishikwa kama wewe unatembea tembea umetoka katika safari zako, uningizwa cell, wewe ni innocent huja fanya chochote, lakini umeshikwa, lakini

ukishikwa kwenye cell unakuta mtu ni mwenda wazimu mwingine ni muuaji, kama ile ya Thika unakuta pengine waliuliwa ndani ya cell na wewe ulikuwa pale pale umeshikwa tu kwa njia ya muda kwa hivyo ningetaka Katiba ambayo iko hapa, wale innocent ama mtu ambae haja fanya makosa mengi makubwa na kwa vile wameona katika polisi, wampatie ile inaitwa Bond atoke na aitwe kwenye Court hiyo ni ingine.

Naendelea soko huru katika marketing ya vitu vyetu. Kulingana na vile vijana (inaudible) uchumi zimezoroteka unasikia katika maredio kwamba hakuna Kenya imeharibika katika uchumi. Vijana wengi sana wamesoma wamehitimu wamekosa makazi wamerudi mashambani especially area within Mpeketoni, hivi sasa wale vijana wakifanya ile kazi yakulima mazao yake watakuza katika mashamba kuna toka kuna wafanyi kazi ambao wamewekewa, zamani tulikuwa tunaona ukianzisha biashara yako kulikuwa na control price, hii soko huru ilikuwa ni mambo ambao imeletwa kutoka kuiga mambo ya ngambo lakini sasa nimeona imetulemea.

Hivi sasa sisi ambao ni wafanyi kazi au wana biashara wadogo wadogo, soko huru imetuweza kwa sababu unakuta mfanyi kazi ambae amepatiwa wholesaler, yeye ndio anauza wholesale the same time yeye ndio anauza retailer, sasa katika ile biashara yake kwa sababu ana uwezo yakuenda Mombasa ama wapi anakuja anauza, ametuuzia ile kitu na wholesale halafu mimi mteja ambae nakuja kununua sukari kilo moja ananiuzia na the same price ya wholesaler, sasa mimi niki nunua vitu vyangu ninaenda mashambani hakuna mtu ataweza kuja kununua vitu hizo anajua pale vitu vinauziwa rahisi. Kwa hivyo soko huru tunaona Katiba imetunyanyasa katika huo.

Haya vyombo vya kutangaza katika wakati kuna vipindi vya Rais ambao wanafanya campaign katika Jamuhuri yetu ya Kenya tumeona tu ni Rais ambaye anatawala katika nchi wakati campaign imeendelea, lakini vyama vingine ambavyo vimewakilishwa na ma Rais wengine wakifanya campaign katika mikoa yetu ama District zetu, hatujaona katika Runinga kwa hivyo tungetaka hivi sasa ile KBC iwe independent na isiwe ya Serikali, iwe ni runinga ya mtu yeyote ambaye anafanya campaign kama mzee mwingine aliingia hapa anasema ndege inakuja ni kweli? Moi huja na ndege ama Serikali, ule Rais anakuja na ndege lakini ule mwingine kama wale wako katika vyama vingine hawatumi vile vitu vya kazi vya Serikali kwa hivyo tungetaka hawa ambao wanafanya siasa wawe (inaudible) .Kama ni Rais wakati vyama vimevunjwa Bunge wote wawe katika(inaudible) .moja kusiwe kuna mtu ambayo anapendekezwa huyu yuko katika under Government na huyu yuko katika raia, hiyo tungetaka tuangalie ingine.

Tungetaka kusema kwamba katika hii nchi yetu kuna mababu wetu ambao wamefariki lakini kuna wazee wa mitaa na tunaandikia sisi ambao tumshirikwa Kenya hii. Tuna sikia kwamba watu walipigania tukawa na uhuru, lakini nchi yetu tutaenda kumuona kuna mtu moja tu unaweza kumuona ana acre elfu moja licha hivyo, kuna watu wengine wako Mathare katika mini valleys utaona wana mito, mito wamejenga makaratasi na babu zao ama wazazi wao walipigania uhuru. Hawa watu kwa nini hawakufikiriwa ...(inaudible) mtu moja awe. Kwa hivyo ninapendekeza above 18 years mtu yote yuko Kenya na kuna nchi nyingi kubwa ukiingia kwenye gari mpaka Nairobi kuna nafasi nyingi ambako watu wataweza kuishi tungetaka mtu ambaye

yuko above eighteen years apate ardhi hata ni ka piece kidogo tu awe akijivunia katika nchi yake.

Katika political affairs ningetaka kusema kwamba katika nchi yetu tulipitisha kuwe na vyama vingi, lakini hivi vyama vingi tunaviona tunataka anga katika Katiba hii tunayo kama ingewezekana na wawe wanani sikia tuwe na vyama vitatu, tusiwe na vya viwili lakini zaidi ya vitatu vitakuwa hazituletei mwangaza mzuri.

Pia tungetaka political party, hawa watu wanaitwa Mayor, Chairman wa County Council, kama District Chairman, tungetaka Urban Council awe anachaguliwa na sisi wananchi ambao tunaketi tunajua tabia zake na tuna ndio ufisadi unaingia katika hizo, kwa County Council unasikia kuna ufisadi mwingi. Kwa hivyo tunaka huyo mtu na tuwe na mandate yakumtoa na akionekana ameenda kombo.

Com: Hassan: Malizia haraka

Amos Waweru: Okay, ningetaka Bunge lenyewe, nalo lipatiwe uwezo especially ku-appoint Judge mkuu wa Kenya. Rais asipatiwe mamlaka yaku chagua Jaji mkuu ili tuwe na usawa katika Judiciary. Nafikiria hapo ndio nitasimamia yangu na asante sana, nashukuru.

Com: Hassan: Ngoja kidogo, ngoja kidogo Commissioner ako na swali.

Com. Dr. Musonik: Nimekuwa nikiuliza swala moja kila siku (inaudible) ni tatu sasa kuna kama hamsini itakuwa vipi?

Com. Hassan: Anakuuliza kile critetaia yakurudisha iwe tatu

Amos Waweru: kulingana na mambo nimesema vyama vitatu ni sababu kuna vile vyama ambao ni kikuu ambao zina katika mchoro, katika Kenya tunajua chama ki kuu ni kipi, chama second ni kipi na kingine, hizo vyama kama tungeziweka tufaanyiwe maoni ya wananchi, tungependekeza tuwa na vyama vitatu kwa maoni ya wananchi iletwe background kama tungetaka vyama vitatu ama vipi?

Com. Hassan: Okay Asante. Mwangi Daniel, ni wewe? endelea

Mwangi Daniel: Asante sana.

Com Hassan: Tafadhali tunyamaze.

Mwangi Daniel: Yangu tu ni maoni kuhusu hii Katiba au Serikali yetu. Sasa kurekebisha Serikali yetu mwanzo lazima tujue

